

KANISA LA YESU KRISTO LA WATAKATIFU WA SIKU ZA MWISHO • APRILI 2013

# Lahona

**Yesu Kristo: Mkombozi na  
Mfano, uk. 18, 26**

**Marafiki ni Watu Ambao . . . , uk. 52**

**Je, Umeongoka? Njia 10 za Kujua , p. 56**

**Kuzungumza juu ya Hekalu pamoja na  
Watoto Wenu, pp. 62, 64**



*"Mwangaza  
wa Kristo ni  
ule uwezo  
mtakatifu au  
ushawishi una-  
oenea kutoka  
kwa Mungu  
kupitia Yesu  
Kristo. Hutoa  
mwanga na  
uzima kwa  
kila kitu."*

Mzee Richard G. Scott wa  
Jamii ya Mitume Kumi  
na Wawili, "Peace of  
Conscience and Peace  
of Mind," *Liahona*,  
Nov. 2004, 15.



## JUMBE

- 4 Ujumbe wa Urais wa Kwanza: "Amelefufuka"**  
Na Rais Henry B. Eyring
- 7 Ujumbe wa Mwalimu Mtembelezi: Maagano ya Hekalu**

## MAKALA YA CHAPISHO

- 12 Kifo na Maisha: Mtazamo wa Watangulizi kuhusu Ufufuo**  
*Watangulizi na manabii wa mapema wanashuhudia kupata matumaini katika ufuluo.*

## 18 Misheni na Huduma ya Yesu Kristo

Na Mzee Russell M. Nelson  
*Tunaweza kuiga maswala matano ya maisha ya Mwokozi tunapotaka kumfuata na kuelewa Upatanisho Wake.*

## 26 Wiki ya Pasaka

*Katika wiki ya mwisho ya maisha Yake, Mwokozi alitenda muujiza mkuu wa yote.*

## 30 Kuwasaidia Watoto Kujitayarisha Kubatizwa

Na Jessica Larsen na Marissa Widdison  
*Ni nini wazazi wanawenza kutenda ili kufanya ubatizo wa mtoto wao kuwa na maana zaidi?*

## 34 Vutiwa kwa Hekalu

Na Mzee Jairo Mazzagardi  
*Jifunze jinsi hekalu linawenza kusaidia kuleta uongofu.*

## IDARA

- 8 Daftari ya Mkutano Mkuu wa Aprili: Kujifunza Hotuba za Mkutano Mkuu Pamoja**  
Na Greg Batty
- 9 Kufundisha Kwa Nguvu ya Vijana: Umuhimmo wa Marafiki Wazuri**
- 10 Kile Tunachoamini: Roho Mtakatifu Hufariji, Huvuvia, na Hushuhudia**
- 36 Sauti za Watakatifu wa Siku za Mwishi**
- 74 Habari za Kanisa**
- 80 Mpaka Tutakapokutana Tena: Kunywa kutoka kwa Chemichemi**  
Na Aaron L. West

## KWENYE JADALA

Mbele: Kielelezo kwa Picha na Tim Taggart  
© IRI. Nyuma: Kielelezo kwa Picha na Matthew Reier. Ndani ya jadala la mbele: Picha na Kristine Šumska.



40

**40 Kuchagua Sehemu Bora**

Na Matthew D. Flitton

*Ili kujipa sharti kikamilifu kwa injili ya Yesu Kristo, ilimbidi Zoltán awache vitu fulani vizuri.*

52

**42 Maswali na Majibu**

*Je, ninawezaje kueleza rafiki yangu kwa nini kuvunja sheria ya usafi wa kimwili ni wazo mbaya?*

**44 Jinisi ya Kuhudumu****Katika Wito wa Ukuhani**

Na Rais Thomas S. Monson

*Jifunze msingi wa kufikia, kufundisha, na kugusa maisha ya wale unaowatumikia.*

**45 Nafasi Yetu****46 Mbona Tunahitaji****Kitabu cha Mormoni**

*Sababu nne Kitabu cha Mormoni ni muhimu.*

**48 Ukuaji katika Udongo wenyewe****Rutuba: Vijana Waaminifu Nchini Uganda**

Na Cindy Smith

*Wavulana na wasichana hawa wanaimarishwa kwa kujitolea kwaajili ya injili.*

**52 Kwa Nguvu za Vijana:  
Je, nani Rafiki wa kweli?**

Na Elaine S. Dalton

**54 Ninajua Vipi: Mwaliko wangu wa Wokovu**

Na Emerson José da Silva

*Wakati hatimaye nilikubali mwaliko wa rafiki yangu, nilijua kuwa nilikuwa nimepata kitu cha muhimu.*

**56 Njia Kumi za Kujua  
Kuwa Umeongoka**

Na Tyler Orton

*Kile nilijifunza kuhusu uongofu hunisaidia kufuatilia maendeleo yangu katika injili.*

**59 Bango: Kazi Ngumu  
Inaistahili Sana**

*Ona kama unawezaku-pata Liahona iliofichwa katika toleo hili. Kidokezo:  
Tumia macho yako ya ushujaa.*



61

**60 Mmisionari Mdogo  
wa Bibi Deny**

Na Emilia Maria Guimaraes Correa  
*Upendo wa Vitor wa injili ulizua uongofu wa bibi yake.*

**61 Mashahidi Maalum: Kwa nini  
Kanisa Lina Jina Refu Hivi?**

Na Elder M. Russell Ballard

**62 Kusherekea Mahekalu!**

Na Darcie Jensen

*Duniani kote, watoto husherehe-keea kuwa na hekalu karibu nao.*

**64 Maswali na Majibu ya Hekalu**

*Majibu kwa maswali kama vile,  
Kwa nini tuna mahekalu? Nini hufanyika ndani yao?*

**65 Muziki: Familia Zinaweza  
Kuwa Pamoja Milele**

Na Ruth Muir Gardner  
na Vanja Y. Watkins

**66 Kuleta Mafundisho ya  
Msingi Nyumbani: Yesu Kristo  
Alirejesha Kanisa Lake katika  
Siku za Mwisho****68 Kwenye Mapito: Mahali  
Kanisa Lilianzishwa**

Na Jan Pinborough

**70 Kwa Watoto Wadogo****81 Picha ya Nabii:  
Wilford Woodruff**

Jarida la kimataifa la Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho

**Urais wa Kwanza:** Thomas S. Monson,  
Henry B. Eyring, Dieter F. Uchtdorf

**Jamii ya Mitume Kumi na Wawili:** Boyd K. Packer,  
L. Tom Perry, Russell M. Nelson, Dallin H. Oaks, M. Russell  
Ballard, Richard G. Scott, Robert D. Hales, Jeffrey R.  
Holland, David A. Bednar, Quentin L. Cook, D. Todd  
Christofferson, Neil L. Andersen

**Mhariri:** Craig A. Cardon

**Washauri:** Shayne M. Bowen, Bradley D. Foster,  
Christoffel Golden Jr., Anthony D. Perkins

**Mkurugenzi Mkuu:** David T. Warner

**Mkurugenzi wa Usaizidi wa Familia na Washiriki:**

Vincent A. Vaughn

**Mkurugenzi wa Majorida ya Kanisa:**

Allan R. Loyborg

**Meneja wa Biashara:** Garff Cannon

**Mhariri Mtendaji:** R. Val Johnson

**Wasaidizi wa Mhariri Mtendaji:** Ryan Carr,

LaRene Porter Gaunt

**Msaidizi wa Uenezi:** Melissa Zenteno

**Uandishi na Uharii:** Susan Barrett, David Dickson,  
David A. Edwards, Matthew D. Flitton, Mindy Raye  
Friedman, Lori Fuller, Gary H. Garff, Jennifer Grace Jones,  
Hikari Loftus, Michael R. Morris, Richard M. Romney, Paul  
VanDenBerghe, Julia Woodbury

**Mkurugenzi wa Utendaji wa Sanaa:**

J. Scott Knudsen

**Mkurugenzi wa Sanaa:** Tadd R. Peterson

**Sanifu:** Jeanette Andrews, Fay P. Andrus, C. Kimball Bott,  
Thomas Child, Kerry Lynn C. Herrin, Colleen Hinckley,  
Eric P. Johnsen, Scott M. Mooy, Brad Teare

**Mratibu wa Haki Miliki:** Collette Nebeker Aune

**Meneja wa Uzalishaji:** Jane Ann Peters

**Uzalishaji:** Connie Bowthorpe Bridge, Howard G.  
Brown, Julie Burdett, Bryan W. Gygi, Kathleen Howard,  
Denise Kirby, Ginny J. Nilson, Ty Pilcher, Gayle Tate  
Rafferty

**Kable Chapa:** Jeff L. Martin

**Mkurugenzi wa Uchapishaji:** Craig K. Sedgwick

**Mkurugenzi wa Usambazaji:** Evan Larsen

Kwa usajili na bei inje ya Merikani na Kanada, enda store.  
lds.org au wasiliana na kituo cha usambazaji cha Kanisa  
lako ama kiongozi wa kata au tawi.

**Wasilisha maandiko na maswali** mitamboni katika  
liahona.lds.org; na barua pepe liahona@ldschurch.org;  
ama barua Liahona, Rm. 2420, 50 E. North Temple St.,  
Salt Lake City, UT 84150-0024, USA.

Liahona (neno katika Kitabu cha Mormoni linalomaanisha  
“dira” ama “kielekezo”) imechapishwa katika Kialbeni,  
Kiamereni, Bislama, Kibulgaria, Kikambodia, Kisebuano,  
Kichina, Kichina (kilichorahisishwa), Kikroesha, Kicheki,  
Kidenishi, Kiholanzi, Kiingereza, Kiestoni, Kijji, Kifinishi,  
Kifaransa, Kijerumani, Kigiriki, Kiangaria, Kialasandi,  
Kiindonesia, Kiitaliano, Kijapani, Kiriribati, Kikorea,  
Kilatvia, Kilithuania, Kimalagasi, Kiarshalizi, Kimongolia,  
Kinorwei, Kipolishi, Kireno, Kiromania, Kirusi, Kisamoa,  
Kislovenia, Kihispania, Kiswahili, Kiswidi, Kitagalagi,  
Kitahiti, Kithai, Kitonga, Kiukreni, Kiurdu, na Kivietinamu.  
(Marudio hutofautiana kwa lugha.)

© 2013 na Intellectual Reserve, Inc. Haki zote zimehifadihiwa  
imechapishwa katika Marekani.

Nakala na nyenko za picha katika Liahona zinaweza  
kunakiliwa kiumafaka, kwa matumizi yasiyo ya kibashara ya  
kanisa au nyumbani Nyenko za picha haziwezi kunakiliwa  
kama vikwazo vimeeleewza katika laini ya sifa na mchoro.  
Maswali juu ya haki ya kunakili yanapawsa kuelekezwa  
kwa ofisi ya Intellectual Property, 50 E. North Temple St.,  
Salt Lake City, UT 84150, USA; barua pepe:  
cor-intellectualproperty@ldschurch.org.

**For Readers in the United States and Canada:**  
Swahili (ISSN 2326-3695) is published once a year (April)  
by The Church of Jesus Christ of Latter-day Saints,  
50 E. North Temple St., Salt Lake City, UT 84150. USA  
subscription price is \$1.00 per year; Canada, \$1.20 plus  
applicable taxes. Periodicals Postage Paid at Salt Lake City,  
Utah. Sixty days' notice required for change of address.  
Include address label from a recent issue; old and new  
address must be included. Send USA and Canadian  
subscriptions to Salt Lake Distribution Center at address  
below. Subscription help line: 1-800-537-5971. Credit  
card orders (American Express, Discover, MasterCard,  
Visa) may be taken by phone or at store.lds.org. (Canada  
Post Information: Publication Agreement #40017431)

POSTMASTER: Send address changes to Salt Lake  
Distribution Center, Church Magazines, P.O. Box 26368,  
Salt Lake City, UT 84126-0368

## Mawazo ya Mkutano wa Jioni ya Familia Nyumbani

*Toleo hili lina makala na shughuli ambazo zinaweza kutumika kwa ajili ya jioni ya familia  
nyumbani ifuatayo ni mifano michache.*



### “Wito na Huduma ya Yesu Kristo,”

ukurasa 18: Elder Russell M. Nelson ashiriki  
masuala matano ya maisha ya Yesu Kristo  
ambayo tunaweza kuiga. Zingatia kujadili  
masuala haya na jinsi ya kuyatumia mai-  
shani mwenu. Ungetaka kusoma hadithi ya  
maandiko kutoka kwa maisha ya Mwokozi  
ama kutazama video ya Bibilia (biblevideos.  
lds.org) ambayo inaonyesha mojawapo  
wa masuala hayo. Unaweza kuhitimisha  
kwa kutoa ushuhuda wa maisha Yake na  
huduma na kuimba “More Holiness Give  
Me” (*Hymns*, no. 131).

**“Je, ni nani Rafiki wa Kweli?”** ukurasa  
52: Ungetaka kuanza kwa kuuliza, ni  
nani rafiki wa kweli? Soma fasili ya Mzee

Robert D. Hales na jadili tunapaswa kuwa  
na rafiki wa aina gani. Zingatia kuelezea  
tokeo la wakati ambao mtu alikutendea  
kama rafiki wa kweli, na zungumzia sifa  
ambazo zinaweza kusaidia wanafamilia  
kuwa marafiki bora kwa wengine.

**“Kusherehekea Mahekalu!”** ukurasa  
62: Pamoja na familia yako, tazama picha  
za njia tofauti watoto wamesherehekea  
mahekalu. Zingatia kuonyesha picha ya  
hekalu lililo karibu nanyi na kuzungumza  
kuhusu sababu mahekalu ni muhimu. Hi-  
miza kuwa katika hekalu peke yake ndiko  
familia zinaweza kuunganishwa. Ungepe-  
nda kumaliza kwa kuimba “Families Can  
Be Together Forever” (ukurasa 65).

## KATIKA LUGHA YAKO

Liahona na nyenko zingine za kanisa zinapatikana katika lugha nyingi  
katika [languages\\_lds.org](http://languages_lds.org).

## MADA KATIKA TOLEO HILI

*Nambari zinawakilisha ukurasa wa kwanza wa makala.*

**Familia**, 30, 65

**Furaha**, 37

**Huduma**, 44, 70

**Ibada**, 18

**Imani**, 48

**Kazi ya hekalu**, 7, 64, 38,  
65, 80

**Kazi ya umisionari**, 34,  
39, 48, 52, 54, 60

**Kifo**, 4, 12, 39

**Kipaumbele**, 40

**Kitabu cha Mormoni**, 46

**Kufundisha**, 8, 9, 30

**Kujitolea**, 40

**Maagano**, 7

**Mahekalu**, 34, 62

**Maombi**, 18, 45

**Mfano**, 48

**Mkutano mkuu**, 8, 37

**M pangilio wa Kanisa**, 61

**Roho Mtakatifu**, 10, 36

**Sakramenti**, 18

**Smith, Joseph**, 66

**Tumaini**, 12

**Ubatizo**, 30

**Ufufuo**, 4, 12, 26

**Ufunuo**, 10, 46

**Ukuhani**, 44

**Uongofu**, 34, 54, 56, 60

**Upatanisho**, 18, 26, 45

**Urafiki**, 9, 52, 54

**Urejesho**, 66

**Usafi wa Kimwili**, 42

**Ushawishi**, 36, 38

**Utijifu**, 40, 42, 56

**Uvumilivu**, 59

**Viwango**, 42, 45

**Woodruff, Wilford**, 81

**Yesu Kristo**, 4, 18, 26



### Na Rais Henry B. Eyring

Mshauri wa Kwanza katika  
Urais wa Kwanza

# Ameufufuka

**U**shuhuda wa ukweli wa Ufufuo wa Yesu Kristo ni chanzo cha matumaini na azimio. Na inaweza kuwa hivyo kwa mtoto ye yote wa Mungu. Ilikuwa kwangu mimi siku moja katika majira ya joto ya Juni 1969 wakati mama yangu alifariki, imekuwa miaka mingi tangu, na itakuwa hadi nimuone tena.

Huzuni kutoka kwa kutengwa kwa muda ilibadilishwa punde kuwa furaha. Ilikuwa zaidi na tumaini kwa ajili ya muungano wa furaha. Kwa sababu Bwana amefunua mengi kupitia manabii Wake na kwa sababu Roho Mtakatifu amenidhibitishia ukweli wa Ufufuo, ninaweza kuona katika mawazo yangu vile itakavyokuwa kuungana na wapendwa wetu waliotakaswa na kufufuka:

“Hawa ndio wale watakaotoka katika ufufuo wa wenye haki.

“Hawa ndio wale ambao majina yao yameandikwa mbinguni, mahali ambako Mungu na Kristo ni waamuzi wa wote.

“Hawa ndio wale watu wenye haki walio-kamilishwa kwa njia wa Yesu aliye mpatanishi wa agano jipya, aliye kamilisha upatanisho huu makamilifu kwa njia ya umwagikaji wa damu yake yeye mwenyewe” (M&M 76:65, 68–69).

Kwa sababu Yesu Kristo alivunja minyororo ya kifo, watoto wote wa Baba wa Mbinguni wanaozaliwa duniani watafufuka katika mwili ambao daima hautakufa. Kwa hivyo ushuhuda wangu na wako wa ukweli huo mtukufu unaweza kutoa uchungu wa kupoteza mwanaafamilia mpendwa ama rafiki na kubadilisha kwa furaha ya kutarajia na azimio imara.

Bwana ametupa sisi sote zawadi ya ufufuo, ambapo roho zetu zinawekwa katika miili iliyo bila upungufu wa



kimwili (ona Alma 11:42–44). Mama yangu ataonekana kuwa kijana na aking’aa, matokeo ya umri na miaka ya mateso ya kimwili yakiwa yametolewa. Hio itamjia yeye na sisi kama zawadi

Lakini wale wetu wanaotamani kuwa naye milele la-zima wafanye chaguo kustahili kwa ajili ya uhusiano huo, kuishi ambapo Baba na Mwanawe Mpandwa aliyefufuka wanaishi kwa utakatifu. Hapo ndipo mahali pekee ambapo maisha ya familia yanaweza kuendelea milele. Ushuhuda wa ukweli huo umeongeza dhamira yangu ya kuhitimu mwenyewe na wale ninaowapenda kwa kiwango cha juu kabisa cha ufalme wa celestia kupitia Upatanisho wa Yesu Kristo ukifanya kazi maishani mwetu (ona M&M 76:70).

Bwana anatupa mwongozo katika jitihada hii ya uzima wa milele katika maombi ya sakramenti yanayonisa idia na yanaweza kukusaidia. Tunaalikwa kufanya upya maagano yetu ya ubatizo katika kila mkutano wa sakramenti.

Tunaahidi daima kumkumbuka Mwokozi. Nembo na dhabihu Yake zinatusaidia kufahamu ukubwa wa thamani aliyolipa Yeye ili kuvunja minyororo ya kifo, kutupatia rehema, na kutoa msamaha wa dhambi zetu zote tukichagua kutubu.

Tunaahidi kutii amri Zake. Kusoma maandiko na maneno ya manabii waliohai na kusikiliza wanenaji wana-oongozwa katika mikutano yetu ya sakramenti kunatukumbusha maagano yetu kwa kufanya hivyo. Roho Mtakatifu huleta mawazoni mwetu na miyo amri tunazohitaji zaidi kutii siku hiyo.

Katika maombi ya sakramenti, Mungu huagiza kutuma Roho Mtakatifu kuwa pamoja nasi (ona Moroni 4:3; 5:2; M&M 20:77, 79). Nimeona katika wakati huo kwamba



PICHA NA MATTHEW REIER, AMEFUKA, NA DEL PARSON, HAIFAI KUNAKIWA

Mungu anaweza kunipa kile kinachohisika kama mahojiano ya kibinagsi. Yeye huleta kwa usikivu wangu kile nimefanya kinacho-mpendeza Yeye, haja yangu kwa ajili ya toba na msamaha, na majina na nyuso za watu Yeye angetaka niwatumikie kwa ajili yake.

Miaka nenda miaka rudi, uzoefu huo

unaorudiwa umegeuzea tumaini kuwa hisia za upendo na kuleta uhakika kwamba rehema ilifunguliwa kwa ajili yangu na Upatanisho wa Mwokozi na Ufufuo.

Nashuhudia kuwa Yesu ndiye Kristo aliye-fufuka, Mwokozi wetu, na mfano wetu kamili na mwongozo wa maisha ya milele. ■

## KUFUNDISHA KUTOKA KWA UJUMBE HUU

Tunapaswa tu "kulinjishe maandiko yote nasi, ili yatufundishe na kutuelimisha" (1 Nefi 19:23). Zingatia kusoma maombi ya sacramenti, yanayopatikanata katika Mafundisho na Maagano 20:76–79. Baada ya kusoma mafundisho ya Rais Eyring kuhusu maombi ya sacramenti, ungetaka kualika wale ambao unafundisha kufikiri kuhusu jinsi maombi haya yanaweza kuongoza maisha yao na kuwasaidia kurejea kuishi tena na Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo.

## Mahojiano Yako ya Kibinafsi na Mungu

Rais Eyring hufundisha kuwa tunaposikiliza maombi ya sakramenti, tunaweza kuhisi kama tunakuwa na mahojiano ya kibinafsi na Mungu. Rais Eyring hufikiri kuhusu sehemu tatu zifuatazo. Zingatia kuandika maswali haya katika jarida lako na kuyatafakari kila Jumapili mwezi huu. Unapotafakari

na kupokea ushawishi kutoka kwa Roho Mtakatifu, unaweza kuandika kuhusu hizo katika jarida lako.


- Nimefanya nini ambacho kimempendeza Mungu?
- Ninahitaji kutubu na kuomba msamaha kwa nini?
- Mungu angenitaka nimtumikie nani?

## WATOTO

## Daima Mkumbuke Yesu

Yakobo anajaribu "daima kumbuka" Mwokozi (M&M 20:77). Angalia chumba chake cha kulala.

Unagundua nini kinachoweza kumsaidia daima kumkumbuka Yesu?



Soma kwa maombi na kama ifaavyo, ukijadili pamoja na kina dada unaowatembelea. Tumia maswali ili kukusaidia kuwaimarisha dada zako na kuifanya Muungano wa Usaidizi wa Kina Mama kuwa sehemu hai ya maisha yako mwenyewe. Kwa taarifa zaidi, nenda kwenye [www.reliefsociety.lds.org](http://www.reliefsociety.lds.org).

## Maagano ya Hekalu

**M**aagizo ya wokovu yanayopo-kelewa katika hekalu siku moja ambayo yatatutwezesha kurejea kwa Baba yetu wa Mbinguni katika uhusiano wa kifamilia ya milele na kuimari-shwa na baraka na nguvu kutoka juu zinastahili kila kujitolea na kila bidii,<sup>1</sup> alisema Rais Thomas S. Monson Kama bado haujaenda hekaluni, unaweza kujitayarisha kupokea maagizo mataktifu ya hekalu kwa:

- Kuamini katika Baba wa Mbinguni, Yesu Kristo na Roho Mtakatifu.
- Kukuza ushuhuda wa Upatani-sho wa Yesu Kristo na urejesho wa injili.
- Kuunga mkono na kufuata nabii aliyehai.
- Kufuzu kwa kupokea sifu ya hekalu kwa kulipa zaka, kuwa msafi kimaadili, kuwa mwami-nifu, kutii Neno la Hekima, na kuishi kulingana na mafundisho ya Kanisa.
- Kutoa muda, talanta, na mali ili kusaidia kujenga Ufalme wa Bwana.



- Kushiriki katika kazi ya historia ya familia.<sup>2</sup>

Rais Monson alifundisha zaidi, “Tunapokumbuka maagano tunayo-fanya katika [hekalu], tutawea zaidi kustahimili kila jaribio na kushinda kila jaribu.”<sup>3</sup>

### Kutoka kwa Maandiko

Mafundisho na Maagano 14:7; 25:13; 109:22

#### MUHTASARI

1. Thomas S. Monson, “The Holy Temple—a Beacon to the World,” *Liahona*, Mei 2011, 92.
2. Ona *Daughters in My Kingdom: The History and Work of Relief Society* (2011), 21.
3. Thomas S. Monson, *Liahona*, Mei 2011, 93.
4. *Daughters in My Kingdom*, 29–30.
5. Sarah Rich, katika *Daughters in My Kingdom*, 30.

### Ninaweza Kufanya Nini?

**1.** Je, ninaabudu hekaluni mara kwa mara?

**2.** Je, ninawahimiza dada zangu kupokea baraka za hekalu?

Imani, Familia,  
Usaidizi



### Kutoka kwa Historia Yetu

“Zaidi ya Watakatifu 5,000 walijaza Hekalu la Nauvoo baada ya kuwekwa wakfu. . . .

“Uwezo, nguvu na baraka za maagizo ya hekalu [zinawahimili] Watakatifu wa Siku za Mwisho wakati wa safari yao [Magharibi], wakati walipo [pitia] baridi, joto, njaa, umaskini, magonjwa, ajali na kifo.”<sup>4</sup>

Kama wengi wa akina dada wa Muungano wa Usaidizi wa Kina Mama, Sarah Rich alihudumu kama mfanyakazi wa hekalu. Alizungumzia uzoefu wake: Kama haingekuwa ni imani na maarifa ambayo tulipata katika hekalu hilo na Roho wa Bwana, safari yetu ingekuwa kama moja achukuaye hatua gizani. Lakini tulikuwa na imani katika Baba yetu wa Mbinguni, tukihisi kuwa sisi tulikuwa watu Wake wateule . . . , na badala ya huzuni, tulihisi kufurahia kwamba siku ya ukombozi wetu imekuja.”<sup>5</sup>

Safari ya kutoka haikuwa “hatua gizani” kwa wanawake waaminifu wa Watakatifu wa Siku za Mwisho walihimiliwa na maagizo yao ya hekalu.

# KUJIFUNZA HOTUBA ZA MKUTANO MKUU PAMOJA

*Kubadilisha njia yetu ya kurejelea mkutano kuliimarisha zaidi majadiliano yetu ya injili kama familia.*

**Na Greg Batty**

Kwa miaka tumefurahia kusoma kwa kupitia toleo la mkutano kama familia, makala moja kwa wakati tulipoanza, tulikusanyika mezani tu na kwa zamu tulisoma kila mmojaaya kwa sauti. Lakini tuligundua kuwa tulikuwa tukisoma ili kuipitia, bila kutua ili kuelewa ujumbe.

Ili kupata zaidi kutoka kwa kile tulichokuwa tukisoma, mke wangu nami tulinunua nakala moja ya toleo la mkutano kwa kila mwana familia na tukapanga mazungumzo mangapi tungefaa kujifunza kila wiki ili tuweze kuyasoma yote kabla ya mkutano mkuu ufuatao. Wiki kadha tunge-soma hotuba moja, na wiki zingine ingekuwa mbili, lakini kila mtu alifaa kusoma hotuba na kuweka alama katika sehemu walizopenda. Kisha kwa Mkutano wa Jioni wa familia nyumbani tungefundi shana kutoka kwa sehemu tulizoweka alama.

Mara nyingi watoto wetu walikuwa na maswali yaliyofungua majadiliano yetu, au mke wangu nami tuliuliza maswali kutoka kwa masomo yetu. Tulidhamini kusikia vijana wetu wakieleza majibu yao ya maswali hayo, wakishiriki vitu walivyojifunza katika

seminari kanisani, au katika masomo yao ya kibinafsi. Hii ikawa njia nzuri ya kusikiliza shuhuda zisizo rasmi za kila moja mara kwa mara katika mazingira ya starehe na utulivu.

Punde tuligundua kuwa masomo yetu ya maandiko ya asubuhi yali-chukua toni sawa. Baadhi ya siku tulipitia mistari michache tu kabla wakati kuyoyoma kutoka kwa mjadala kuhusu mistari hiyo na jinsi ililingana na yale yaliyokuwa yakite-ndeka karibu nasi.

Asubuhi zetu sasa zimejawa na mazungumzo, vicheko, na umoja kabla ya kila moja wetu kwenda nje kwa shughuli zetu binafsi. Tuna ushuhuda imara wa ushauri ya nabii wetu wa kujifunza na kuomba pamoja kila siku. Familia yetu imebadilishwa kuwa moja ambayo inajifunza kutoka kwa na kuimarishwa kila mmoja. Yote haya ni matokeo ya kutaka kupata zaidi kidogo kutoka kwa mkutano mkuu. ■

*Greg Batty anaishi Utah, USA.*



## KUJIFUNZA NA KUTUMIA JUMBE ZA MKUTANO MKUU

"Kumbuka kuwa jumbe tulizosikiza mkutanoni huu zitachapishwa katika toleo la Mei la majorida ya *Ensign* na *Liahona*. Ninawahimiza musome jumbe hizi, mtafakari mafundisho yake, na kisha muyatumie maishani mwenu."

**Rais Thomas S. Monson, "Neno la Kufunga," *Liahona*, Mei 2010, 113.**



# UMUHIMU WA MARAFIKI WAZURI

**M**arafiki wana ushawishi mkubwa juu ya matendo yetu, hasa kati ujana wetu. “Watashawishi jinsi unafikiri na kutenda, na hata kusaidia kuamua mtu utakaye kuwa.”<sup>1</sup> Na unapochagua marafiki wazuri, “watakuwa nguvu na baraka kwako. Watakusaidia kuwa mtu bora na watafanya iwe rahisi kwako kuishi injili ya Yesu Kristo.”<sup>2</sup>

Fungua kurasa 52–53 katika toleo hili, Elaine S. Dalton, rais mkuu wa Wasichana, alifundisha umuhimu wa kutafuta na kuwa rafiki mzuri. “Kutaka wema wa mtu mwingine ni kiini cha urafiki wa kweli”, asema.

Kujenga urafiki juu ya kanuni hizi kutawasaidia vijana kutengeneza mahusiano ya kudumu na stadi za kijamii zinazokwenda mbali zaidi tu na kuwa “rafiki” katika maeneo ya mitandao ya kijamii. Kama mzazi unaweza kuwasaidia watoto wako kuelewa umuhimu wa kuwa rafiki mzuri na wa kuchagua marafiki amba watawahimiza kuishi injili. Mapendekezo yafuatayo yanaweza kuwa ya manufaa.

## Mapendekezo ya Kufundisha Vijana

- Kama familia, yachunguze mandiko kwa mfano wa marafiki wazuri. Jadili sifa zilizofanya mahusiano hayo kuwa imara. Zingatia David na Jonathan

(ona 1 Samueli 18–23), Ruth na Naomi (ona Ruth 1–2), na Alma na wana wa Mosia (ona Mosia 27–28; Alma 17–20).<sup>3</sup>

- Rejelea sehemu ya marafiki katika *Kwa nguvu ya Vijana* Shiriki na vijana wako jinsi urafiki unaweza kuathiri maisha yako. Wahimize kushiriki jinsi wameathiri na kuathiriwa na marafiki wao.
- Soma makala ya Dada Dalton katika toleo hili. Zungumza kuhusu lengo ambalo bintiye, Emi, aliweka kutafuta marafiki wazuri. Saidia watoto wako kuweka malengo kuhusu aina ya marafiki amba wanataka kutafuta na kuwa.
- Zingatia kuwa na Mkutano wa Jioni wa familia nyumbani kushiriki mawazo ya kujenga urafiki, kama vile: “Ili kuwa na marafiki wazuri, kuwa rafiki mzuri. Onyesha nia ya kweli kwa wengine; tabasamu na wajulishe unawajali. Tendea kila mtu kwa wema na heshima, na jiepushe na kuhukumu na kukosoa wale walio karibu nawe.”<sup>4</sup>

## Mapendekezo ya Kufundisha Watoto

- Kuwa rafiki kunajumuisha kusaidia wengine. Soma “Standing



## MAANDIKO JUU YA URAFIKI

- Mithali 17:17; 18:24  
Muhibiri 4:9–10  
Mathayo 25:34–40  
Luka 22:32.  
Mosia 18:8–11

Up for Caleb” katika *Liahona* ya Machi 2009 na uzungumze na watoto wako kuhusu jinsi wanyoweza kuwa wapole kwa kila mtu wanayekutana naye.

- Katika kila hali, lazima tuamue ni aina gani ya rafiki tutakuwa. Imbeni pamoja “I’m Trying to Be Like Jesus”<sup>5</sup> kisha zungumza na watoto wako kuhusu jinsi wanyoweza kuchagua kuwa rafiki mzuri, kama Mwokozi, katika maandhari tofauti. ■

## MUHTASARI

1. *Kwa Nguvu ya Vijana* (kijitabu, 2011), 16.
2. *Kwa Nguvu ya Vijana*, 16.
3. Ona Jeffrey R. Holland, “New Era, Juni 1998, 62–66.
4. *Kwa Nguvu ya Vijana*, 16.
5. “I’m Trying to Be Like Jesus,” *Kitabu cha Watoto cha Wimbo*, 78–79.

# ROHO MTAKATIFU HUFARIJI, HUHAMASISHA NA HUSHUHUDIA

**K**ipawa cha Roho Mtakatifu ni mojawapo wa baraka kubwa tunaweza kupokea katika maisha haya, kwa kuwa Roho Mtakatifu, huhamasisha, hutuonya, hututakasa, na hutuongoza. Anaweza kutujaza na “tumaini na upeendo kamili” (Moroni 8:26). Hufundisha “ukweli wa vitu vyote” (Moroni 10:5). Sisi hupokea ufunuo na vipawa vya kiroho kutoka kwa Mungu kuitia Roho Mtakatifu. Muhimu zaidi, sisi hupokea shuhuda zetu za Baba wa Mbunguni na Yesu Kristo kuitia Roho Mtakatifu.

Kabla ubatizwe, ungehisi Roho Mtakatifu mara kwa mara. Lakini tu kwa kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu baada ya kubatizwa kwako ndipo ungeweza kufurahia uenzi wa kudumu wa Roho Mtakatifu, mradi unastahili. Kipawa hicho kilipeanwa

na mwenye Ukuhani wa Melkezediki kwa kuwekelea mikono (ona Mateendo 19:6; M&M 33:15). Kila Sabato kufuatia, unaweza kufanya upya magano yako ya ubatizo unapopokea sakramenti na hivyo kupokea baraka ya Bwana kuwa unaweza “daima kuwa na Roho Wake” kuwa pamoja nawe (M&M 20:77).

Roho Mtakatifu, kwa mara nyingi anajulikana kama Roho, ni mshiriki wa tatu wa Uungu. Nabi Joseph Smith alifundisha: “Baba ana mwili wa nyama na mifupa wenyewe kushikika kama wa mwanadamu; Mwana vile vile; lakini Roho Mtakatifu hana mwili wa nyama na mifupa, lakini ni mtu wa Kiroho. Kama isingekuwa hivyo, Roho Mtakatifu asingeweza kukaa ndani yetu” (M&M 130:22).

“Kwa sababu Roho wa Bwana haishi kwenye mahekalu yasio matakatifu” (Helamani 4:24), lazima tuwa wastahiki wa uenzi Wake. Tunafanya hivyo na, mionganoni mwa mambo mengine, kuwa na mawazo mema, kuishi kwa uadilifu, na kuttaka kutii amri. ■

Kwa habari zaidi, ona 2 Nefi 31:13, 17; 32:5; 3 Nefi 27:20; Moroni 10:5–8; Joseph Smith—Historia 1:70.



## TUSICHUKULIE KIPAWA HIKI KUWA JAMBO LA KAWAIDA

Kama ilivyo na vipawa vyote, zawadi hii lazima ipokelewe na kukubaliwa ili ifurahiwe. Wakati mikono ya ukuhani iliwekelewa kichwani mwako kukudhibitisha kama mshiriki wa Kanisa, ulisikia maneno, “Pokea Roho Mtakatifu.” Hii haikumaanisha kuwa Roho Mtakatifu angekuwa mwenzi wako daima bila masharti. Maandiko yanatuonya kuwa Roho wa Bwana ‘haitashindana na mwanadamu milele’ (Mwanzo 6:3). Tunapodhibitishwa, tunapewa *haki* kwa uenzi wa Roho Mtakatifu, lakini ni haki ambayo lazima tuendele kupata kuitia utifu na ustahiki .

Mzee Joseph B. Wirthlin (1917–2008) wa Jamii ya Mitume Kumi na Wawili, *The Unspeakable Gift, Liahona*, Mei 2003, 28.

**Baada ya kupokea kipawa  
cha Roho Mtakatifu, tun-  
weza kufanya mambo me-  
ngi kualika ushawishi Wake  
katika maisha yetu:**

*Ombo.*



*Jifunze maandiko.*



*Kushiriki katika sacramenti kwa ustahiki.*



*Kuabudu Hekaluni.*

*Tazama vyombo safi vya  
habari, tumia lugha safi, na  
kuwa na mawazo mema.*

# Kifo NA MaLsha

MITAZAMO YA WATANGULIZI  
JUU YA UFUFUO.

*Waongofu wa kwanza wa Kanisa waliposafiri magharibi mwa Merikani kukusanyika na Watakatifu, walikumbana na kifo lakini walistihimiliwa na imani yao mpya katika injili ya urejesho. Yafuatayo ni nukuu kutoka kwa maelezo ya watangulizi yanayoonyesha tumaini la Watakatifi katika Ufufuo, pamoja na mafundisho kutoka kwa Marais wa tano wa kwanza wa Kanisa.*

*Robert Aveson, akirejelea hadhithi ya baba Msandinavia Mtakatifu wa Siku za Mwisho asiyetajwa ambaye mwanawe alifariki safarini kutoka New York hadi Utah mnamo 1866:*

“Na usaidizi wa rafiki kaburi dogo lilichimbwa na mabaki yakawekwa pale ndani. Mtoto aliyefariki kutokana na ugonjwa unaoambukizwa, hapakuwa na waombolezaji, hamnashe-rehe rasmi, hamna nembo za maua, hamna wimbo wa kiroho, hamna neno la taabini. Lakinini kabla ya baba aliyefiwa kuondoka alitamka maombi fupi ya kuweka wakfu katika lugha yake ya asili (Kidenishi) kama ifuatavyo: . . .

Baba wa Mbinguni: Wewe ulinipa hazina hii ndogo—mvulana huyu mpendwa, na sasa wewe umemuita. Tafadhalii ruhusu kwamba mabaki yake yabaki hapa salama mpaka asubuhi

ya ufufuo Mapenzi yako yatimizwe Amina.”

“Na akiamuka kutoka ardhini maneno yake yakuaga yalikuwa:

“Kwaheri, mpPENDWA wangu mdogo Hans—mwanangu mzuri.’ Kisha kwa kichwa legevu na moyo wa kuuma alishika njia yake kwa kambi yake.”<sup>1</sup>


*Rais Joseph Smith (1805–44):*

“Ni jambo la kuliwaza kwa waombolezaji wanapoitwa kuwachana na mume, mke, baba, mama, mtoto, au ndugu mpendwa, kujua kwamba, ingawa mwili wa kidunia umewekwa chini na kuharibiwa, watafufuka tena kukaa katika mafukizo ya milele katika utukufu wa milele, si kuhuzunika, kuteseka, au kufa tena, bali watakuwa warithi wa Mungu na warithi pamoja na Yesu Kristo.”<sup>2</sup>



*Joseph Watson Young (1828–73), mpwa wa Brigham Young ambaye alisafiri kutoka Uingereza hadi Marekani mnano 1853:*


“Ilikuwa tokeo la ombolezo kufungia kiumbe mwenzagu kwa kimya cha kina saa la kiza la usiku na mashahidi wachache tu wapweke. Hakuwa na jamaa pamoja naye au mtu ye yote hasa wa kuomboleza isipokuwa mtumishi mwenzake. Haya ni matumaini ya furaha ya asili ya binadamu yakiangamizwa kwa masaa. Kijana huyu alikuwa amewacha yote ili kuende katika Sayuni, na moyo wake ulichomwa na matalariojio hai ya usoni, kufikiria kidogo kwamba angefungia mwili wake wa kidunia kwa wimbi la njaa. Hata hivyo, alikuwa si kama wale wasio na matumaini, kwa kuwa amani yake ilifanywa kwa Mungu wake, na alikuwa na uhakika kamili wa ufufuo mtukufu asubuhi wa wenye haki”.<sup>3</sup>



*Kushoto: Rais Brigham Young  
Juu: Joseph Watson Young.*

*Rais Brigham Young (1801–77):*

“Jameni bonde la giza na kivuli tunayoita kifo! Kupita kutoka hali hii ya kuwepo mbali na mwili wa kidunia inahusika, katika hali ya udhaifu [utupul], ya ajabu jinsi gani. Kiza jinsi gani bonde hili. Ajabu jinsi gani barabara hii, na lazima tuisafirie peke yetu. Nangependi kuwambieni nyinyi, rafiki na ndugu zangu, kama tungeweza kuona mambo kama yalivyo, na kama tutakavyoyaona na kuyaelewa, kivuli hiki cha giza na bonde ni jambo dogo kwamba tutageuka na kulitazama na kufikiria, wakati tumelivuka, kwa nini hii ni faida kubwa ya kuwepo kwangu kote, kwa maana nime-pita kutoka hali ya huzuni, ghamu, msiba, ole, taabu, dhiki na maumivu, na kukata tamaa hadi katika hali ya kuwepo, ambapo ninaweza kufurahia maisha kwa kiwango kikamilifu kabisa hadi panapowezekana kufanyika bila mwili.”<sup>4</sup>






*Dan Jones (1811–62), mwongofu wa Kiwelishi ambaye, pamoja na Bi. Williams na washiriki wengine wa Kanisa, alipanda meli kwenda Marekani mnamo 1849:*

“Bi. Williams, wa Ynysybont karibu na Tregaron [Wales], amezidiwa haraka, na dalili ni kuwa hataishi kwa muda mrefu. Alisema kuwa heshima ya juu kabisa ali-yowahi kupokea ulikuwa kuwa mshiriki wa kanisa la kweli la Mwana wa Mungu, ya kwamba hakukuwa na uoga moyoni mwake kuhusu maisha yajayo na kuwa dini yake sasa imonyesha nguvu zake zaidi kuliko hapo awali. Aliwashauri wanawe kwa dhati kuendelea kuwa waaminifu hadi kifo ili waweze kupata pamoja naye ufufuo bora. Aliendelea kuwa timamu kuititia usiku, na saa kumi na robo asubuhi

ifuatayo roho yake ikaenda kwa amani, na kuacha tabsamu midomoni mwake.”<sup>5</sup>

*Rais John Taylor (1808–87):*

“Kunaliwaza vipi kwa wale ambao wanaitwa kuomboleza kupotea kwa wapenzi katika kifo, kujua kwamba tutahusishwa nao tena. Kunatia moyo vipi kwa wote ambao wanaishi kulingana na kanuni za ukweli zilizofunuliwa, pengine zaidi kwa wale ambao maisha yao yametumika vizuri, ambao wamevumilia joto na mzigo wa siku, kujua kuwa kabla ya kuwafikia kwa muda mrefu tutapasua vikwazo vya kaburi, na kutokea roho hai na zisizokufa, kufurahia jamii ya marafiki zetu waliojribiwa na kuaminiwa, katu kuadhibiwa tena na mbegu ya kifo, na kumaliza kazi ambao Baba ametupa tufanye!”<sup>6</sup>



*Kulia: Rais John Taylor.  
Juu: Dan Jones.*



*Andrew Jenson (1850–1941), Mhamiaji wa Kidenishi ambaye alisafiri katika kundi la mkokoteni la Andrew H. Scott kutoka Nebraska, USA, hadi Utah mnamo 1866.*

Tuliposhuhudia mabaki ya kidunia yao [wasafiri wenzetu] yakiwekwa kwenye ardhi, kwenye jangwa, sote tulilia, ama kuhisi kulia; kwa kuwa fikra ya kuzika wapendwa kwa jinsi hii, ambapo marafiki na jamii lazima punde wakimbie kuenda, bila tumaini ya kuwai kutembelea mahala pa kupumzikia pa wapendwa wao walioaga, ilikuwa ya kuhuzunisha na jaribio kweli. Lakini kaburi zao zitapatikana wakati Gabrieli atakapopiga tarumbeta yake katika asubuhi wa ufufuo wa kwanza. Hawa waliooaga basi walilaza miili yao chini walipokuwa wakitembea kuelekea Sayuni. Bwana aliwaita nyumbani kabla wafike walikokuwa wakienda, hawakuruhusiwa kuona Sayuni katika mwili; lakini



*Kushoto:  
Rais Wilford  
Woodruff. Juu:  
Andrew Jenson.*

watapokea utukufu na kufurahia hapo baadaye; waliaga wakijitahidi kutii Mungu na kutii amri zake, na wabarikiwa ni wale wanaokufa katika [Bwana].”<sup>7</sup>

*Rais Wilford Woodruff (1807–98).*

“Bila injili ya Kristo utengano kwa kifo ni mojawapo wa mada ya kuhuzunisha kabisa ya kutafakari; lakini punde tu tunapopokea injili na kujifunza kanuni za ufufuo huzuni, dhiki, na mateso yanayoletwa na kifo yanaolewa, kwa kiwango kikubwa. Ufufuo wa waliokufa unajitokeza mbele ya akili iliyoelimika ya mwanadamu, na hana

msingi wa roho wake kulalia. Huu ndio msimamo wa Watakatifu wa Siku za Mwisho hata leo. Tunajijilia, hatuko gizani katika swala hili, Mungu ametufunulia na tunaelewa kanuni ya ufufuo wa waliokufa, na injili huleta uzima na kutokufa kwa ufahamu.”<sup>8</sup>



*Kwa kuwezesha usomaji, tahajia kadha, matumizi ya vituo vya uandishi, na matumizi ya herufi kubwa yamesanifishwa.*

#### MUHTASARI

1. Robert Aveson, “Leaves from the Journal of a Boy Emigrant,” *Deseret News*, Mar 12, 1921, 4:7; inapatiikan lds.org/churchhistory/library/pioneercompanysearch.
2. *Teachings of Presidents of the Church: Joseph Smith* (2007), 52.
3. Joseph W. Young, Journal, Mar. 6, 1853, Church History Library, Salt Lake City, Utah; inapatiikan katika mtandao



*William Driver (1837–1920), mtangulizi aliyesafiri kutoka Uingereza hadi New York, USA, mnano 1866:*

Willie, mtoto wangu mpendwa, alikuwa mgonjwa sana usiku mzima hadi 7:30 asubuhi, alipowachiliwa kutoka kwa mateso yake. Mungu bariki nafsi yake. Jinsi alivyoteseka. Aliaga kupitia mkokoteni wa Bwana Poulter kusimama kwenye mlima wa St. Ann, Wandsworth, Surrey, Uingereza. Eh, jinsi ninavyoomboleza dhiki hii kuu Ewe Bwana, nisaidie kwa uwezo wako kuuvumilia kama kwa mkono wako na nishawishi kukutumikia Wewe kwa ulodi na



*Kulia: Rais Lorenzo Snow.  
Juu: William Driver.*

uaminifu zaidi, na ni weze kuishi ili kujitayarisha kukutana naye katika dunia yenye furaha na bora zaidi na dake mpendwa, Elizabeth Maryann, na katika

ufufuo wa wenyehaki niweze kuwa hapo kukutana nao.”<sup>9</sup>

*Rais Lorenzo Snow (1814–1901):*

“Katika maisha yafuatayo tutakuwa na miili mitukufu na tutakuwa bila ugonjwa na kifo. Hakuna kilichopendeza zaidi kama vile mtu katika hali ya ufufuo na utukufu. Hakuna kilicho cha kupendeza zaidi kushinda kuwa katika hali hii na kuwa na wake wetu na watoto na marafiki nasi.”<sup>10</sup> ■

[mormonmigration.lib.bry.edu](http://mormonmigration.lib.bry.edu).

4. *Teachings of Presidents of the Church: Brigham Young* (1997), 273.

5. “Barua Kutoka kwa Nahodha D. Jones kwa mhariri wa *Udgorn Seion*,” katika Ronald D. Dennis, *The Call of Zion: The Story of the First Welsh Mormon Emigration*, vol. 2 (1987), 164–65; inapatikana mormon migration.lib.bry.edu.

6. *Teachings of Presidents of the Church: John Taylor* (2001), 50–51.

7. Andrew Jenson, Journal, Aug. 20, 1866, katika *Journal History of The Church of Jesus Christ of Latter-day Saints*, Oct. 8, 1866, Church History Library, Salt Lake City, Utah, 6; inapatikana lds.org/churchhistory/library/pioneercompanysearch.

8. *Teachings of Presidents of the Church:*

*Wilford Woodruff* (2004), 82–83.

9. Frank Driver Reeve, ed., *London to Salt Lake City in 1866: The Diary of William Driver* (1942), 42; inapatikana mormonmigration.lib.bry.edu.

10. Lorenzo Snow, katika Conference Report, Oct. 1900, 63.



**Na Mzee Russell M. Nelson**

Wa Jamii ya Mitume  
Kumi na Wawili

# Wito na Huduma ya **YESU KRISTO**

*Ushuhuda bora wa kumsujudu kwetu  
Yesu ni kwetu kumuiga Yeye.*

**K**ama mmoja kati ya “mashahidi wa kipekee wa jina la Kristo duniani kote” (M&M 107:23), Ninaamini ninatumika vyema nikifundisha na kushuhudia juu Yake. Kwanza, ninaweza kuuliza swali ambalo Yeye aliuliza Mafarisayo: “Mwaonaje katika habari za Kristo? ni mwana wa nani?” (Mathayo 22:42).

Maswali haya mara nyingi huja akilini ninapokutana na viongozi wa serikali na vitengo vyta dini tofauti. Wengine hukiri kuwa “Yesu alikuwa mwalimu mkuu.”

Wengine husema, “Alikuwa Nabii.” Wengine tu hawamjui Yeye kamwe. Hatupaswi kushangazwa kabisa. Hata hivyo, watu wachache kiasi wako na kweli za injili ya urejesho ambazo tunazo. Washiriki wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho ni mionganoni mwa wale walio wachache wanaodai kuwa Wakristo.

Hali yetu leo ilitabiriwa karne zilizopita na Nefi:

“Na ikawa kwamba niliona Kanisa la Mwanakondo wa Mungu, na hesabu yake ilikuwa chache . . . ; walakini nikaona kwamba kanisa la Mwanakondo, ambao walikuwa ni watakatifu wa Mungu, pia nao walikuwa kote usoni mwa dunia; na utawala wao usoni mwa dunia ulikuwa mdogo. . . .

“Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliona nguvu za Mwanakondoo wa Mungu, kwamba ziliwashukia watakatifu wa kanisa la Mwanakondoo, na kwa watu wa agano wa Bwana, ambao walitawanyika kote usoni mwa dunia; na walikuwa wamejikinga kwa utukufu na kwa nguvu za Mungu katika utukufu mkuu.”

(1 Nefi 14:12, 14).

Haki hio, nguvu hio, na utukufu huo—kweli, baraka zetu zote nyingi—zinatokana na ufahamu wetu wa, utiifu kwa, na shukrani na upendo kwa Bwana Yesu Kristo.



Wakati wa safari yake fupi kiasi duniani, Mwokozi alitimiza malengo mawili makuu. Moja lilikuwa “kazi na utukufu [Wake]—kuleta kutokufa na uzima wa milele wa wanadamu” (Musa 1:39). Lingine alisema kwa urahisi: “nimewapa kielelezo, ili kama mimi ninavyowatendea, nanyi mtende vivyo” (Yohana 13:15).

Lengo Lake la kwanza tunajua kama Upatanisho. Hii ilikuwa wito Wake wa ajabu duniani. Kwa watu wa Amerika ya kale, Bwana aliyefufuka alipeana maelezo ya wito Wake:

“Nilikuja kwenye ulimwengu kufanya mapenzi ya Baba, kwa sababu alinituma.

Na Baba yangu alinituma ili nipate kuinuliwa juu kwenye msalaba; na baada ya kuinuliwa juu kwenye msalaba, kwamba ningeteletu watu wote kwangu” (3 Nefi 27:13–14).

Katika kuendeleza hotuba Yake, alifunua lengo Lake la pili—kuwa kielelezo wetu: “mnajua vitu ambavyo mnahitajika kufanya . . . ; kwani vitendo ambavyo mmeniona nikifanya hivyo pia mtafanya” (3 Nefi 27:21).

Lengo lake la kwanza, nimeelezea kama *wito Wake*. Lengo Lake la pili ningependa kuitambua kama huduma *Yake*. Wacha turejelee sehemu hizi mbili za maisha *Yake*—Wito na Huduma *Yake*.

### **Wito wa Yesu Kristo—Upatanisho**

Wito wake ulikuwa Upatanisho. Wito huo ulikuwa ni *Wake* wa kipekee. Akiwa ameza liwa na mama wa kiulimwengu na Baba wa kiungu, alikuwa ndiye wa pekee ambaye angeweza kuweka maisha *Yake* chini kwa kujitolea na kuyachukua tena (ona Yohana 10:14–18). Matokeo matakatifu ya Upatanisho *Wake* yalikuwa ya daima na milele. Alichukua uchungu wa kifo na akaufanya kuwa wa muda dhiki ya kaburi (ona 1 Wakorinthio 15:54–55). Jukumu lake la Upatanisho

lilijulikana hata kabla ya Uumbaji na Kuanguka. Halikuwa tu la kupeana ufufuo na kutokufa kwa kila mwanadamu, lakini lili-kuwa pia kutuwezesha kusamehewa dhambi zetu—kulingana na matarajio yaliyowekwa Naye. Hivyo basi Upatanisho *Wake* ulifungua njia ambayo tungeunganishwa Naye na familia zetu milele. Tarajio hili tunaloenzi kama uzima wa milele—zawadi kuu ya Mungu kwa mwanadamu (ona M&M 14:7).

Hakuna mwingine angeliweza kufanya Upatanisho. Hakuna mtu mwingine, hata na mali na nguvu kuu, angeweza kuokoa nafsi moja—hata yake mwenyewe (ona Mathayo 19:24–26). Na hakuna mtu mwingine binafsi atakayetarajiwa au kukubaliwa kumwaga damu kwa ajili ya uokovu wa milele wa mwanadamu mwinigine. Yesu aliifanya “mara moja tu” (Waebrania 10:10).

Ingawa Upatanisho ulitekelezwa wakati wa Agano Jipy, matokeo ya Agano la Kale kwa mara nyingi yalitabiri umuhimu wake. Adamu na Hawa waliamuriwa watoe dhabihu kama “mfano wa dhabihu ya Mzaliwa wa Pekee wa Baba” (Musa 5:7). Kivipi? Kwa kumwaga damu. Kutokana na uzoefu wao mwenyewe walidhibitisha maandiko kuwa “uhai wa mwili u katika damu” (Mambo ya Walawi 17:11).

Madaktari wanajua kuwa mara tu damu inapowacha kuenda kwa ogani, shida huanza. Kama mbubujiko wa damu kwa mguu umedakizwa, gangrini huenda ikafuatia. Kama mbubujiko kwa akili umekatizwa, upoozaji huenda ukafuatia. Kama damu imeshindwa kububujika kwa kawaida kupitia mshipa wa moyo, mshtuko wa moyo huenda ukatokea. Na ikiwa hemoraji hajazuiwa, kifu hufuatia.

Adamu, Hawa na uzao uliofuatia waliji-funza kuwa wakati wowote walipomwanga damu kutoka kwa mnyama, maisha yake

WOMAN BEHOLD THY SON (STABAT MATER) / NA JAMES TISSOT © BROOKLYN MUSEUM, BROOKLYN, NEW YORK; KIPACHIKWA: MAELEZO KUTOKA KWIA IN THE GARDEN OF GETHSEMANE, NA CARL HENRICH BLOCH



**M**<sup>wokozi</sup>  
**a**<sup>lia-</sup>  
**n**<sup>za</sup>  
**kumwaga** **damu**  
**Yake** **kwa** **ajili**  
**ya** **kila** **mwa-**  
**nadamu** **si**  
**kwenye** **msa-**  
**labu**, **ambako**  
**mateso** **ya**  
**Upatanisho** **yali-**  
**malizwa**, **lakini**  
**kattika** **Bustani** **la**  
**Gethsemani.**



yalikatizwa. Kwa shughuli yao ya dhabihu, si tu mnyama *yoyote* angetosha. Alikuwa awe mwana-kondoo wenu atakuwa hana ila, mume wa mwaka mmoja (ona, kwa mfano, Kutoka 12:5). Matarajio haya yalikuwa pia ni ya ishara ya dhabihu itakayomtendekea Kondoo wa Mungu asiye na ila.

Adamu na Hawa walipewa amri: "Kwa hiyo, nawe utafanya yale yote uyafanyayo katika jina la mwana, nawe utatubu na kumlingana Mungu katika jina la Mwana milele yote" (Musa 5:8). Tangu siku hiyo hadi katika meridiani ya siku, dhabihu ya mnyama iliendelea kuwa kielelezlo na kivuli cha Upatanisho utakaotendeka wa Mwana ya Mungu.

Wakati upatanisho ulikamilishwa, dhabihu hio kuu na wa mwisho ilitekeleza amri ya Musa (ona Alma 34:13–14) na ikamaliza (Mambo ya Walawi 17:11). Yesu alieleza jinsi vipengee vya dhabihu ya kale vilitekelezwa na Upatanisho na kukumbukwa kiashiria na sakramenti. Zingatia tena rejleo kwa maisha, mwili na damu.

"Basi Yesu akawaambia, Amin, amin, nawaambieni, Msipoula mwili wake Mwana na Adamu na kuinywa damu yake, hauna uzima ndani yenu.

"Aulaye mwili wangu, na kuinywa damu yangu, anao uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho" (Yohana 6:53–54).

Kwa sababu ya Upatanisho wa Yesu Kristo, kila mwana-damu—hata kwa wengi watakao—wataokolewa. Mwokozi alianza kumwaga damu Yake kwa wanadamu wote si kwa msalaba lakini katika ya Bustani la Gethsemani Pale alichukua juu Yake uzito wa dhambi za dunia ya wote waliowahi kuishi. Chini ya mzigo huo mzito, alitokwa damu kwenye kila kinyweleo (ona M&M 19:18). Mateso ya Upatanisho yalimalizwa kwenye msalaba Kalivari.

Umuhimu wa Upatanisho ulifupishwa na Nabii Joseph Smith. Alisema "Kanuni za msingi za dini yetu ni ushuhuda wa Mitume na Manabii, kuhusu Yesu Kristo, kwamba alikufa, akazikwa, na akafufuka tena siku ya tatu, na kupaa mbinguni; na mambo yote mengine ambayo yanahusiana na dini yetu ni viambatisho tu"<sup>1</sup>

Na mamlaka haya na shukrani ya dhati, Ninafundisha na kushuhudia juu Yake.

## Huduma ya Yesu Kristo—Mfano

Lengo la Bwana la pili la thamani sana duniani ilikuwa kushiriki kama mfano kwetu. Maisha yake ya mfano yalijumuisha huduma Yake duniani. Yalijumuisha mafundisho Yake, mifumbo na hotuba. Yalijumuisha Miujiza Yake, upendo mkarimu, na subira kwa watoto wa watu (ona 1 Nefi 19:9). Yalijumuisha matumizi Yake ya huruma ya mamlaka ya ukuhani. Yalijumuisha haira Yake ya haki aliposhutumu dhambi (ona Warumi 8:3) na alipotupilia meza ya wabadilishi pesa (ona Mathayo 21:12). Yalijumuisha pia huzuni Wake mkubwa. Alifanyiwa mzaha, na kupoigwa, na kukataliwa na watu Wake mwenyewe (ona Mosia 15:5)—hata kusalitiwa na mfuasi mmoja na kukataliwa na mwengine (ona Yohana 18:2–3, 25–27).

Hata vile vitendo vyake vya huduma vilikuwa vya kushangaza, havikuwa na bado si vya kipekee Kwake. Hakuna kipimo cha idadi ya watu ambao wanaweza kufuata mfano wa Yesu. Vitendo sawa na hivyo viimetendwa na manabii Wake na mitume na wengine mionganoni mwa washiriki Wake walio na mamlaka. Wengi wamevumilia mateso kwa ajili Yake (ona Mathayo 5:10; 3 Nefi 12:10). Katika wakati wetu, unajua akina ndugu na dada ambao wamevumilia kwa dharti—hata kwa matokeo mabaya—kuiga mfano wa Bwana.

Hivyo ndivyo inapaswa kuwa. Hiyo ndiyo tumaini Lake kwetu. Bwana anatuumba tufuate mfano Wake. Maombi yake yako wazi kabisa:

- “Mnapaswa kuwa watu wa aina gani? . . . Hata vile nilivyo, (3 Nefi 27:27; ona pia 3 Nefi 12:48).
- “Nifuateni, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu” (Mathayo 4:19).

- “Nimewapa kielelezo, ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende hivyo” (Yohana 13:15; ona pia Yohana 14:6).

Haya na maandiko mengine hayakuandi-kwa kama mapendekezo. Ni amri tukufu! Tunapaswa tuige mfano Wake!

Ili kusaidia matakwa yetu ya kumfuata Yeye, pengine tungezingatia vipengele vitano vya maisha Yake ambavyo tunaweza kuiga.

### Upendo

Ikiwa tungeuliza ni sifa gani ya maisha Yake ungetambua kwanza, ninadhani unge-taja sifa Yake ya upendo. Hiyo ingejumui-sha huruma, ukarimu, wema, fadhilli, uchaji Mungu, buraa, rehema, haki na mengine. Yesu aliwapenda Baba na mama Yake (ona Yohana 19:25–27). Alipenda familia Yake na Watakatifu (ona Yohana 13:1; 2 Wathesalonike 2:16). Alimpenda mtenda dhambi bila kukubali dhambi (ona Mathayo 9:2; M&M 24:2). Na alitufunza jinsi tunaweza kuonyesha upendo wetu Kwake. Alisema, “Mkinipenda, mtazishika amri zangu (Yohana 14:15). Kisha, ilikusisitiza kuwa upendo wake haukuwa bila matarajio, aliongezea, “Mkizishika amri zangu, mtakaa katika upendo wangu; kama vile mimi nilivyzishika amri za Baba yangu na kukaa katika pendo lake” (Yohana 15:10; ona pia M&M 95:12; 124:87).

Dhihirisho lingine la upendo wa Mwo-kozi ilikuwa utumishi Wake. Alitumikia Baba Yake, na alitumikia watu ambao aliishi nao na kufanya kazi nao. Kwa njia zote mbili tunapaswa tuige mfano Wake. Tunapaswa tumtumikie Mungu, “kwenda katika njia zake zote, na kumpenda” (Kumbukumbu la Torati 10:12; ona pia 11:13; Yoshua 22:5; M&M 20:31; 59:5). Na tunapaswa tupende majirani wetu kwa kuwatumikia (ona Wagalatia 5:13; Mosia 4:15–16). Tunaanza na familia zetu.

THE SERMON ON THE MOUNT, NA JAMES TISSOT; KIPACHIKWA: MAIEZO KUTOKA KWA CHRIST AND THE RICH YOUNG RULER, NA HEINRICH HOFMANN, KUFADHILWA NA C. HARRISON CONROY CO.



*S ifa inayo-tofautisha mafundisho ya Mwokozi juu ya yale yote ya walimu wengine ilikuwa ni kuwa alifundisha ukweli wa umuhimu wa milele. Ni Yeye pekee yake ndiye angeweza kutu-funulia lengo letu maishani.*



Upendo wa kina unaoshikanisha wazazi kwa watoto wao unaendelezwa kwa utumishi kwao katika wakati wao wa utegemeo kamilifu. Baadaye maishani watoto watiifu wanaweza kuwa na nafasi ya kulipiza upendo huo wanapotumikia wazazi wao wakongwe.

### **Maagizo**

Kipengele cha pili cha mfano ya Mwokozi kilikuwa usisitizo Wake wa maagizo matakatifu. Wakati wa huduma Yake duniani alionyesha umuhimu wa maagano ya wokovu. Alibatizwa na Yohana katika Mto Jordan. Hata Yohana aliuliza, “Kwa nini?”

Yesu alieleza, Kwa kuwa ndivyo itupasavyo *sisi* kuitimiza haki yote” (Mathayo 3:15; sisisitizo limeongezwa). Agizo halikuwa tu muhimu, ila mfano uliowekwa na Yesu na Yohana ulikuwa pia muhimu.

Baadaye Bwana alianzisha agizo la sakramenti. Alieleza ishara ya sakramenti na kutoa nembo zake tukufu kwa wafuasi Wake (ona Mathayo 26:26–28; Marko 14:22–24; Luka 24:30).

Baba yetu wa Mbinguni alipeana maelezo pia kuhusu maagizo. Alisema: “Lazima mzaliwe tena katika ufalme wa mbinguni, kwa maji na kwa Roho, na kuoshwa kwa damu, hata damu ya Mwanangu wa Pekee; ili mpate kutakaswa kutoekana na dhambi zote, na kufurahia maneno ya uzima wa milele katika ulimwengu huu, na uzima wa milele katika ulimwengu ujao, hata utukufu katika mwili usiokufa” (Musa 6:59).

Wakati wa shughuli za Bwana za baada ya muda duniani, maagizo ya juu ya wokovu yalifunuliwa (M&M 124:40–42). Amewezesha kwa ajili ya maagizo haya katika mahekalu Yake matukufu. Katika siku zetu, miosho, mitakaso, na mialikifisho yanapewa kwa watu binafsi ambao wamejitayarisha vizuri (ona M&M 105:12, 18, 33; 110:9; 124:39). Hekaluni, mtu binafsi aweza kuunganishwa na bwana ama mke, kwa wakongwe, na kwa uzao (ona M&M 132:19). Msimamizi wetu ni Mungu wa sheria na mpangilio (ona M&M 132:18). Lengo lake kwa maagizo ni sehemu kuu ya mfano Wake kwetu.

### **Maombi**

Kipengele cha tatu cha huduma ya mfano wa Bwana ni maombi. Yesu aliomba kwa Baba Yake wa Mbinguni na pia alitufundisha jinsi ya kuomba. Tunapaswa tuombe kwa

Mungu Baba wa Milele katika jina la Mwana Wake, Yesu Kristo, kupitia uwezo wa Roho Mtakatifu (ona Mathayo 6:9–13; 3 Nefi 13:9–13; Tafsiri ya Joseph Smith, Mathayo 6:9–15). Ninapenda Maombi Makuu ya Upatanisho yaliyotolewa na Bwana yaliyorekodiwa katika Yohana, sura ya 17. Ndani yake Mwana anazungumza wazi na Baba Yake kwa niaba ya wafuasi Wake, ambao Yeye anawapenda. Ni mfano wa maombi ya kufaa na ya huruma.

### **Maarifa.**

Kipengele cha nne cha mfano wa Bwana ni matumizi ya maarifa Yake matukufu. Kama ilivyorejelewa awali, wengi wasio Wakristo walikiri kuwa Yesu alikuwa mwalimu bora. Kweli, Alikuwa Lakini ni nini kilitofautisha mafundisho Yake? Je, alikuwa ni mwalimu hodari wa uhandisi, hesabu au sayansi? Kama Muumbaji wa dunia hii na mengine (ona Musa 1:33), kwa kweli angekuwa. Ama, kama Mbuni wa maandiko, angefundisha ubuni wa maandishi vizuri sana.

Sifa inayotofautisha mafundisho Yake juu ya yale yote ya walimu wengine ilikuwa ni kuwa alifundisha ukweli wa umuhimu wa *milele*. Ni Yeye pekee yake ndiye angeweza kutufunulia lengo letu maishani. Ni kumpitia Yeye pekee ndiko tungeweza kujifunza *maisha kabla ya maisha duni-an* na uwezo wetu wa *maisha baada ya maisha duniani*.

Wakati mmoja Mwalimu Bora aliwaambia wasikilizaji wake walioshuku kuwa wako na shuhuda tatu juu Yake:

- Yohana Mbatizaji
- Matendo ambayo yesu alikuwa amekamilisha.
- Neno la Mungu Baba wa Milele (ona Yohana 5:33–37).

Kisha akatoa shahidi nne: “Mwayachunguza maandiko; kwa sababu mnadhani ninyi mna uzima wa milele ndani yake: na hayo ndiyo yanayonishuhudia” (Yohana 5:39).

Neno *dhani* katika fungu hilo linaweza kwa mara ya kwanza kuonekana kuwa mahali halifai. Lakini ni muhimu kwa ajili ya maana Yesu alikuwa anajaribu kueleza. Ali-jua kuwa wengi wa wasikilizaji Wake bayana *walidhania* kuwa maisha ya milele yalikuwa katika maandiko. Lakini *walikosea*. Maandiko pekee yake *hayawezi* kupeana maisha ya milele. Kwa kweli kuna nguvu katika maandiko, lakini nguvu hiyo huja kutoka kwa Yesu Mwenyewe. Yeye

*ndiye* Neno: *Logos*. Nguvu ya uzima wa milele zi ndani Yake, ambaye “hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye neno alikuwa Mungu” (Yohana 1:1; ona pia 2 Nefi 31:20; 32:3). Kisha, kwa sababu ya ungumu wa wenyewe kushuku Wake, Yesu aliendelea kuwashutumu: “Wala hamtaki kuja kwangu mpate kuwa na uzima [wa milele]” (Yohana 5:40).

Bwana angetushinda na maarifa Yake ya kiungu, lakini hafanyi hivyo. Anaheshimu wakala wetu. Anaturuhuru furaha wa kugundua. Anatuhimiza kutubu makosa yetu wenyewe. Anaturuhusu kuwa na uzoefu wa uhuru unaokuja kutokana na kutaka kwetu kutii sheria Zake tukufu. Ndio, njia anayotumia maarifa Yake inatupatia sisi mfano mkuu.

### **Uvumilivu**

Kipengele cha tano ya uchungaji wa Bwana ni msimamo wake wa kuvumilia hadi mwisho. Katu hakujitoa kutoka kwa uteuzi Wake. Ingawa alipitia mateso zaidi ya yale tunayoweza kutafakari, hakuwa wa kulegea. Kupitia majaribio ya kina alivumilia hadi mwisho wa jukumu Lake: kulipia kosa kwa ajili ya dhambi ya wanadamu wote. Maneno Yake ya mwisho aliponing’inia msalabani yalikuwa, “Imeisha” (Yohana 19:30).

### **Matumizi Maishani Mwetu**

Vipengele hivi vitano vya huduma Yake vinaweza kutumika maishani mwetu wenyewe. Kwa kweli shuhuda bora za kusujudu kwetu Yesu ni kwetu kumuiga.

Tunapoanza kufahamu Yesu ni nani na kile ambacho ametutendea, tunaweza kuelewa, kwa kiwango fulani, mantiki ya amri ya kwanza na kuu: “Nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote” (Marko 12:30). Vingine, yote tunayofikiri na kutenda na kusema yapaswa yalloweshwe katika upendo wetu Kwake na Baba Yake.

Jiulize, “Kunaye ye yeyote ninayempenda zaidi ya Bwana?” Kisha linganisha jibu lako na viwango vilivyowekwa na Bwana:

- “Apendaye baba au mama kuliko mimi, hanistahili”
- “Ampendaye mwana au binti kuliko mimi, hanistahili” (Mathayo 10:37).

**M**aisha ya  
Bwana  
ya  
mfano yalijumui-  
sha huduma Yake  
wa muda duni-  
ani. Yalijumuisha  
mafundisho Yake,  
mafumbo na  
hotuba. Yaliju-  
muisha matumizi  
Yake ya huruma  
ya mamlaka ya  
ukuhani.



Upendo kwa familia na marafiki, hata kwa uzuri wake wote, ni wa kiini zaidi wakati unadhibitishwa katika upendo wa Yesu Kristo. Upendo wa wazazi kwa watoto una maana zaidi hapa na baadaye kwa sababu Yake. Mahusiano yote ya mapenzi yanatukuzwa katika Yeye. Upendo wa Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo unatupa mwangaza, uvutio na ushawishi kuwapenda wengine kwa njia bora zaidi.

*Maagizo* hutupa fokasi ya utumishi wa umuhimu wa milele. Wazazi wanapaswa wazingatie ni agizo gani linahitajika kufuatia kwa kila mtoto. Walimu wa nyumbani wanapaswa wafikirie kuhusu agizo la kufaa linalohitajika kufuatia katika kila familia wanaotumikia.

Mfano wa Mwokozi wa *maombi* unatukumbusha kuwa maombi ya kibinagsi, maombi ya familia, na utekelezaji wa uteuzi wetu katika Kanisa kwa maombi unapaswa kuwa sehemu ya maisha yetu. Kujua na kufanya matakwa ya Baba hutupa uwezo mkuu wa kiroho na kujiamini (ona M&M 121:45). Kwenye upande wa Bwana ndipo tunataka kuwa.

*Maarifa* “kuhusu vile vitu vilivyo, na vile vitu vitavyo-kuwa” (Yakobo 4:13) yanatukubalisha kutenda juu ya kanuni za kweli na mafundisho. Maarifa hayo yatainua kiwango chetu cha tabia. Vitendo ambavyo vingependekewza na hamu na hisia vitashindwa na vitendo vilivyou-ndwa na mantiki na haki.

Msimamo wa *kuvumilia hadi muisho* humaanisha kuwa hatutauliza kutolewa katika wito wa kuhudumu. Humaanisha kuwa tutavumilia katika kufutilia lengo la kustahili. Humaanisha kuwa hatutawai kukata moyo kwa ajili ya mpendwa ambaye amepotoka. Na humaanisha kuwa daima tutatunza mahusiano yetu ya milele ya familia, hata wakati wa shida ya ugonjwa, ulemavu au kifo.

Kwa moyo wangu wote ninaomba kuwa ushawishi unaobadilisha wa Bwana uweze ukalete tofauti ya kina katika maisha yako. Wito Wake na huduma Yake iweze kubariki kila moja wetu na milele na milele. ■

*Kutoka kwa hotuba ya mkutano ya ibada uliotolewa Agosti 18, 1998, Chuo Kikuu cha Brigham Young. Kwa nakala mzima katika Kingereza, nenda speeches.byu.edu.*

#### **MUHTASARI**


1. *Teachings of Presidents of the Church: Joseph Smith* (2007), 49.

# Wiki ya Pasaka

Mwokozi wetu Yesu Kristo alitekeleza Upatanisho—ambao ulijumuhiha mateso Yake Gethsemani, Usulubisho Wake kule Golgotha, na Ufufuo Wake kutoka kaburini—wiki ya mwisho ya maisha Yake.

Katika Baraza kule Mbinguni kabla dunia kuumbwa, Baba wa Mbinguni alitupa mpango Wake kwa ajili yetu, watoto Wake. Tulipiga kelele kwa furaha wakati Baba wa Mbinguni alimchagua Yesu Kristo kutekeleza mpango wa wokovu (ona Ayubu 38:7 na Ibrahimu 3:27). Akiwa amezaliwa na Maria kule Bethlehemu, Yesu aliishi maisha bila dhambi. Kwa sababu ya Upatanisho Wake, tunaweza kurudi kuishi na Baba yetu wa Mbinguni na kupokea uzima wa milele. Yesu Kristo atarudi tena kwa nguvu na utukufu kuishi duniani wakati wa Mileniumu, na atasimama kama Hakimu wa kila mtu siku ya mwisho.

Zifuatazo ni picha kutoka kwa video za Bibilia ambazo zinaeleza wiki ya mwisho ya maisha ya Mwokozi. Zingatia kusoma mistari ya maandiko iliyoorodheshwa kwa ajili ya kila picha. Kwa wendo wa kina wa kila tukio, rejelea upatanifu wa Injili nne katika Kamusi ya Bibilia, au Mwongozo wa Maandiko. Video za Bibilia zinapatikana [biblevideos.lds.org](http://biblevideos.lds.org).



*Siku ya tano kabla ya Pasaka, Yesu alibebwa kuingia Yerusalemu kwenye punda kama iliviotabiriwa. Watu walimtambua Yeye kama Mfalme wao, wakashangilia "Hosana" na kuweka nguo zao na matawi ya kuti ardhini mbele ya punda. (Ona Mathayo 21:1-11; Marko 11:1-11; Zekaria 9:9.)*



*Kwa mara ya pili wakati wa huduma Yake duniani, Yesu alisafisha kitala cha hekalu. "Nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala; bali ninyi mmeifanya kuwa pango la wanyang'anyi," aliwaambia wabadili pesa (Mathayo 21:13). Kisha wengi wa walio vipofu na walemavu wakaja Kwake hekaluni, na akawaponya. Lakini makuhani wakuu na waandishi walipoona miujiza Yake, wali-kuwa na hasira na wakatafuta njia ya kumwangamiza Yeye. (Ona Mathayo 21:12-17; Marko 11:15-19.)*

*Yesu Kristo, Mwana wa Pekee wa Baba, alijishusha hadhi kuja duniani kuokoa kila mtu kutokana na Kuanguka. (Ona 1 Nefi 11:16-22, 26-33; Alma 7:10-13.)*




*Wiki nzima, Mwokozi alitoa baadhi ya hotuba Zake za kukumbukwa, ikiwa mafundisho Yake juu ya senti ya mjane. (Ona Marko 12:41–44; Luka 21:1–4.)*

*Katika Bustani la Gethsemani, Mwokozi alipiga magoti na kuomba, mateso Yake kwa ajili ya dhambi ya dunia ku-sababisha Yeye “kutetemeka kwa sababu ya maumivu, na kutoka damu kwenye kila kinyweleo, na kuteseka mwili na roho” (M&M 19:18). Punde Yuda Eskariota na mkusanyiko wa watu walio-jiami walimkamata Yesu, na wanafunzi wote wakamwacha Bwana na kutoroka. (Ona Mathayo 26:36–56; Marko 14:32–50; Luka 22:39–53.)*



*Wakati wa chakula Chake cha mwisho, Yesu aliwaahidi mitume Wake kuwa wangepokea Mfariji, au Roho Mtakatifu, atakapokuwa ameenda. Aliwafundisha kumkumbuka kwa kupokea sakramenti. Mwishoni mwa usiku, Yesu alitoa Ombi la Upatanishi, ambapo aliomba kuwa wanafunzi wawzeza kuwa na umoja. (Ona Mathayo 26:17–30; Marko 14:12–26; Luka 22:14–32; Yohana 13–17.)*





Baada ya jaribio lisiohalali na mateso mabaya, Yesu Kristo alijitolea Mwenyewe kusulubiwa, akikamilisha "dhabihu kubwa na ya mwisho" iliyowezesha wokovu kwa watoto wote wa Mungu (ona Alma 34:14–15). Kabla ya giza kufika, wafuasi wa Yesu waliutoa mwili Wake msalabani, wakamvalisha kwa nguo ya kitani na vikolezo, na kumweka kaburini. (Ona Mathayo 27; Luka 23; Marko 15; Yohana 19.)



Asubuhi ya Jumapili ikapambazuka, na Maria Magdalena na wanawake wengine waaminifu wakafika kwenye kaburi kuupaka mafuta mwili wa Yesu zaidi. Walilipata jiwe la kaburi limetolewa na malaika wawili waliotangaza habari ya furaha: "Hayupo hapa, kwani amefufuka" (Mathayo 28:6). Mvokozi aliyefufuka alikuwa ameshinda kifo cha kimwili na kutuwezesha sisi sote kuishi tena: "Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa" (1 Wakorintho 15:22). (Ona Mathayo 28; Marko 16; Luka 24; Yohana 20). ■

# Kuwasakiia Watoto

## KUJITAYARISHA KWA AJILI YA UBATIZO

Na Jessica Larsen na Marissa Widdison

Majarida ya Kanisa

**U**ttoni ni msimu wa vitu vya mara ya kwanza vya furaha. Mara ya kwanza kuendesha balskeli, kuenta shulen, au kujaribu chakula kipyu ni baadhi ya matukio ya furaha yanayounda maisha ya mtoto. Kama watu wazima tuko na nafasi ya kuwasaidia watoto kwenye njia ya kugundua. Kama watu wazima Kanisani, tunayo pia nafasi ya kuwasaidia kukua katika injili (ona M&M 68:25). Tunaweza kufanya nini kuhakikisha ubatizo wa mtoto—agano la kwanza mtu hufanya na Baba yetu mpeendwa wa Mbinguni—ni tukio la kupendeza na la maana?

“Ni lengo la msingi la Kanisa hili kufundisha vijana: kwanza nyumbani kisha kanisani,” alifundisha Rais Boyd K. Packer.<sup>1</sup>

Katika mifano ifuatayo, wazazi wanashiriki jinsi walivowatayarisha watoto wao kwa ajili ya maagizo na maagano ya ubatizo na uthibitisho.

### Sisi Huanza Mapema

“Mwaka ambao kila mtoto anafika miaka saba ni wakati wa kusherekeea,” asema Lori, mama ya watoto wanne. Yeye na bwanake huwfundisha watoto wao kuhusu ubatizo kutoka siku wanapozaliwa. Hata hivyo, wakati kila mtoto hufika miaka saba, familia yao huanza matayisho ya kipekee zaidi. Wao huwa na somo la Mkutano wa Jioni wa familia nyumbani kila mwezi kuhusu mada tofauti zinazohusiana na ubatizo, kama vila maagano na mfano wa Yesu.

Lori anasema kuwa masomo katika mwezi wa kuzaliwa wa mwaka ya nane ya watoto huwa nyeti zaidi. Huwa anawaonyesha watoto nguo walizovaa walipopokea jina na baraka, na huzungumuzia siku ambayo agizo hilo lilifanywa.

“Ni wakati bora wa kulenga baraka za maagano ya hekalu,” Lori anangazia. “Sisi huhakikisha kila mara kuwa



tunafundisha kuwa chaguo la kubatizwa ni hatua ya kwanza katika kujitayarisha kwa ajili ya baraka za hekalu.”

### Sisi Huifanya kuwa Shughuli ya Familia

Monica, Mama ya watoto wanne, anapendekeza kuhwashughulisha watoto wakubwa kiasi katika kuwasaidia ndugu zao wadogo kujitayarisha panapowezeekana. “Kuwasikia ndugu au dada yao kijana akishuhudia na kushiriki uzoefu wake kwa kweli huongeza nguvu,” anasema. Lori huongeza kuwa wakati mwingine wao huuliza watoto



wanaojitayarisha kwa ajili ya ubatizo kufundisha yale walijifunza kwa ndugu zao wadogo.

#### Sisi Huitumia kama Kifaa cha Umisionari

Wakati binti wa Daniel alipofika miaka nane, alijua kuwa angetaka kushiriki siku yake ya ubatizo na marafiki wasiowashiriki wa Kanisa. Hivyo basi familia iliamua kuwalika marafiki kutoka shulen na ujirani kwa ubatizo wa Allison. Marafiki hawa waliombwa waje na mistari ya Bibilia wanayopenda katika ubatizo. Baada ya ubatizo, Allison aliweka

mstari kwenye vifungu katika jozi la maandiko yake mapya na akaandika majina ya marafiki wake kwenye ukingo.

“Ndio, kama familia yake, tulishughulika kabisa siku hiyo. Lakini tulimkubalisha pia kuwa na marafiki baadaye kwa muda na kuzungumza nao kuhusu kile alichohisi,” Daniel alisema. “Ilikuwa wakati mzuri sana kuona mtoto wetu akiweka mfano.”

#### Sisi Hufanya zoezi la Mahojiano ya Askofu

Kimberly, mama wa watoto wanaokaribia umri wa kubatizwa, anakumbuka akitembea katika ofisi ya askofu kwa ajili ya mahojiano yake ya ubatizo alipokuwa na umri wa miaka nane. “Nilikuwa na wasi wasi sana!” Kimberly anasema.

Sasa ye ye hujaribu kuhakikisha kuwa watoto wake hawakumbani na hisia za wasi wasi. Yeye na bwanake huzungumza na watoto wao kuhusu mahojiano ya askofu na kuwa uliza maswali kuhusu ubatizo katika maandhari kama ya mahojiano. Mahojiano haya hufanya zaidi ya kuwafahamisha watoto na mpangilio wa mahojiano — huwa pia yanawahimiza watoto kufikiria kwa kina kuhusu kile agizo la ubatizo linamaanisha kwao.

#### Tuko na Nafasi Mzuri

Wazazi hawa kwa upesi huashiria kuwa hawajafanya chochote vyta kupindukia katika kuwatayarisha watoto wao kwa ajili ya ubatizo na udhibitisho, lakini wengi wao walitumia maneno kama “kamili” na “dhabiti” kueleza masomo ambayo walifundisha kwa miaka iliyopita. “Tulihakikisha kuwa watoto wetu walifahamu kuwa hii ilikuwa hatua muhimu maishani mwao, na kuwa ilikuwa ni jambo kubwa,” Kimberly asema. Tulihakikisha kila mara kuwa tulikuwa wenyewe kuwatayarisha, na si tu kuwa na tumaini kuwa walimu wao wa Msingi walikuwa wakiwafunza.”

Ni nafasi nzuri vipi tumepewa kusaidia kuwatayarisha watoto tunaopenda kwa ajili ya ubatizo na udhibitisho! Tunapofanya hivyo kwa maombi, Bwana atakuwa nasi kufanyiza uzoefu huu wa kwanza wa kufanya agizo kuwa msingi mkuu wa ukuaji wa kiroho kwa siku za usoni. ■

*Kurasa mbili zifuatazo zinajibu maswali kadha ambayo watoto wanayo kuhusu ubatizo na udhibitisho.*

#### MUHTASARI

1. Boyd K. Packer, “Teach the Children,” *Liahona*, May 2000, 16.

## Kuelewa Ubatizo

Na Marissa Widdison

Magazeti ya Kanisa



### *Ni Nani atanibatiza?*

Yeyote atakaye kubatiza anahitaji kuwa na ukuhani—uwezo wa kutenda katika jina la Mungu. Wakati Yesu alitaka kubatizwa, Alimuendea Yohana Mbatizaji, ambaye alikuwa na ukuhani (ona Mathayo 3:13).

Mtu atakaye kubatiza atapata ruhusa kutoka kwa askofu au rais wa tawi.



### *Je, ni lazima niende chini ya maji ili kubatizwa?*

Yesu alibatizwa kwa kuzamishwa, inayomaanisha Alienda kabisa chini ya maji na kwa haraka kurudi juu tena. (ona Mathayo 3:16). Hivi ndivyo utakavyobatizwa. Kubatizwa katika njia hii kunatukumbusha kuwa tunawacha nyuma maisha yetu ya zamani na kuanza maisha mpya ya msimamo katika kumtumikia Mungu na watoto Wake.



### *Je, ni ahadi gani ninazoweka ninapobatizwa?*

Unapobatizwa, unafanya agizo, ama ahadi ya njia mbili, na Baba wa Mbinguni. Unamuahidi kuwa utfanya vitu fulani, na Yeye anaahidi kukubariki. Agano hili limeelezwa katika maombi ya sakramenti yanayosemwa kila Jumapili (ona M&M 20:77–79). Unaahidi:

- Kumkumbuka Yesu Kristo.
- Kutii amri Zake.
- Kuchukuwa juu yako jina la Kristo, ambayo humaanisha kuweka kazi Yake mbele maishani mwako na kufanya kile anachotaka badala ya kile dunia inataka.

Unapoweka ahadi hii, Baba wa Mbinguni anaahidi kuwa Roho Mtakatifu atakuwa nawe na kuwa dhambi zako zitasamehewa.



### **Roho Mtakatifu ni nini?**

Kipawa cha Roho Mtakatifu ni moja-wapo wa vipawa vya thamani kuu vya Baba wa Mbinguni. Ubatizo wako kwa maji si kamilifu hadi waume walio na Uku-hani wa Melkizediki wakupatie baraka ya kupokea Roho Mtakatifu (ona Yohana 3:5).

Roho Mtakatifu ni mshiriki katika Uun-gu. Yeye hushuhudia Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo na hutusaidia kujuua kile kilicho kweli. Yeye hutusaidia kuwa na nguvu kiroho. Yeye hutu-onya juu ya hatari. Yeye hutusaidia kujifunza. Roho Mtakatifu ana-weza kutusaidia kuhisi upendo wa Mungu.

Unapodhibitishwa kama mshiriki wa Kanisa, Roho Mtakatifu ana-weza kuwa nawe daima ukichagua haki.



### **Je, ni kwa nini ninafaa kuwa anglau wa umri mi- aka nane ili kubatizwa?**

Bwana anafundisha kuwa watoto hawapaswi kubatizwa hadi wawe wa umri ya kutosha kuelewa tofauti kati ya mema na mbaya, ambayo maandiko yanasema ni umri wa miaka nane. (ona Moroni 8:11–12; M&M 29:46–47; 68:27).



**Na Mzee**  
**Jairo Mazzagardi**  
Wa Wale Sabini

# Kuvutiwa Hekaluni

*Kwa wengi wa watu wema, hekalu huvutia  
hisia ambazo zinaweza kwa mara moja  
kuingia moyoni.*

**K**abla niitwe kama mshiriki wa Jamii ya Pili ya Wale Sabini, mke wangu nami tulikaa miaka mingi tukihudumu katika Mahekalu ya Campinas na São Paulo Brazil. Katika mahekalu yote mawili, nilishangazwa mara nyingi kuwa watu waliosafari kupita karibu na hekalu wangevutiwa kwake hadi wangesimama, waingie na kuuliza juu yake.

Walipoingia, tuliwajulisha kuwa hawangeweza kuendelea mbele zaidi bila matayarisho yafaayo. Kisha tulielezea lengo la hekalu, tukashiriki mafundisho machache ya msingi ya injili, na kuwaalika wao kukutana na wamisionari. Kwa wengi wa watu wema, hekalu lenyewe ni mmisionari mkuu kwa sababu linavutia hisia zinazoweza kwa mara moja kuingia moyoni.

Mke wangu, Elizabeth, nami tunazijua nguvu za hisia kama hivyo kihasili. Karibu miaka 40 iliyopita, rafiki mzuri na mwenzangu, mshiriki wa Kanisa, alianza kuleta mambo ya injili kwetu katika mazungumzo ya kawaida. Kwa mara kadha, aliwatuma wamisionari kututembelea. Tuliwependa wamisionari na tukakubali kuchukua mafunzo, lakini



hatukuwa na moyo wa kupendelea kujua yale waliyokuwa nayo ya kufundisha.

Hayo yalibadilika mnamo Oktoba 1978, ambapo mwenzangu aliwaalika marafiki kadhaa, ikitujumuisha sisi, katika ufunguzi wa Hekalu la São Paulo Brazil. Alikomboa mabasi kadhaa yeche mwenyeche ili marafiki zake wangeambatana naye hekaluni, umbali wa karibu maili 50 (80km).

Wakati Elizabeth alipoingia mahali pa kubatiza, alihisi kitu ambacho kamwe hajawaihisi tena, kitu ambacho aligundua baadaye kuwa Roho Mtakatifu. Hisia hio ilikuwa ni furaha tele moyoni mwake. Alijua katika dakika hio kuwa Kanisa lilikuwa la kweli na kuwa lilikuwa Kanisa alilotaka kushiriki.

Hisia sawa na hio ilinjia mimi mwishoni mwa ufunguzi huo, tulipotembezwa katika chumba cha kuunganisha na kufundishwa fundisho la familia za milele. Fundisho hilo lilingusa mimi. Nilikuwa nimefuzu katika weledi wangu, lakini nilikuwa nimehisi utupu katika nafsi yangu. Sikujua kile kingejaza shimo hilo, lakini nilihisi kuwa nilikuwa na kitu cha kufanya na familia yangu. Hapo, katika chumba cha kuunganisha familia, vitu vilianza kueleweka akilini na moyoni mwangu.

Siku chache tu, wamisionari walituongelesha tena. Wakati huu tulikuwa tunataka sana kusikiza ujumbe wao.

Wamisionari walituhimiza kuomba kila mara kuhusu ukweli. Niliamua hii ilikuwa njia pekee mimi *ningeweza* kuomba. Nilijuwa singefanya msimamo wa kuungana na Kanisa bila kuwa na ushuhuda wa kweli. Nilikuwa na wasi wasi wa kumjia Baba wa Mbinguni kuulizia udhibitisho kutoka Kwake, lakini wakati huo huo, nilijua ange-nijibu. Nilishiriki Naye matakwa ya kina ya moyo wangu na kumuuliza anipe jibu ambalo lingenihakikishia kuwa kuungana

na Kanisa kulikuwa njia sahihi.

Wiki iliofuata katika Darasa la Shule ya Jumapili, rafiki yetu aliyekuwa ametualika katika ufunguzi wa hekalu alikuwa amekaa nyuma yangu. Alisonga mbele na kuanza kunizungumzia. Maneno aliyosema yalijibu kabisa kile nilichokuwa nimeomba kujua. Sikuwa na shaka kuwa Baba wa Mbinguni alikuwa akinizungumzia kumpitia Yeye. Wakati huo, nilikuwa mtu mkali, mgumu, lakini moyo wangu ukayeyuka na nikaanza kulia. Rafiki yangu alipomaliza, alialika mke wangu nami kubatizwa. Tulikubali

Mnamo Oktoba 31, 1978, chini ya mwezi moja baada ya uzoefu wetu katika hekalu la São Paulo, tulibatizwa na kudhibitishwa. Siku ya pili tulishiriki katika kikao cha pili cha kuweka wakfu hekalu la São Paulo Brazil. Mwaka moja baadaye tulirudi hekaluni na wana wetu wawili kuunganishwa pamoja kama familia. Fursa zote tatu zilikuwa za kupendeza, na uzoefu za kukumbuka. Tumeendelea kukuza hisia hizo na ibada ya hekalu ya kila mara kwa miaka mingei.

Miaka ishirini na nane tangu siku tulibatizwa, mke wangu nami tulismama tena katika Hekalu la São Paulo Brazil. Nilikuwa nimeitwa kama rais wa hekalu. Ilikuwa uzoefu nyeti kwetu kutembelea ukumbi wa nyumba ya Bwana na kuhisi upya hisia nyeti zilizokuja vichochoeo vya uongofu wetu.

Hekalu linaendelea kumpatia mke wangu nami furaha kuu. Tunapoona wenzi vijana wakiingia hekaluni kuunganishwa kama familia ya milele, tunahisi tumaini kuu.

Watu wengi ulimwenguni kwote wako tayari kusikiza ujumbe wa injili. Wanahisi kiu sawa na nilichohisi zaidi ya miaka 30 iliopita. Hekalu na maagizo yake yana nguvu ya kutosha kukata kiu hicho na kujaza mashimo yao. ■

## KITU KILIKUWA KIBAYA NA NDEGE YANGU

Jioni moja nilipokuwa nikiendesha ndege yangu ililojaabiria kwenye barabara ya ndege, nilikuwa na hisia kuwa kitu kilikuwa kibaya na mfumo wa steringi ya ndege. Ili kuthibitisha ushawishi wangu wa kiroho, niliondoka kwenye njia ya kupaa na kufanya mageuzi machache ya digrii 360. Hakuna kilichoonekana kuharibika.

Nilishangaa, "Je, nipae na kuwapeleka abiria wanakoenda kwa muda mzuri, ama nirudi kwenye lango?" Nilijua kurudi ingesababisha kuchelewa sana. Njia ya kupaa huwa ni ya njia moja tu; ningehitajika kungoja wadhibiti njia wa chini kunitengeneza nafasi kuendesha kinyume cha nyendo. Kisha

ingetubidi tungoje kikosi cha urekebishaji kukagua ndege. Kuchelewa kungesababisha shida kwa shirika la ndege na kwa abiria waliokuwa na watu wakukutana na maunganisho ya kufanya. Pia niliwazia jinsi idara ya urekebishaji ingesema kuhusu repoti yangu kuwa ndege lilikuwa na shida wakati sikuwa na chochote cha kuonyesha ila tu hisia wa nguvu.

Kama kapteni wa ndege, nilikuwa na jukumu la usalama wetu, kwa hivyo nikaamua kufuata msukumo wangu na kurudi.

Tulipofika langoni, nilimwambia mekanika kuwa nilihisi kitu kilikuwa kibaya na ndege lakini sikuja

shida ilikuwa nini. Hakuamini kuli-kuwa na shida

"Pengine ilikuwa tu ni njia ya kupaa iliyokuwa na maji," alisema. "Unaweza kuwa ulikuwa unateleza kwenye lami." Alikubali, hata hivyo, kuangalia chombo cha steringi kwenye gurudumu la mbele. Baada ya kuiangalia, aliniuliza niwashukishe abiria ili aweze kupeleka ndege katika uendeshaji wa majoribio.

Aliporudi dakika 30 zilizofuata, alisikitika sana. Wakati wa uendeshaji wa majoribio, alikuwa amesikia suti ya kusagasaga. Alipofunga breki alipokuwa akigeuka kurudi katika lango, alipoteza udhibiti wa ndege na akawa karibu kuondoka kwenye njia ya kupaa.

Ukaguzi wa karibu ulifunua kuwa breki ziliikuwa zimepitia utengenezaji usiostahili jioni iliopita. Ningalishukisha ndege baada ya safari yetu, breki zingekataa, na ningepoteza udhibiti wa ndege.

Nilipokea ndege ingine ya kuendesha, na nikawapeleka abiria wangu kwa usalama walikokuwa wakienda masaa matatu baadaye.

Ninafurahia kuwa nilisikiliza ushawishi wa Roho. Ninajua kuwa Roho atatuongoza tukitafuta uongozi wa Bwana na kusikiliza ushawishi ambao unakuja. ■

Craig Willie, Utah, USA

**N**iliwazia jinsi idara ya urekebishaji ingesema kuhusu repoti yangu kuwa ndege lilikuwa na shida wakati sikuwa na chochote cha kuonyesha ila tu hisia ya nguvu.



# KUPATA FURAHA MAISHANI

**K**atika wakati mmoja nilikuwa nii kisoma hotuba ya mkutano mkuu ya Mzee Richard G. Scott wa Jamii ya Mitume Kumi na Wawili. Ingawa nilikuwa nimesikiza na kusoma hotuba hii awali, fungu moja lilinivutia na kubaki katika mawazo yangu.

Masaa machache baadaye mwana wangu, aliyekuwa akiishi katika fleti na marafiki, akaja matembezi. Alikuwa amehudumu katika misheni ya muda na kushiriki katika semesta chache za chuo. Alikuwa hana uhakika wa mwelekeo upi elimu angechukua na njia gani ya kazi angefuatilia. Kwa sababu alikuwa amechoshwa na kuhisi kuwa shule, kwa sasa, ilikuwa ni kupoteza wakati na pesa, alikatiza masomo yake na kuanza kufanya kazi kwa muda kamilifu.

Aliniambia kuwa mmoja wa marafiki zake alikuwa amependekeza kuwa waende katika kisiwa kule Bahamas ama Karebiani, wapate ajira, na kufurahia kwa miezi michache. Mwanagu alikuwa amefurahia kuhusu matarajio. Ningona kwa urahisi jinsi uzoefu kama huo usio na kujali ungekuwa wa kuvutia kwa kijana mvulana.

Hapo tu, ujumbe wa Mzee Scott wa busara ukaniija akilini. Nilichukua *Ensign* na kumsomea mwanagu yafuatayo: "Uko hapa duniani kwa lengo tukufu. Si kuburudishwa bila msimamo ama kuwa daima katika kufuatilia anasa wakati wote. Uko hapa kujari-biwa, kujidhibitisha ili uweze kupokea

baraka za ziada Mungu alizonazo kwa ajili yako. Athari ya kupunguza makali ya uvumilivu inahitajika", (*Finding Joy in Life, Ensign*, Mai 1996, 25).

Bila neno, mwanangu alilichukua jarida, akatembea mbali, na kusoma hotuba yote. Baadaye yote aliyosema ilikuwa kuwa hangeendelea katika safari yake ya kisiwani.

Kwa muda aliingia katika akademi ya polisi, njia iliomwelekeza kwa mke wake wa siku za usoni. Walioana katika Hekalu la Mesa Arizona na leo wanalea watoto watatu wazuri. Mnamo 2012 mwanagu alimaliza

shahada yake ya kwanza na kwa kweli "anapata furaha maishani."

Safari iliyopendekezwa ya mwanagu ingekuwa uzoefu mzuri, kwa upande mwingine, ingeweza kuwa hatari ya kiroho. Kila wakati ninapotafakari tukio hili, Roho hugusa moyo wangu.

Ninashukuru kwa ajili ya maneno ya manabii na kuwa nilishawishiwa kukumbuka hotuba ambayo ilinisaidia kutoa mwongozo. Ninashukuru pia kuwa mwanangu alisikiliza mjambe wa Bwana na kukubali Roho kumshawishi. Ninajua kuwa baraka nyingi na huruma huja tunaposikiliza na kufuata mafundisho ya Mwokozi na watumishi Wake. ■

Karen Rockwood, Idaho, USA



**W**akati mwanagu aliniambia kuwa mmoja wa marafiki wake alipendekeza kuenda Bahamas ama Karebian kujivinjari kwa miezi michache, ujumbe wa Mzee Scott ulinijia akilini.

# SIMU ILIKATIKA

M<sup>an</sup>ano Marchi 1997, nilipokuwa nikiishi katika jiji la Russia Rostov-on-Don, mume wangu nami tulibatizwa katika Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho.

Nilipojifunza mafundisho ya Kanisa, mengi ya maswsali yangu yalijibowi. Ilikuwa ya kuvutia kujifunza juu ya mpango wa wokovu, ikiwa pamoja na ibada ya ubatizo kwa wafu. Nilishangaa kujifunza kuwa tungeweza kubatizwa kwa niaba ya mababu zetu wafu.

Mwaka baada ya ubatizo wetu, rais wa misheni alitualika kujitayarisha

kuenda hekaluni. Kama sehemu ya maandalizi yetu, tulianza kufanya utafiti wa historia ya familia. Siku moja nilipokuwa nikifikiria kuhusu kufanya kazi hii, simu ikapigwa. Ilikuwa ni mama mkwe wangu. Nilimuuliza ikiwa angeweza kunitumia orodha ya mababu wafu upande wa familia ya mume wangu. Alishangaa na kuniambia kuwa ubatizo kwa ajili ya wafu haikuwa fundisho la Kristo lakini badala yake ni kitu Wamormoni walikuwa wametunga. Sikuwa na uhakika jinsi ya kumjibu kwa sababu sikuwa na ufahamu na marejeleo ya maandiko yaliyounga mkono fundisho.

Nilipokuwa nikifikiria jinsi ya kujibu, simu ilikatika. Sikuwa na uhakika kwa muda kile kilichokuwa kimetendeka, lakini nilikata simu na kuenda chumbani mwangu. Nilichukuuwa Agano Jipyä mkononi mwangu, nikapiga magoti kuomba, na kumuliza Baba wa Mbinguni kunionyesha ni wapi ningalipata jibu.

Mwishoni mwa ombi langu, Nilihingua Bibilia. Nilihisi ni kama mtu alikuwa amenieleza nisome mstari wa 29 wa kurasa ule ule niliokuwa nimefungua. Nilikuwa katika sura ya 15 ya 1 Wakorintho, ambayo inazungumzia fundisho la ubatizo kwa ajili ya wafu.

Nilikuwa nimeguswa na kushangaa kuwa Baba wa Mbinguni ali-kuwa amejibu maombi yangu kwa wakati huo huo. Ilikuwa ni hisia nzuri.

Nilikuwa nikiwazia kwa kina kuhusu uzoefu huu ambapo kwa ghafla simu ikalia tena. Ilikuwa ni mama mkwe wangu, akiuliza ni kwa nini simu ilikuwa imekatika. Nilimuambia sikuwa najua ni kwa nini lakini nikamuuliza afunque Bibilia yaka na asome 1 Wakorintho 15:29.

Siku chache baadaye orodha ya jamaa marehemu ilikuwa mezani mwangu. Mama mkwe wangu alikuwa amesoma maandiko na sasa aliamini kuwa Mwokozi, kupitia mtume Paulo, alikuwa amefundisha fundisho la ubatizo kwa ajili ya wafu.

Mungu ameahidi baraka kuu kwa wale ambao wanafanya kazi hii ya wokovu. Ninajua hii ni kweli. ■

Seda Meliksetyan, Armenia



Mama mkwe wangu aliniambia kuwa ubatizo kwa ajili ya wafu haukuwa fundisho la Kristo lakini badala yake ni kitu Wamormoni walikuwa wametunga.

# NINAWEZA KUPATA JARIDA KAMA HII WAPI?

**N**ilipokuwa katika safari na familia yangu kutoka Nevada, Marekani, kuelekea Alaska, Marekani, nilianzisha mazungumzo na mwanamke mrefu, mrembo, wa kirafiki katika njia baina ya viti.

Aliniuliza nilikokuwa nikienda, na nikamuambia tulikuwa tukielekea Juneau, Alaska, kumtembelea bi wetu na familia yake. Aliniambia kuwa alikuwa ametoka Las Vegas. Kisha, kwa hisia, akaongeza kuwa alikuwa anaenda Juneau kuwatemebelea wakwe zake ili kuwa na ushiriki wa kumbukumbu kwa ajili ya mumewe, ambaye alikuwa ameoana naye kwa miaka 20. Alikuwa ameaga hivi karibuni kuto-kana na saratani.

Niliangalia chini ya njia pana na kujiwazia jinsi nilikuwa na bahati kujua mpango wa wokovu na kuwa mhudumu wa hekalu katika Hekalu la Las Vegas Nevada. Nilijiuliza ni nini ningefanya mwanamke huyu ili kuinua nafsi yake.

Ghafla, kwa uwazi kama kengele, nilikumbuka nukuu na Rais Joseph Smith niliyokuwa nimepeana katika Muungano wa Usaidizi wa kina mama. Alipoanzisha Muungano wa Usaidizi wa kina mama, aliashiria kuwa kina dada “watapaa hadi kwa usaidizi wa mgeni; watamwaga mafuta na divai katika moyo uliojeruhiwa wa waliogandamizwa; watapanguza machozi ya mayatima na kufanya

**N**ilijiuliza ni nini ningeweza kumfanya ili kuinua nafsi ya mwanamke huyu, ambaye mumewe alikuwa ameaga hivi karibuni.



moyo wa mjane kuwa na furaha” (*Teachings of Presidents of the Church: Joseph Smith* [2007], 452).

Niliangalia katika njia pana mara nydingine. Nilimuona mgeni katika dhiki, mjane na moyo uliojeruhiwa. Nilikumbuka kuwa nilikuwa nimesoma *Ensign* ya Julai 2012 mapema siku hiyo. Ilikuwa na baadhi ya makala ya kuvutia ambayo nilidhani yangempa moyo na faraja.

Nilijipatia ujasiri wangu, nikafungua jarida kwa makala, na kumuliza asome. Nilimuangalia kwa karibu na nikashangaa kuwa alisoma kila mstari—kwa makini. Alipokuwa amemaliza, alisoma makala mengine.

Kwa dhahiri kitu alichokuwa amesoma kilimgusa moyoni. Alilikumbatia jarida kwa nguvu kifuani mwake na kisha akapanguza chozi machoni mwake.

“Ninaweza kupata Jarida kama Hili wapi?” aliniuliza. Nilimuambia kuwa angebaki nalo. Kisha akasoma zaidi.

Tulipofika Juneau, alishika mkono wangu, akaniangalia machoni, na kusema, “Asante.”

Nilijifunza funzo kuu kutoka kwa uzoefu huo. Tumezungukwa na wageni walio na miyo ilijojeruhiwa wanaohitaji neno jema la kuwafariji na ambao wanahitaji kujua kile ambacho sisi Watatifu wa Siku za Mwisho tunajua. ■  
Sharon Rather, Nevada, USA

*Wakati mwingine unalazi-mika kuwacha kitu kizuri kwa ajili ya kitu bora.*

# KUCHAGUA Sehemu BORA

**Na Matthew D. Flitton**

Majarida ya Kanisa

**S**iku moja Zoltán Szücs wa Sze ged, Hungary alimshangaza kocha wake wa kukayaki kwa kumuambia kuwa hangeenda Ujerumani kwa mashindano.

“Ilikuwa katika siku sawa na ubatizo wangu, kwa hivyo nilisema hapania,” Zoltán alisema.

Katika umri wa miaka 17, Zoltán alikuwa ameshinda mashindano mengi ya kukayaki. Ni mchezo maarufu katika Hungary, na Zoltán alikuwa mzuri—mzuri vya kutosha hadi kuwa mweledi alikuwa na uwezekano wa halisi. Zaidi ya kuamua kukosa shindano moja tu, Zoltán angewacha kukayaki kabisa hivi karibuni. Alikuwa na kitu bora cha kufanya

Kukayaki kulikuwa ni vizuri kwa Zoltán. Kwa miaka akifanya mazoezi na kocha wake, alikuwa amejifunza kujidhibiti, utiifu, na kutia bidii. Zoltán alikuwa amejifunza pia kuepuka dutu na tabia ambazo zingedhuru utendaji wake. Haikuwa maisha rahisi; ilikuwa ya upeweke, na kuelekea kuwa mweledi kungechukua muda zaidi. Weledi hufanya mazoezi masaa 12 kila siku na ni lazima washindane Jumapili.

“Kukayaki kulichukuwa muda wa masaa yangu,” Zoltán anasema. “Nili-kuwa mlokole. Kwa sababu hiyo, nili-wacha vitu vingi nje ya maisha yangu.”

Hiyo ndiyo sababu Zoltán aliamua kuwa hangeweza kujishughulisha mwenyewe yote katika injili na kukayaki pia. Mnamo 2004 alimuambia kocha wake hatakayaki tena.

Awali mwaka huo wamisionari walikuwa wameanza kumfundisha mamake Zoltán. Hakushiriki katika masomo. Alikubali shingo upande mwaliko wa ubatizo wa mamake. Lakini moyo wake uliguswa na yale ali-yohisi mara tu alipoingia katika jumba la kanisa. Zoltán alikubali kukutana na wamisionari, kwa sehemu kuwa angejitalbulisha nao.

Wamisionari walinivutia kwa sababu walikuwa ni watu wa kawaida lakini waliishi kiwango cha juu, anasema.

Kwa sababu ya kiwango cha juu ambacho Zoltán alikuwa tayari anaishi kama mkayaki, alikubali mafundisho ya injili kwa urahisi kama ya thamani. Alibatizwa miezi miwili iliyoofuata.

Mwanzoni alidhani kuwa angeendelea kukayaki lakini bila kufanya

mashindano Jumapili. Lakini kwa sababu yeye ni aina ya mtu ambaye, mara tu anapoamua kutekeleza shughuli au mwendo, anataka kufanya vyema, alichagua kuwachana na kukayaki kabisa.

Aliaribu mara moja kukayaki kama jambo la kupidisha wakati baada ya ubatizo wake. Alipofanya hivyo, kocha alimuomba asaidie kuwafundisha wengine na kupanga safari kwa vile yeye hangeshindana. Lakini hakutaka kujitolea katika kukayaki—ama shughuli ingine—ambayo ingezuia ufiasi wake.

Hivyo basi Zoltán akaweka kafi yake kando na kujitolea mwenyewe kwa huduma katika uamuzi una-otukumbusha ule Rais Howard W. Hunter (1907–95) alifanya alipooa. Rais Hunter alikuwa mwanamuziki shupavu ambaye alicheza vyombo kadhaa vya muziki. Jioni alikuwa akicheza katika orkestra, lakini maisha ya wale aliohusiana nao yalikuwa hayapatani na viwango vya injili. Kwa hivyo Rais Hunter aliviweka vyombo vyake vya muziki mbali na kuvitumia katika fursa za kuimba na familia peke yake.<sup>1</sup>



*Zoltán Szűcs, wa Sze-ged, Hungary, aliwacha kukayaki ili kuwa na muda zaidi kwa ajili ya injili.*

Zoltán anakosa kukayaki, lakini alitambua kuwa upendo wake wa kukayaki ulikuwa na nguvu ya kutosha kushindana na, na labda kushinda, upendo wake wa Bwana kama angelikaal karibu sana na mchezo huu.

Kanuni hio hio inaweza kutumika kwa shughuli yoyote ile ambayo inatutoa kutoka kwa yule ambaye Mungu anataka tuwe. Kwa kila moja wetu inaweza kuwa bora kupitia maisha bila vitu fulani—hata kama ni vitu vizuri—badala ya kuhatarisha maisha yetu ya milele ili kuwa navyo.

“Kanisa likawa maisha yangu,” Zoltán asema. “Kujua kwamba kuka-yaki hakungekuwa hai ningalitaka ku-shughulika na kuwa ingekuwa jambo la kustarehe tu, ikawa rahisi kuwacha. Badala, nilitaka kumweka Baba wa Mbinguni kuwa fokasi yangu.”

Zoltán akaanza kujifunza injili kwa nguvu sawa ye ye huleta kwa harakati yoyote ile. Akaweka lengo la kuhudumu misheni. Alitaka kubaki katika nchi yake na kuwafundisha wengine.

Alihudumu Hungary na sasa ana-fanya kazi kama mwalimu wa Kingereza wa sekondari. Anaendelea kuweka vipaumbele vyake katika injili. “Kuna vitu tunavyopaswa kuwacha kwa vile vinatuzuia na Mungu,” anasema. “Ni rahisi kuwachana na mabaya tunayoju tunapaswa. Mara nyingi hatutambua tunapopaswa kuwacha kitu kizuri kwa ajili ya kitu bora. Tunafikiria kuwa kwa sababu si kibaya, tunaweza kukishikilia na bado kufuata mpango wa Mungu.” Lakini Zoltán anajua kuwa ni lazima tuwache kile kizuri kama kinatuzuia kufuata mpango wa Mungu kwetu. ■

#### MUHTASARI

1. Ona Eleanor Knowles, *Howard W. Hunter* (1994), 81.

# Je, ninavezaje kueleza rafiki yangu kuwa kuvunja sheria ya usafi wa kimwili ni wazo baya?

**B**aba wa Mbinguni anataka tuwe na furaha na wakustahili Roho Wake, hivyo basi Anatupatia amri kutusaidia kuweka mawazo yetu, maneno, na vitendo ndani ya mipaka sahihi. Sheria ya usafi “wa kiwili husaidia kuweka nguvu za uzazi ndani ya mipaka ya ndoa. Sababu moja Yeye hutuamuru kwamba nguvu ya uzazi itumike tu kati ya mume na mke ni kwa sababu watoto wana haki ya kuzaliwa ndani ya vifungo vya ndoa.”<sup>1</sup>

Unawenza kushiriki nakala ya *Kwa Nguvu ya Vijana* na rafiki yako. Inatoa sababu kadhaa kwa nini ni vizuri kuweka sheria ya usafi wa kiwili: “Wakati wewe u msafi kimaadili ya kujamiihana, unajiandaa kufanya na kushika maagano matakatifu katika hekalu. Unajitarisha kujenga ndoa imara na kuleta watoto ulimwenguni kama sehemu ya familia ya milele na familia ya upendo. Unajikinga kutookana na uharibifu wa kiroho na kihisia ambaa huja kwa kushiriki urafiki wa kujamiihana nje ya ndoa. Unajikinga pia dhidi ya magonjwa hatari. Kubaki msafi kimaadili ya kujamiihana hukusaidia kuwa na ujasiri na furaha ya kweli na huboresha uwezo wako wa kufanya maa-muzi mazuri kwa sasa na baadaye.”<sup>2</sup>

## Hekalu



Baba yetu wa Mbinguni ana madhumuni tukufu kwetu sisi sote, na kusudi hilo linawezza kutimizwa katika hekalu. Tunapaswa tuwe wa kustahili kuingia hekaluni ili familia zetu ziweze kufunganihwa milele. Tutaishi na Baba yetu wa Mbinguni tena, na muhimu zaidi tutakuwa na furaha isiyo na mwisho, ambayo wasiostahili hawezi kuwa nayo.

Alofa M., umri miaka 18, Samoa

## Ndoa na Familia



Tunahimizwa kuwa wasafi kimaadili ya kujamiihana ili tuweze kuwa wa kustahili kuingia hekaluni na kushika maagano matakatifu. Tukifua sheria ya usafi wa kimwili, tunawenza kujenga ndoa imara na familia katika siku zijazo. Shetani daima atatujaribu, lakini kupitia maombi, maandiko, na marafiki wema, tunawenza kushinda.

Resty M., umri miaka 16, Philippines

## Matokeo Mabaya

Kuna matokeo mengi mabaya kwa kuvunja sheria ya usafi wa kimwili, lakini si yote unajifunza kuhusu katika darasa la afya. Kuvunja sheria ya usafi wa kimwili kunawenza kufukuza Roho nje ya maisha yako, kuumiza wale walio karibu nawe, na kufanya kujisikia vibaya kuhusu wewe mwenyewe. Ninapendekeza kutazama video ya Jumbe za Wamormoni iitwayo: “Usafi? Je, Ni nini Mipaka” [katika youth.lds.org katika Kiingereza, Kireno, na Kihispania].

Matthew T., umri miaka 17, Utah, USA

## Usafi na Heshima

Kwa kufuata sheria ya usafi wa kimwili, tunabaki wasafi mbele ya Mungu, tunajiheshimu, na tunawasaidia wengine kutuheshimu pia. Tukitii sheria ya usafi wa kimwili, tunaonyesha kwamba sisi ni watoto wa Mungu na kwamba tunazingatia viwango vya juu. Tutaepuka majuto. Tunapotii Baba yetu wa Mbinguni, hasa kuhusu sheria hii, maisha yetu yatakuwa ya furaha zaidi hapa duniani na katika ulimwengu ujao.

Alyana G., umri miaka 19, Philippines

## Kipawa Kitakatifu

Ikiwa kipawa cha uzazi kitadharau-liwa, kipawa hiki cha thamani kutoka kwa Mungu kingetendewa vibaya kama kitu cha kawaida. Kutoa kipawa haihisi kuridhisha kama mtu una-yempa hadhani ni maalum. Mmoja lazima daima atumie kipawa cha uzazi kwa utakatifu; kwa kuwa sisi sote ni mahekalu ya Mungu na tunapaswa tubaki wasafi kama hekalu.

*Jaron Z., umri miaka 15, Idaho, USA*



## Roho kuwa Nasi

Unapobaki kuwa msafi kutokana na dhambi, utakuwa mwenye furaha sana na utabarikiwa.

Miili yetu ni kama mahekalu, na Baba wa Mbinguni haishi katika mahekalu yaliyo machafu (Alma 7:21). Kwa hi-vyo tunapobaki kuwa wasafi kutokana na dhambi, Roho anaweza kuishi nasi.

*Maryann P., umri miaka 14, Arkansas, USA*

## Maswali Muhimu

Jibu swali la rafiki yako kwa kuuliza baadhi ya maswali: "Je, kama mwenzi wako wa siku zijazo angekuwa anakutazama wewe sasa?" Watu wote nimesikia kuhusu ambao wamevunja sheria ya usafi wa kimwili wamejuta kufanya hivyo. "Je, kama mtoto wako wa siku zijazo akikuuliza kama umevunja sheria ya usafi wa kimwili?" Rafiki yako anahitaji kujifunza jinsi sheria ya usafi wa kimwili ni muhimu sasa, kabla ya mwana au binti aulize swali hilo. Una-hitaji kujiweka kuwa msafi na hasili ili kuwa na maisha ya furaha, afya bila hatia ya kuvunja sheria takatifu.

*Robyn K., umri miaka 13, Utah, USA*

## Wema na Usafi



Bwana hufurahia wema na usafi wa kimwili, na kila kitu kinapaswa kufanyika kwa wakati wake ufaao. Sheria ya usafi wa kimwili ni amri kutoka kwa Bwana. Maombi na uenzi wa Roho ni mchanganyiko kamili wa kujua kwa-mba kuwa msafi kimwili ni baraka.

*Selene R., umri miaka 18, Nicaragua*

## Katika Ndoa

Ningemuelezea rafiki yangu kwamba kuvunja sheria ya usafi wa kimwili ni wazo baya kwa sababu nguvu ya uzazi imetengenezewa waliooana kisheria. Tunapovunja sheria ya usafi wa kimwili, tunapoteza Roho Mtakatifu katika maisha yetu.

*Augustina A., umri miaka 15, Ghana*

## MUHTASARI

1. Familia: Tangazo kwa Ulimwengu, *Liahona*, Nov. 2010, 129.
2. *Kwa Nguvu ya Vijana* (kijitabu, 2011), 35.



## KUVUNJA SHERIA YA USAIFI WA KIMWILI HUSABABISHA MADHARA MAKUBWA

Ndani ya agano la kudumu la ndoa, Bwana hukubalisha mume na mke ute-kelezaji wa mamlaka matakatifu ya uzazi katika uzuri wao wote na urembo ndani ya mipaka aliyoweka. . . .

"Hata hivyo, hayo matendo yameka-tazwa na Bwana nje ya ahadi ya kudumu ya ndoa kwa sababu yanadhoohofisha makusudi Yake. Ndani ya agano takatifu la ndoa, mahusiano kama hayo yako kulingana na mpango Wake. Yanapote-kelezwa katika njia ingine yoyote, yako kinyume na matakwa Yake. Yanasababi-sha madhara makubwa ya kihisia na ki-roho. Hata ingawa washiriki hawatambui kwamba inatendeka sasa, watatambua baadaye. Uasherati hujenga kikwazo kwa ushawishi wa Roho Mtakatifu."

**Mzee Richard G. Scott wa Jamii ya Mitume Kumi na Wawili, "Making the Right Choices," *Ensign*, Nov. 1994, 38.**

## SWALI LINALOKUJA

**Ninapaswa nifanye  
nini wakati mada  
inaletwa katika shule  
ambayo inakwenda  
kinyume na mafundi-  
sho ya Injili, kama vile  
kutoa mimba?**

Tuma jibu lako kabla ya Mei 15 kwa [liahona@ldschurch.org](mailto:liahona@ldschurch.org) ama na barua pepe kwa:

*Liahona*, Questions and Answers 5/13  
50 E. North Temple St., Rm. 2420  
Salt Lake City UT 84150-0024 USA

Majibu yanaweza kuhaririwa kwa ajili ya urefu na ufanuzi.

Taarifa ifuatayo na ruhusa lazima ijumuishwe katika barua pepe yako au barua: (1) jina kamili, (2) tarehe ya kuzaliwa, (3) kata au tawi, (4) kigingi au wilaya, (5) ruhusa yako ilioandikwa, na kama u chini ya miaka 18, ruhusa ilioandikwa na mzazi wako (barua pepe ina kubalika) ili kuchapisha majibu yako na azimio la hali ya juu ya picha.



**Na Rais**  
Thomas S. Monson

# JINSI YA KUHUDUMU KATIKA WITO WA UKUHANI

**J**e, umewahi kutafakari thamani ya nafsi ya binadamu? Umewahi kuijiliza kuhusu **uwezo** ambaou upo ndani ya kila mmoja wetu?

Niliwai kuhudhuria mkutano mkuu wa kigingi ambapo rais wa kingingi wangu wa zamani Paul C. Child alifungua Mafundisho na Maagano 18 na kusoma: “Kumbuka **thamani ya nafsi** ni kubwa mbele za Mungu” (aya ya 10).

Rais Child kisha akauliza, “ni nini thamani ya nafsi ya binadamu?” Alie-puka kuita askofu, rais wa kigingi, au mjambe wa baraza kuu kutoa jibu. Badala yake, alimchagua rais wa jamii ya wazee.

Mtu aliyegutushwa alibaki kimya kwa kile kilichoonekana kama milele na kisha akasema, “Thamani ya nafsi ni **uwezo wake wa kuwa kama Mungu.**”

Wote waliokuwa pale walitafakari jibu hilo Rais Child akaendelea na ujumbe wake, lakini

nikaendelea kutafakari juu ya jibu hilo lililovutiwa.

**Ili kufikia, kufundisha, kugusa** nafsi za thamani ambazo Baba yetu ametayarisha kwa ujumbe wake ni kazi kubwa. Mafanikio mara chache ni rahisi. Kwa ujumla unatanguliwa na **machozi, majaribio, uaminifu, na ushuhuda.**

Watumishi wa Mungu huchukua faraja kutoka uhakikisho la Bwana: “Mimi ni pamoja nanyi siku zote” (Mathayo 28:20). Ahadi hii kubwa inawainua nyinyi ndugu wa Ukuhani wa Haruni ambao mmeitwa kwa nafasi ya uongozi katika jamii ya mashemasi, walimu, na makuhani. Inawahimiza nyinyi katika maandalizi yenu ya kumtumikia katika eneo la misheni. Inawafariji ninyi wakati wa kukata tamaa, ambayo huja kwa wote.

**“Kwa hiyo, msichoke kutenda mema,”** asema Bwana, kwa kuwa mna-jenga msingi wa kazi kubwa. Na kutokana na mambo madogo huja yale yaliyo makuu.

Tazama, Bwana anahitaji moyo na akili yenye kukubali” (M&M 64:33–34). **Imani ya kudumu, uaminifu wa daima, na hamu ya dhati** daima zimetambulisha wale wanaomtumikia Bwana kwa mioyo yao yote.

Kama ndugu ye yeyote ndani ya mvumo wa sauti yangu wanajisikia hawajajandaa, hata hawezi kujibu wito wa kuhudumu, ili kujitolea, kubariki maisha ya wengine, kumbuka ukweli: “**Yule ambaye Mungu huita, Mungu humuwezesha**” ■

*Kutoka kwa hotuba ya mkutano mkuu wa Aprili 1987.*

## JE, UMETUMIA VIPI HAYA?

Kujua kuwa Bwana yu upande wangu kunanisaidia kukumbuka ni kwa nini ninaenda misheni: Kumtumikia Bwana na kuwaleta wengine kwa Mwokozi, Yesu Kristo. Najua hatanipitisha kwa chochote ambacho siwezi kuhimili wakati niko kwenye misheni yangu”

**Dilan M., Utah,  
USA**




## SHAURIANA NA BWANA

**N**ilipokuwa na umri wa miaka 15, nilimpenda msi-chana katika darasa langu shulenii na nilitaka kumpatia miadi. Alikuwa mrembo, lakini nilijililiza kama ninapaswa kumuliza awe nami kabla ya kuwa na umri wa miaka 16. Nilikumbuka Alma 37:37, ambayo inasema, "Shauriana na Bwana kwenye matendo yako yote, na atakuongoza kwa yale mema." Nikafanya hivyo. Niliomba na kusubiri siku kadhaa kwa jibu la Bwana kabla ya kufanya uamuzi.

Siku moja kanisani, Askofu wangu aliniita katika chumba na kunialika kutoa hotuba Jumapili ijayo. Fikiria mada ilikuwa gani? Usifanye miadi mpaka uwe angalau umri wa miaka 16. Nilihisu kuwa hii ilikuwa jibu la Bwana kwangu, na ilikuwa ni hapana. Ningewejaze kufundisha kitu ambacho sikuwa ninafanya?

Kwa sababu nilikuwa nimeushauriana na Bwana, niliweza kujifunza mapenzi ya Bwana kwa ajili ya maisha yangu na pia kuyakimbia majoribu. Najua kwamba tukishauriana na Bwana, Yeye atatuambia mapenzi Yake na tutabarikiwa sana.

Eduardo Oliveira,  
Ceará, Brazil



## ANDIKO LANGU PENDEZI

### MAFUNDISHO NA MAAGANO 24:8.

Andiko hili hunifanya nihisi vizuri ninapopitia majoribio kwa sababu linasema, "mimi nipo pamoja nawe, hata mwisho wa siku zako." Hii humaanisha kwangu mimi kwamba, nikimtafuta, Baba wa Mbinguni atakuwa pale daima pamoja nami mpaka mwisho wa maisha yangu.

Alex Ortiz, Nuevo Casas Grandes, Mexico



## NGUVU YA UPATANISHO

**W**akati wamisionari walinfundisha, mada kuu katika masomo yao ili-kuwa kila mara Yesu Kristo na Upatanisho Wake. Walieleza kwamba Upatanisho ni zawadi kutoka kwa Yesu Kristo kwa ajili ya kila mmoja wetu. Ni kipawa ambacho tunaweza kutumia katika maisha yetu ya kila siku tunapokabiliwa na majoribio au tunapotenda dhambi. Nguvu ya Upatanisho inainua, inaponya, na inatusa-dia kurudi kwenye njia adilifu


na nyembamba ambayo inangoza hata maisha ya milele.


Wamisionari walipokuwa wakishiriki haya, nilipata hisia kali ilioshuhudia kuwa ilikuwa ni ya kweli, na nikaamua kuji-uniga na Kanisa.

Baadaye niliamua kuhudumu katika misheni kwa sababu nilitaka kusaidia wengine kujua kuhusu kipawa hichi cha ajabu. Kwa kufundisha na kushiriki kuhusu Upatanisho, nimeona wengine wakibadilika kwa njia mpya ya maisha. Badiliko kamili lilinjia, si tu kwa kusikia kuhusu Upatanisho lakini kwa kuutumia katika maisha yangu pia.


Najua kwamba Upatanisho ni halisi. Tunapokaribisha ushawishi wake katika mai-sha yetu, haijalishi ni hali gani tunakabiliana nayo, kila kitu kinaweza kushughulikiwa na tutahisi furaha.

Ioriti Taburuea, Kiribati





Bibilia Takatifu



Kitabu cha Mormoni

KWA NINI TUNAHITAJI

# KITABU CHA MORMONI

Baadhi ya watu wanaweza kukuliza ni kwa nini tunahitaji Kitabu cha Mormoni wakati tayari tuna Biblia. Kwa kweli, Yesu Kristo alishuhudia kuwa hili lingetokea (ona 2 Nefi 29:3). Kuna sababu nyingi kwa nini Kitabu cha Mormoni ni muhimu katika siku yetu (kwa mfano, ona 2 Nefi 29:7–11). Hizi ni sababu chache tu kwa nini ni muhimu.

## Ushahidi Mwingine wa Yesu Kristo

Maandiko yanatuonyesha mpangilio wa kutumia mashahidi wengi ili kudhibitisha ukweli katika Kanisa la Kristo. Kitabu cha Mormoni kinongeza ushahidi wa pili kwa Biblia kama ushuhuda wa Kristo. Mzee



## MASHAHIDI WAWILI

“Biblia ni mmoja wa ushuhuda wa Yesu Kristo, Kitabu cha Mormoni ni mwingine. Kwa nini huu ushuhuda wa pili ni muhimu hivyo? Mchoro ufuatao unaweza ukasaidia: Unaweza kuchora mistari ngapi iliyonyooka kupitia kituo kimoja kwenye kipande cha karatasi? Jibu ni mingi. Kwa muda, tuseme kituo hicho kina wakilisha Biblia na kwamba mamia ya mistari hio iliyonyooka iliyochorwa kupitia kituo hicho inawakilisha tafsiri tofauti za Biblia na kwamba kila moja ya tafsiri hizo zinawakilisha kanisa tofauti.

Nini kinafanya, hata hivyo, ikiwa kwenye kipande hicho cha karatasi kuna kituo kingine kinachowakilisha Kitabu cha Mormoni? Mistari mingapi iliyonyooka inaweza kuchorwa katy ya pointi hizi mbili za rejeleo: Biblia na Kitabu cha Mormoni? Moja tu. Ufafanuzi mmoja tu wa mafundisho ya Kristo unawezakusalia ushuhuda wa ushuhuda huu muwili.

Tena na tena Kitabu cha Mormoni kinasimama kama ushuhuda, thibitisho, fafanuzi, unganishi ya mafundisho yanayofundishwa katika Biblia.

**Mzee Ted R. Callister wa Urais wa Wale Sabini, “Kitabu cha Mormoni—Kitabu kutoka kwa Mungu,” Liahona, Nov. 2011, 75.**

Mark E. Petersen (1900–84) wa Jamii ya Mitume Kumi na Wawili aliwaikusema, “Sababu kuu tuna Kitabu cha Mormoni ni kwamba kwa mawai-dha ya mashahidi wawili au watatu, mambo yote yatadhihirishwa. (Ona 2 Wak. 13:1.) Tuna Biblia, pia tuna Kitabu cha Mormoni. Vinajumuisha sauti mbili—maandishi mawili ya ma-andiko—kutoka kwa watu wawili wa kale walotenganishwa kwa upana, wote wakishuhudia uungu wa Bwana Yesu Kristo.”<sup>1</sup> Rais Ezra Taft Benson (1899–1994) ameongeza, “Tusisahau kwamba Bwana mwenyewe alitoa Kitabu cha Mormoni kama ushahidi mkuu Wake.”<sup>2</sup>

### Ukamilifu wa Injili

Tunajua kwamba “mambo wazi na ya thamani yalichukuliwa kutoka” Biblia katika wakati (1 Nefi 13:40). Kitabu cha Mormoni kinafanua ma-fundisho ya Kristo na kuleta utimilifu wa injili duniani mara nyingine tena (ona 1 Nefi 13:38–41). Kwa mfano, Kitabu cha Mormoni kinatusaidia ku-jua kwamba ubatizo lazima ufanywe kwa kuzamishwa (ona 3 Nefi 11:26) na kwamba watoto wadogo hawana haja ya kubatizwa (ona Moroni 8:4–26).

### Kitovu cha Kanisa la Urejesho

Joseph Smith alishuhudia ya kwa-mba Kitabu cha Mormoni ni “jiwe kuu la msingi katika dini yetu”<sup>3</sup> (utangulizi wa Kitabu cha Mormoni). Kwa vile tunajua haya, haionekani bahati mbaya kwamba Kanisa la Yesu Kristo wa Watatifu wa Siku za Mwisho liliundwa

April 6, 1830, siku 11 tu baada ya Kitabu cha Mormoni kuwa kinapati-kana kwa mauzo kwa umma mnamo Machi 26, 1830. Kanisa halikuundwa mpaka maandiko yake makuu ya msingi yalikuwa yanapatikana kwa washiriki wake.

### Baraka katika Maisha Yetu


Kuhusu Kitabu cha Mormoni, Joseph Smith alifundisha kwamba “mtu angemkaribia Mungu zaidi kwa kufuata mafunzo yake, zaidi ya kitabu kingine.”<sup>4</sup> Kina uwezo wa kuba-dilisha maisha—ikiwa ni pamoja na yako na ya wale unaoshiriki Kitabu cha Mormoni nao. Rais Henry B. Eyring, Mshauri wa Kwanza katika Urais wa Kwanza, ameshuhudia, “Athari ya Kitabu cha Mormoni juu ya tabia yako, nguvu, na ujasiri kuwa shahidi wa Mungu ni wazi. Mafundisho na mifano ya ujasiri katika kitabu hicho itakuinua, itakuongoza na kukutia moyo. Kujifunza Kitabu cha Mormoni kwa maombi kutajenga imani katika Mungu Baba, katika Mwanawe Mpewda, na katika injili Yake. Kutajenga imani yako katika manabii wa Mungu, wa kale na wa kisasa. Kunaweza kukuleta karibu na Mungu kuliko kitabu chochote ki-ningine. Kinaweza kubadilisha maisha kuwa bora.”<sup>5</sup> ■

### MUHTASARI

1. Mark E. Petersen, “Evidence of Things Not Seen,” *Ensign*, May 1978, 63.
2. *The Teachings of Ezra Taft Benson* (1988), 204.
3. Joseph Smith, katika utangulizi wa Book of Mormon.
4. Joseph Smith, katika utangulizi wa Book of Mormon.
5. Henry B. Eyring, “A Witness,” *Liahona*, Nov. 2011, 69–70.



## JIUNGE NA MAZUNGUMZO



**A**prili mzima mtakuwa mkijifunza kuhusu Uasi na Urejesho katika jamii zenu za ukuhani na Wasichana na Madarasa ya Shule ya Jumapili (kama kata yako au tawi lina masomo mapya katika lugha yako). Kuja kwa Kitabu cha Mormoni kulikuwa ni sehemu muhimu ya Urejesho. Baada ya kusoma makala haya, fikiria jinsi maisha yako ni tofauti kwa sababu una Kitabu cha Mormoni. Unaweza kuandika hisia zako katika shajara yako na fikiria kuzishiriki na wengine kwa kushuhudia nyumbani, kanisani, au kwenye vyombo yva habari yva kijamii.



UKUAJI KATIKA  
UDONGO WA RUTUBA:  
VIJANA WAAMINIFU NCHINI

Na Cindy Smith

# UGANDA



Wanapokubali na kuishi Injili ya Yesu Kristo, vijana nchini Uganda wanaona imani na tumaini likukua kwote karibu nao.

**K**atikati mwa Afrika Mashariki, nchi nzuri ya Uganda imebarikiwa na milima mingi yenye miwa na migomba ya ndizi—na vijana waliotayari kukubali na kuishi Injili ya Yesu Kristo.

Kigingi cha kwanza Uganda kiliundwa mwaka 2010. Kanisa linakua kwa kasi, na wavulana na wasichana wengi katika kila kata na tawi.

### Kupandisha Bendera, Kuwa Mfano

Wasichana katika kata moja walivutwa na mafundisho ya Dada Elaine S. Dalton, Rais Mkuu wa Wasichana, juu ya wema: “Sasa ni wakati kwa kila mmoja wetu kuinuka na kupeperusha bendera kwa kuita ulimwengu kurudi kwa wema.”<sup>1</sup> Wasichana walipanda mlima ulio juu ya mji na kuinua bendera za dhahabu kuashiria ahadi zao za kuwa mifano wa wema. Pamoja waliimba “High on the Mountain Top” (*Wimbo*, nambari. 5).


Wasichana hawa wamepandisha viwango vyao vya kibinafsi vya haki. Utiifu wao umeimarisha ushahidi wao na kushawishi wengine. Dada Dalton amesema, “Kamwe usiwaikudharau nguvu za ushawishi wako wa wema”<sup>2</sup> Na kama bendera, mfano wa wasichana hawa unapepea ulimwenguni kote.

Kama wasichana wengi nchini Uganda, Sandra hutembea zaidi

ya maili kuenda kanisani, husaidia kusafisha kanisa siku ya Ijumaa, na huhudhuria seminari Jumamosi. Wakati wa wiki, ye ye huamka kabla ya 11:00 asubuhi kusoma vitabu vya shulenii, na kisha hutembea kuenda shule, kurudi nyumbani baada ya saa 12:00 jioni. Alikosa mwaka wa shule kwa sababu ya matatizo ya kifedha lakini hukumbana na changamoto yake kwa mtazamo mzuri: “injili kwa kweli imenisaidia kukaa imara na kutohamishika.”

Sandra ni mshiriki wa pekee wa Kanisa katika familia yake, lakini wazazi wake husaidia huduma yake

Sandra





*Juu: Vijana wanahudhuria ibada ya kigingi pamoja  
Juu: Susan (katikati),  
mkimbizi nchini Uganda,  
alipata amani katika Injili  
na aliwaleta ndugu zake na  
watoto wengine kanisani.*

*Katikati: Wasichana wa  
kata hii wanafurahia kazi ya  
Maendeleo ya Kibinafsi.*

*Kulia: Dennis aliwachana  
na timu ya kadanda ya ku-  
lipwa ili kuhubiri Injili. Yeye  
na vijana wengine katika  
jamii yake ya ukuhani walijitelea na kushinda changa-  
moto ili kuhudumu misheni.*

ya Kanisa, kama vile kusaidia wakati kata ilisafisha viwanja vya watoto mayatima mtaani. Familia yake huona jinsi injili imemsaidia kuwa na nguvu, hata wakati anakabiliwa na matatizo ambayo hayajasuluhishwa. Akitafakari juu ya chanzo cha nguvu hio, Sandra anasema, "Ninapoenda Kanisani, ninajisikia kama ninavalia silaha za Mungu" (ona Waefeso 6:11–17).

Mwongofu wa hivi karibuni, Susan, analipenda Kanisa. Mzaliwa kutoka Sudan Kusini, familia yake ilikimbia

taabu na ikabarikiwa kupokea wa-misionari katika Uganda. Kama mki-mbizi, alipata amani na ulinzi katika Injili. Siku za Jumapili angewaleta ndugu zake wadogo kanisani, na pia watoto wengine 10 ambaao si washiriki wa Kanisa. Baada ya kifo ghafula cha mwana familia, alirudi Sudan Kusini, ambapo anasubiri Kanisa liundwe katika eneo lake. Susan na Sandra wote wanakumbana na changamoto, lakini wanategemea Mungu na kufurahia matunda ya kuishi Injili ya Yesu Kristo (ona Alma 32:6–8, 43).

### **Kujitolea Kuhudumu katika Misheni**

Vijana nchini Uganda huanza kucheza kandanda kama wavulana wadogo, wakitumia matawi ya yaliyofumwa kama mpira. Tangu alipokuwa mdogo sana, Dennis alikuwa na kipaji cha mchezo, na shule yake ya sekondari ilimpa udhamini ili kuchezea timu yao. Baada ya kumaliza shule ya sekondari, timu





ya kulipwa ilimpa malipo, chumba, na malazi. Ilikuwa ni ndoto ya kuwa kweli, lakini Dennis alijua hii ingeharibu mipango yake ya kwenda msheni baadaye katika mwaka.

Hamu ya Dennis kufanya kile Baba yake wa Mbinguni alimtaka afanye



ilikuwa kubwa sana kana kwamba hakutaka hata kujaribiwa kubaki katika timu wakati ungefika kwake kushiriki misheni. Watu wengi walihoji uchaguzi wake, lakini Dennis yu dhabiti kuwa alifanya uamuzi wa haki—kwa ajili yake mwenyewe na wengine. “Ndugu zake wawili wadogo na dadeke mdogo walibatizwa,” anasema. “Sikuwai kamwe kufikiria kuwa dangu angesikia Injili. Ninapomuona Mungu akifanya miujiza katika familia yangu, inanipa matumaini kwa ajili ya siku zangu za usoni.”

Katika kata ya Dennis wavulana hujifunza *Hubiri Injili Yangu* kila wiki. Wamekuwa kama timu, wakifanya kazi kwa karibu na wamisionari wa muda na kuleta marafiki kwa mikutano ya Jumapili na shughuli zingine, ikiwa ni pamoja na mpira wa kikapu

na michezo ya kandanda wakati wa wiki. Makuhani wamewabatiza marafiki na wengine walisaidia kuwafunza pamoja na wamisionari. Zaidi ya miaka kadhaa, timu hii ya vijana imeimarisha kata nzima, na wanenye wao, ikiwa ni pamoja na Dennis, walipokea wito kuenda katika Misheni ya Kenya Nairobi.

Wamefuata ushauri wa Mzee Daudi A. Bednar wa Jamii ya Mitume Kumi na Wawili “kuweni wamisionari kitambo kabla mwasilishe makaratasi yenu ya misheni.”<sup>3</sup> Walifanya hivyo kwa kufanya kazi pamoja kama jamii, timu bora kuliko yoyote nyingine.

Wamisionari wote wanenye walishinda changamoto ili kuhudumu. Wilberforce anaelezea, “Nilikuwa karibu kupoteza matumaini ya kwendwa misheni kwa sababu ya gharama, lakini basi nikasoma Mathayo 6:19–20: ‘Usijiwekee hazina duniani lakini jiwekeeni hazina wenywewe mbinguni.’ Kwa hivyo kwa bidii na kujitolea, niliweza kutimiza lengo langu la kuhudumu misheni ya muda. Naipenda huduma ya umisionari. Hakuna kilicho bora kuliko kutafuta kwanza ufalme wa mbinguni.”

### Matumaini kwa Siku za Usoni

Vijana wa Uganda wanasaidia kujenga ufalme wa Mungu hapa, na tumaini kubwa kwa ajili ya siku zizazo. Ingawa hakuna hekalu Afrika Mashariki, vijana huangazia wakati wataao katika hekalu lililo mbali. Shughuli moja ya kigingi ililenga kujiardaa kuingia hekaluni, na katika hitimisho,

mshiriki wa urais wa kigingi akatoa ushuhuda wake: “Mungu anawapenda. Nyinyi ndio siku za usoni za Kanisa nchini Uganda.” Vijana hawa wenye haki tayari wana ushawishi mkubwa.

Wavulana na wasichana wa Uganda wanaacha mambo ya dunia kwa ajili ya baraka ambazo zitadumu milele. Wamepanda mbegu ya imani na wanailisha na kuitunza (ona Alma 32:33–37). Kama mtu ulioja na matunda (ona Alma 32:42), vijana hushiriki furaha ya injili katika nchi hii yenye rutuba. ■

*Cindy Smith aliishi nchini Uganda wakati mumewe alifanya kazi huko, na sasa wanaishi Utah, Marekani.*

### MUHTASARI

- Elaine S. Dalton, “A Return to Virtue,” *Liahona*, Nov. 2008, 80.
- Elaine S. Dalton, *Liahona*, Nov. 2008, 80.
- David A. Bednar, “Becoming a Missionary,” *Liahona*, Nov. 2005, 45.





# Je, ni nini RAFIKI WA KWELI?

Na Elaine S. Dalton

Rais Mkuu wa Wasichana

**M**aelezo ya rafiki yamebadilika katika dunia ya leo iliounganishwa kiteknologija. Leo unaweza kufikiri kuwa una “marafiki” wengi. Ni kweli: tunafurahia uwezo wa kuwa na taarifa na kujua kwa usasa yale yanayotokea katika maisha ya wengi wa marafiki zetu na vile vile marafiki wa sasa na wa zamani na hata watu ambao hatujakutana nao kibinasi tunaowaita marafiki zetu.

Katika muktadha wa vyombo vya habari vya kijamii, neno “rafiki” mara nyangi hutumika kuelezea *mawasiliano* badala ya *mahuasiano*. Una

uwezo wa kutumia “marafiki” zako ujumbe, lakini hii si sawa na kuwa na uhusiano na mtu ana kwa ana.

Wakati mwagine shughuli yetu ni kwa *kuwa* na marafiki. Pengine tunapaswa kuzingatia *kuwa* rafiki.

Kuna maelezo mengi ya nini maana ya kuwa rafiki. Kamwe sitawai kusahau kumsikia Mzee Robert D. Hales wa Jamii ya Mitume Kumi na Wawili akizungumza kuhusu maana ya kuwa rafiki na ushawishi wa nguvu ya marafiki katika maisha yetu. Maelezo yake yamekuwa na madhara ya kudumu

katika maisha yangu. Alisema, “Marafiki ni watu ambao hufanya kuwa rahisi kuishi Injili ya Yesu Kristo.” Kwa maana hii, kutafuta wema wa juu wa mtu mwagine ni kiini cha urafiki wa kweli. Ni kuweka mtu mwagine kwanza. Ni kuwa madhubuti mwamini, mwajibikaji, na mwenye maadili katika kila kitendo. Pengine ni neno *ahadi* ambalo linafungua maana halisi ya urafiki.

Wakati binti yangu, Emi, alikuwa miaka 15, alifanya uamuzi kuhusu aina gani ya rafiki angeweza kutafuta. Asubuhi moja niliona nakala yake ya Kitabu cha Mormoni imefunguliwa katika Alma 48. Alikuwa ameweka alama mistari iliyomwelezea Kapteni Moroni: “Moroni alikuwa mtu mweenye nguvu na shujaa; alikuwa mtu wa uelewa kamili. Naam, na ye ye alikuwa ni mtu ambaye alikuwa imara katika imani ya Kristo” (mistari 11, 13). Katika ukingo alikuwa ameandika, Nataka kufanya miadi na kuolewa na mtu kama Moroni.

Nilivyomtazama Emi na aina ya vijana alijihuisha nao na baadaye kufanya miadi alipokuwa miaka 16, ningeona kuwa alikuwa akiiga sifa hizo mwenyewe na kuwasaidia wengine kuishi kwa utambulisho



wao kama wana wa Mungu, wamiliki wa ukuhani, na kina baba wa na viongozi wa siku za usoni.

Marafiki wa kweli ushawishi wale ambao wanajihusisha nao kupanda kidogo juu [na] kuwa bora kidogo. Mnaweza kusaidiana, hasa wavulana, kuijandaa kwa ajili ya kuhudumu misheni ya heshima. Mnaweza kusaidiana kubaki wasafi kimaadili. Ushawishi wako mwema na urafiki unaweza kuwa na athari ya milele si tu katika maisha ya wale ambao wanajihusisha nao lakini pia kwa ajili ya vizazi vijavyo.

Mwokozi aliwaita wanafunzi Wake marafiki. Yeye alisema.

“Hii ni amri yangu, Mpendane, kama nilivyowapenda ninyi.

“Hakuna mtu aliye na upendo kumshinda huyu, kwamba autoe hai wake kwa sababu ya marafiki zake.

“Ninyi ni marafiki zangu, ikiwa nyinyi mnafanya ninayowaamuru.

“Siwaiti tena watumishi, maana mtumishi hajui anachofanya bwana wake, lakini ninyi nimewaita *marafiki*; kwa kuwa yote niliyoyasikia kwa Baba yangu mimi nimewajulisha ninyi” (Yohana 15:12–15; mkazo imeongezewa).

Unapoishi na kushiriki injili ya Yesu Kristo, utawavutia watu kwako ambao watataka kuwa marafiki zako—si tu mtu kwenye tovuti ya kijamii lakini ile aina ya rafiki Mwokozi alielekezea kwa maneno yake na mfano wake. Unapojitahidi kuwa rafiki kwa watu wengine na kuwacha nuru yako

iangaze sana, ushawishi wako utabariki maisha ya wengi ambao unajihu-sisha nao. Najua kuwa unapolenga kuwa rafiki kwa watu wengine, kama inavyoelezwa na manabii na mi-fano katika maandiko, utakuwa na furaha na utakuwa ushawishi kwa ajili ya wema duniani, na siku moja utapokea ahadi tukufu iliotajwa katika maandiko kuhusu urafiki wa kweli: “Uhusiano huu huu uliopo mi-ongoni mwetu hapa utakuwepo mionganoni mwetu kule, isipokuwa utazidishwa utukufu wa milele” (M&M 130:2). ■

#### MUHTASARI

1. Robert D. Hales, “This Is the Way; and There Is None Other Way,” katika *Brigham Young University 1981–82 Speeches* (1982), 67.
2. Gordon B. Hinckley, “The Quest for Excellence,” *Liahona*, Sept. 1999, 8.

#### MAWAZO MUHIMU KUHUSU URAFIKI

“Chagua marafiki wanaoshiriki maadili yako ili uweze kuimarisha na kuhamsisha kila mmoja katika kuishi viwango vyajuu.

“Ili kuwa na marafiki wema, kuwa rafiki mwema. . . .

“Unapojitahidi kuwa rafiki kwa watu wengine, usipuuze viwango vyako.”

*Kwa Nguvu ya Vijana (kijitabu, 2011), 16.*



# Mwaliko **WANGU** kwa **WOKOVU**

Na Emerson José da Silva

**K**ama kijana, nilitembelea makanisa mengi na nilichanga-nyikiwa kwa sababu kila moja lilifundisha ufanuzi tofauti wa maandiko. Sikuhisi vizuri kuhusu utovu wa heshima nilipata katika baadhi yao, hivyo basi nikaacha kujaribu kutafuta kanisa la kuhudhuria.

Miaka kadhaa baadaye rafiki yangu, Cleiton Lima, alibatizwa katika Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Sikuza Mwisho. Hakunieleza haya hata vile tulivyokuwa marafiki wazuri, lakini muda ulivyoendelea, nilanza kuona mabadiliko ndani yake. Siku za Jumapili kwa kawaida nilienda nyumbani kwake asubuhi ili tuweze kucheza kandanda, lakini kamwe singempata nyumbani. Hii ilitokea Jumapili mbili au tatu mfululizo. Mwishowe Cleiton aliniambia kuwa hangweza kucheza



Kandanda tena Jumapili kwa sababu alikuwa akiheshimu siku ya Bwana. Nilimwambia, "Kanisa hili linakufanya uwe zuzu."

Kisha Cleiton akanialika kuhudhuria kanisa. Nilimpa udhuru kwa sababu nilikuwa bado sijihusishi na dini. Kwa miezi 10, Cleiton aliwaleta wamisioari kunifundisha, lakini daima nilitoa sababu au kuwaambia kuwa nilikuwa na shughuli sana. Lakini kamwe hakufa moyo.

Siku moja Juni, alinialika nihudhurie ngoma Kanisani. Nilimkejeli, "Je, kutakuwa na chakula ya bure na wasichana wengi?" Akicheka, alisema ndiyo!

Lazima nikubali kuwa nilishindwa na tumbo langu. Nilitembelea kanisa na kulipenda. Nilikaribishwa na kila mtu, nilikula sana, na nikawa na nia ya kuhudhuria mkutano. Nili-pofika kanisani Jumapili, nilikutana na watu wengi na kusikia ushuhuda

wao. Sikuwa na ufahamu wa Kitabu cha Mormoni, lakini nilihisi Roho wa Bwana wakati washiriki mbalimbali wa Kanisa walishuhudia, "Najua kwamba Kitabu cha Mormoni ni kweli, kwa-mba hili ni Kanisa la Yesu Kristo, na kwamba Joseph Smith alikuwa nabii aliyeitwa na Mungu." Nikuwa kamwe sijahisi vizuri kama hivi. Bado sikutaka kukutana na wamisionari, lakini mktano huo wa ushuhuda ulinigusa.

Wiki iliofuata, Cleiton alinialika tena kwenda kanisani. Sikuweza kwa sababu nilikuwa na wajibu mwingine. Ning-ona huzuni usoni mwake nilipomwambia sikujua kama ningeweza kwenda.

Hata hivyo, siku ya Jumapili asubuhi niliamka na hamu ya kwenda kanisani Niliamka saa 12:50 asubuhi, ambayo ilikuwa ni vigumu kwangu, na nilijitayarisha na kusubiri Cleiton aje. Alishangaa aliponiona nimevaa na nikisubiri. Jumapili hiyo Askofu alifundisha kuhusu ukuhani. Nilihisi Roho sana na nikawa na hisia kwamba nilipaswa kuchukua masomo ya wamisionari. Mwishoni mwa mkutano ya Wavulana, nilijua kwamba nitabatizwa.

Kanisa liliptomalizika,  
nilimuambia Cleiton,  
"Nataka kubatizwa!"

Alidhani nilikuwa na utani. Lakini, kisha akasema, "Nikiwaita wamissionari, je, utakutana nao?" Nilimjibu ndiyo.

Nilifundishwa na wamissionari wzuri. Niliposikia ujumbe wa Urejesho, nilipata uthibitisho hata zaidi kwa-mba nilifaa kubatizwa. Lakini nilitaka kujijulia mwenyewe ukweli wa Kitabu cha Mormoni. Wamisionari waliweka alama Moroni 10:3–5 katika Kitabu cha Mormoni changu na wakanialika kuomba na kuuliza Mungu kama ni kweli.

Jioni iliyofuata nilikumbuka kuwa bado sikuwa nimesoma Kitabu cha Mormoni. Nilipoanza kusoma, nilihisi roho kwa nguvu sana. Niliomba, na kabla nimalize, nilijua kwamba Kitabu cha Mormoni ni kweli. Namshukuru Mungu kwa kujibu maombi yangu. Nilibatizwa mnamo Julai 2006.

Baadaye nilihudumu kama mmisionari katika Misheni ya Brazil Cuiaba, na rafiki yangu Cleiton akahudumu katika Misheni ya Brazil Santa Maria. Tulifanya kile ambacho Cleiton alinifanya: kuwaalika watu kumjia Kristo na kuwasaidia kupokea injili ya urejesho kwa kufanya imani katika Yesu Kristo, kutubu, kubatizwa, na kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Hii kwa kweli ndio njia ya wokovu.

Daima tuwaalike marafiki zetu na jamaa kujifunza Injili hii, kwa kuwa Mwokozi alimwalika kila mtu alipo-sema, "Njoni kwangu" (Matthew 11:28). Najua kuwa hili ni Kanisa la Yesu Kristo na kwamba sasa ndio wakati wa kumkaribisha kila mtu kuja Kwake. ■



# NJIA KUMI ZA KUJUA KUWA **UMEONGOKA**

Na Tyler Orton

**N**ilijifunza katika mkutano wa ukuhani kwamba moja ya malengo ya Ukuhani wa Haruni ni kutusaidia “kuwa waongofu kwa injili ya Yesu Kristo na kuishi kwa mafundisho yake.”<sup>1</sup> Nilikuwa sina uhakika wa nini mana ya “kuwa waongofu kwa injili ya Yesu Kristo.” Niliwauliza wazazi wangu na ndugu wakubwa kile walichofikiria inamaanisha, na pamoja tulijadili idadi ya njia unawenza kuona kama unakuwa umeongoka.

Pengine kuna zingine, lakini hapa kuna njia 10 tulizotunga. Kwa vile uongofu ni mchakato wa muda wote wa maisha, si lazima tuwe wakamilifu katika kila sehemu hizi sasa, lakini inaweza kutusaidia kujua kama tunafanya maendeleo.

**1** Wakati umeongolewa, wewe *haujui* tu nini unatakiwa kufanya lakini pia una *hamu* ya kufanya mambo sahihi. Haitoshi tu kuepuka kufanya makosa kwa sababu una hofu ya kupatikana au kuadhibiwa. Wakati kweli umeongolewa, kweli unataka kuchagua mema.

**2** Ishara nyagine ya kuwa mwongofu ni kwamba hauna hamu tena ya kufanya makosa. Wapinga-Nefi-Walehi ni mfano mzuri wa hivi. Walipokuwa waongofu kwa Injili ya Kristo, “waliingia kwenye agano na Mungu kwamba watamtumikia, na kutii amri zake” (Mosia 21:31). Kama Wanefi waliofundishwa na Mfalme Benyamin, walikuwa “hawana tamaa ya kutenda maovu” (Mosia 5:2). Walikuwa kweli wameongolewa kwa Injili ya Kristo,

na majoribu ya Shetani hayakuwa na nguvu juu yao.

**3.** Wakati umeongolewa, unajihu-sisha zaidi na nini Mungu ana-fikiria kuliko kile wengine wanafikiria juu yako. Shulen i mwangu kule Indonesia, wanafunzi huwa wanakunywa sana. Wakati mwingine inaweza kuwa jaribio kwenda kwa burudani wakati kila mtu anafanya vile na kukukejeli kwa kukosa kuenda. Ndugu yangu alialikwa kunywa na kuburudika mara nyingi, lakini kamwe hakukubali—alismama kwa ajili ya kile alichoamini. Ilikuwa vigumu, na alibaki usiku

mara nyingi nyumbani peke yake. Wa-  
katika wanafunzi walikuwa wakimuaga  
katika mahafali yake, watu kadhaa  
walishiriki naye jinsi walivyoshanga-  
zwa kuwa aliweza kupinga shinikizo  
ya rika na kuwa mkweli kwa viwango  
vyake. Walimwambia jinsi walimtaza-  
mia kwa sababu ya hivyo. Alionyesha  
kuwa ameongolewa kwa kukataa  
shinikizo ya rika.

**4.** Unapoongolewa, unajaribu  
uwezavyo kuishi Injili daima—  
si tu Jumapili au wakati ni rahisi lakini  
wakati wote. Matendo yako hayaba-  
diliki kulingana na yule ambaye uko

pamoja naye au yule ambaye anawenza  
kuwa anakutazama. Wenzako wana-  
posema mambo mabaya au wanataka  
kutazama cinema chafu, haukulali tu  
kwa sababu hakuna anayekuangalia;  
badala yake unasimama kwa kile  
unachoamini.

**5.** Wakati umeongolewa, una zaidi  
ya wema na huruma katika uhusiano  
na watu wengine. Hauhukumu,  
wala hukosoi, wala umbeya. Una  
ufahamu zaidi ya hisia za wengine,  
na inakuwa ni kawaida kutafuta njia  
za kuhudumu na kusaidia. Ukiwa  
unatembea chini ya ukumbi wa shule




5.




### NJIA DHABITI YA FURAHÀ

"Bwana anataka washiriki wa Kanisa Lake kuwa waongofu kikamilifu kwa injili Yake. Hii ndio njia ya pekee ya uhakika ya kuwa na usalama wa kiroho sasa na furaha milele."

Mzee Donald L. Hallstrom wa Urais wa Wale Sabini, "Converted to His Gospel through His Church," *Liahona*, Mei 2012, 15.



6.




2.

*Ili kuonyesha kwamba wange-  
kuwa wakweli kwa ahadi yao ya  
kuishi injili, Walamani walio-  
ongolewa walizika silaha zao  
(ona Alma 24).*



7.



**10.** Wakati umeongolewa, una hamu kubwa ya kuwasaidia wengine kujua ukweli na furaha ambayo umepata. Mfano mzuri kutoka kwa maandiko ni ndoto ya Lehi, ambapo yeye alikuwa na hamu ya nguvu ya kushiriki tunda lenye ladha la mti wa uzima na familia yake. Alipokula tunda, wazo lake la kwanza halikuwa kula zaidi kwa ajili yake mwenyewe lakini kutafuta familia yake ili waweze pia kula tunda na kuwa na furaha sawa (ona 1 Nefi 8:12).

Kwa muhtasari, unajua kuwa umeongolewa unapoanza kuishi sheria ya juu, injili ya Yesu Kristo. Unaishi kulingana na madhumuni ya sheria na pia sheria ilivyoandikwa. Unaishi injili katika nyanja zote za maisha yako. Unaishi injili kwa ukamilifu wake, si kwa sababu unalazimika lakini kwa sababu unataka. Wewe ni mtu mwenye furaha na mwema zaidi, na unataka kuwa mtu ambaye Baba wa Mbinguni anataka uwe. Unataka kuwa kama Yesu Kristo na kufuata mfano Wake. Unapokuwa mtu huyo, kwa kweli umeongolewa. ■

*Tyler Orton anaishi Java, Indonesia.*

#### MUHTASARI

1. *Handbook 2: Administering the Church* (2010), 8.1.3.
2. Ezra Taft Benson, “Omba Kila Mara,” *Liahona*, June 1990, 4.

yako na mtu aangushe vitabu vyake, si lazima hata ufikirie juu ya nini cha kufanya. Unasimama moja kwa moja kusaidia.

**6.** Wakati umeongolewa, hamu yako ya kuomba huongezeka na unahisi kama unawasiliana kwa kweli na Mungu unapoomba. Daima utatenga muda wa kuomba bila kujali jinsi unavyojisikia au kile kinachoe-ndelea katika maisha yako. Rais Ezra Taft Benson (1899–1994) alituambia, “Kama hatuhisi kuomba, basi tunapawsa kuomba hadi tuhisi kuomba.”<sup>2</sup>

**7.** Wakati umeongolewa, unatamania Jumapili kwa sababu ni Sabato. Jumapili inapofika, badala ya kufikiri, “Eh, ni siku ambayo siwezi

kufurahia na marafiki zangu au kwendwa sinema, unafikiri, Vizuri, siku ambayo ninaweza kuhuduria kanisa na kuzingatia mambo ya kiroho na kufurahia muda na familia yangu!”

**8.** Wakati umeongolewa, unatii amri na hautafuti sababu, kurazinsha tabia, au kujaribu kupata maeneo yasiyowazi. Haujaribi kusongeza mipaka; unatii amri tu kwa sababu unajua ndiyo njia bora zaidi.

**9.** Wakati umeongolewa, unatamania kulipa sadaka yako. Unaiona kama upendeleo na kuhisi kwamba asilimia 10 si kwamba ni nyingi, hasa ikilinganishwa na baraka na kuridhika unakopata. Baraka hizi zina thamani ya zaidi kuliko fedha ulizolipa.

# KAZI NGUMU INAISTAHILI SANA

Utashangaa kile unaweza kutimiza kama utaendelea kujaribu.

(Ona Kwa Nguvu za Vijana [kijitabu, 2011], 40–41.)



# Wamisionari

## Wadogo wa Bibi Deny

Na Emilia Maria Guimaraes Correa

*"Mwanadamu anapozungumza kwa uwezo wa Roho Mtakatifu uwezo wa Roho Mtakatifu huyapeleka katika mioyo ya watoto wa watu." (2 Nefi 33:1).*

**V**ítor aliishi na mamake na dadake nyumbani mwa Bibi Deny. Bibiye Vítor akawa mgonjwa na hakuweza kuongoka kitandani mwake kwa wiki nyingi. Alikuwa na upweke katika chumba chake peke yake.

Vítor aliamua kwamba angeweza kumkalisha na Bibi Deny. Kila siku, alipofika nyumbani kutoka shule, alichukua nakala ya *Liahona* ndani ya chumba cha Bibiye na kumsomea hadithi kutoka kwa kurasa za watoto.

Baada ya kusoma nakala zote za *Liahona* ambazo familia yake ilikuwa nazo, alianza kumsomea Kitabu cha Mormoni na Biblia. Bibi Deny hakuwa mshiriki wa Kanisa, lakini alipenda kumsikiliza Vítor akimsomea. Alikuwa na furaha ya kujifunza injili.

Bibi aliuiliza maswali mengi. Kama Vítor hakujua majibu, angemuliza

mwalimu wake wa Msingi au ange-tafuta katika maandiko. Bibi alimuita Vítor mmisionari wake mdogo.

Bibi Deny alimwambia Vítor kwamba alikuwa amejifunza mengi kutoka kwake. Aliahidi kumba angeweza kuhudhuria kanisa pamoja naye atakapopona. Yale aliyokuwa amejifunza yalimfanya atake kupata nafuu na kujifunza zaidi kuhusu Injili.

Bibi alipopona, aliweka ahadi yake. Alienda kanisani kujifunza zaidi kuhusu yale aliyokuwa amemfundisha. Haikuwa muda mrefu kabla ya Bibi kubatizwa na kuthibitishwa. Vítor alikuwa amemsaidia kujifunza kwamba injili ni kweli.

Vítor alipokua, alikuwa mmisionari wa muda katika Misheni ya Boston Massachusetts. Kabla ya aondoke, alienda hekaluni—na Bibi Deny. ■

*Emilia Maria Guimaraes Correa anaishi katika Federal District, Brazil.*





Na Mzee M. Russell Ballard

Wa Jamii ya Mitume  
Kumi na Wawili

*Washiriki wa Jamii ya Mitume  
Kumi na Wawili ni mashahidi  
maalum wa Yesu Kristo.*

# Kwa nini Kanisa lina jina refu hivyo?

**Y**esu Kristo mwenyewe ali-lipa Kanisa jina (ona Mafundisho na Maagano 115:4).

Maneno *Kanisa la Yesu Kristo* yanatangaza kuwa ni Kanisa Lake.

*La Watakatifu wa Siku za Mwisho* yanaeleze kuwa ni Kanisa sawa ni

lile Kanisa Yesu Kristo alianzisha alipoishi duniani lakini limerejeshwa katika siku hizi za mwisho.

*Watakatifu* inamaanisha kuwa tunamfuata Yeye na kujaribu kufanya mapenzi Yake.

Washiriki wetu wameitwa *Wamormoni* kwa sababu tunaamini Kitabu cha Mormoni, lakini tunapaswa kutumia jina zima ya kanisa panapowezekana kila mara. ■

*Kutoka "Umuhimu wa Jina," Liahona,  
Nov. 2011, 79–82.*




Na Darcie Jensen

**W**akati Hekalu la Salt Lake lilikamilishwa mwaka 1893, Watakatifu wa Siku za Mwisho walifurahia. Ilikuwa imechukua miaka 40 ya kulijenga hekalu. Kwa sababu watoto walikuwa wamechanga fedha kusaidia kujeinga hekalu, Rais Wilford Woodruff aliamua kufanya vikao vitano nya kuweka wakfu maalum kwa ajili ya watoto kuhudhuria.

Leo mahekalu ni mengi duniani, na watoto bado husherehekeea kuka-milika kwa mahekalu. Angalia jinsi watoto wameshiriki siku hizo na sasa. ■

Darcie Jensen anaishi kule California, USA.

*Zaidi ya watoto 12,000 walikuja katika **Hekalu la Salt Lake** kwa uwekaji wakfu. Watoto hawa kutoka Kata ya Sugar House walipanda gari moshi.*



*Tikiti hii iliwaruhusu watoto wa umri hadi miaka 16 kuhudhuria mikutano maalum ya kuweka wakfu kwa ajili ya **Hekalu la Salt Lake**. Mitume na washiriki wa Urais wa Kwanza walihotubia watoto waliokuwa ndani ya hekalu.*



*Kila wiki kama **Hekalu la Gilbert Arizona** linajengwa, watoto wa Msingi kutoka Kigingi cha Gilbert Arizona Highland wameweka lengo kumtumikia mtu fulani katika kata zao.*



*Wakati mwingine mahekalu huwekwa wakfu upya baada ya kutengenzwa upya. Watoto wa msingi waliimba na kubeba mataa katika utendaji uliosherehekeea kuwekwa wakfu upya kwa **Hekalu la Anchorage Alaska**.*

*Wakati **Hekalu la San Diego California** lilijengwa, watoto wa Msingi kutoka Mexico walitenge-neza zulia la rangi nyingi kwa hekalu. Viongozi Wenyne Mamlaka walismama juu ya zulia wakati wa huduma ya jiwe la tao la pembedi katika kuwekwa wakfu.*



# Kusherekea Mahekalu!



*Watoto wa Msingi kutoka Manitoba, Kanada, walisafiri kwa gari masaa matatu kuenda **Hekalu la Regina Saskatchewan** kugusa kuta na kujitolea kwenda ndani siku moja.*

*Watoto wa Msingi katika ufunguzi wa **Hekalu la Kyiv Ukraine** waliwakaribisha wageni kwa kuimba "Napendelea Kuona Hekalu".*



*Zaidi ya 800 Watoto wa Msingi kutoka Afrika Magharibi waliimba "Mimi ni Mtoto wa Mungu" katika sherehe za kitamaduni kabla ya kuwekwa wakfu kwa **Hekalu la Accra Ghana**.*



*Kila hekalu lina jiwe la tao la msingi linaloonyesha mwaka liliwekwa wakfu. Wakati wa kuwekwa wakfu, Wenye Mamlaka Mkuu hufunga jiwe la tao la pembedi kwa simiti. Isaac B., umri miaka 9, alisaidia kuweka simiti juu ya jiwe la tao la pembedi la **Hekalu la Kansas City Missouri**.*



*Watoto wa msingi walimwimbia Rais Gordon B. Hinckley alipofika kuweka wakfu **Hekalu la Aba Nigeria**.*

# Maswali na Majibu ya Hekalu

## Kwa nini tuna mahekalu?

Mahekalu ya Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho ni mahali patakatifu ambapo sisi hujifunza ukweli wa kushughulika katika maagizo matakatifu.

## Ndani ya hekalu kuko vipi?

Hekalu ni mahali pa amani, pa heshima, na parembo. Kila kitu ndani ya hekalu ni kisafi na katika utaratibu mzuri. Kila mtu huvalia nguo nyeupe na huongea kwa sauti tulivu.

## Nini hufanyika hekaluni?

Mke anaweza kufunganishwa kwa mumewe, na watoto wanaweza kufunganishwa kwa wazazi wao.

Kufunganishwa huko huwezesha familia kuwa pamoja kwa milele. Katika hekalu, wanaume na wanawake pia hupokea kipawa cha baraka za kiroho kiitwacho endaumenti. Wanawea pia kupokea endaumenti na kufunganishwa kwa wale ambao walikufa bila kufanya maagano ya hekaluni.

## Nini kingine hufanyika katika mahekalu?

Licha ya kufunganisha na endaumenti, maagizo mengine hukufanyika mahekaluni. Watu wanaweza kubatizwa na kuitibitishwa kwa niaba ya wale ambao hawakuwa na uwezo wa kujunga na Kanisa walipokuwa hai. Unapofika umri wa miaka 12 na unastahili kuingia hekaluni, unaweza kuwa na nafasi ya kubatizwa na kuthibitishwa kwa niaba ya wale ambao walikufa bila Injili.

## Je, na kama familia yangu haijawahi kwenda hekaluni?

Baba wa Mbinguni anakujuua na kukupenda wewe na familia yako. Anataka kila mtu kuwa na baraka ya maagizo ya hekaluni. Ishi kustahili kuingia hekaluni. Weka lengo sasa kwamba utapokea endaumenti na kuo katika hekalu siku moja. Baba Yako wa Mbinguni atakubariki wewe na familia yako. ■



"Maafiki zangu vijana . . . , daima kuwa na hekalu katika mtazamo wako. Usitende chochote kitakachokuzuia kuingia malango yake na kushiriki baraka takatifu na za milele huko."

Rais Thomas S. Monson, "The Holy Temple—A Beacon to the World," *Liahona*, Mei 2011, 93.



# Familia Zinaweza Kuwa Pamoja Milele

(Iliyorahisishwa)

*Kwa uchangamfu* $\text{♩} = 80-96$ Maneno na Ruth Muir Gardner  
Muziki na Vanja Y. Watkins

Maneno na muziki © 1980 IRI. Mpango © 2012 IRI. Haki zote zimehifadhiwa.  
Wimbo huu unaweza kunakiliwa kwa ajili ya mahitaji, yasiyo ya kibashara ya matumizi kanisanii ama nyumbani.

# Yesu Kristo Alirejesha Kanisa Lake katika Siku za Mwisho



Unaweza kutumia somo hili na shughuli hii kujifunza zaidi kuhusu mada ya Darasa la Msingi la mwezi huu.

**F**ikiria kwenda kutafuta hazina. Ni wapi unaweza kutafuta hazina? Unaweza kuipata vipi? Je, kunaweza kuwa na sanduku la hazina? Ni nini kingekuwa ndani?

Baadhi ya masanduku ya hazina huwa na vito vizuri na sarafu za thamani. Lakini kama washiriki wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho, tuna hazina ambayo ni ya thamani zaidi: Injili ya Yesu Kristo.

Watu wengi hawajui kuhusu hazina hii, kwa hivyo mojawapo wa majukumu yetu ni kuishiriki na watu wengi iwezekanavyo.

Baada ya Yesu na Mitume wake kufa, baadhi ya mafundisho muhimu ya injili na maagizo yalipotea au

kubadilishwa, ikiwa ni pamoja na ubatizo, mamlaka ya ukuhani, mahekalu, manabii hai, na sakramenti.

Hazina hizi zote za injili zilirejeshwa kupitia Nabii Joseph Smith. Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo walimtoekea Joseph Smith katika Msitu Mtakatifu alipoomba kujua ukweli.

Baadaye Joseph alipata mabamba ya dhahabu na kuyatafsiri kuwa Kitabu cha Mormoni. Kitabu cha Mormoni kina mafundisho tunayothamini kwa sababu kinalezea kweli ambazo awali zilikuwa zimepotea. Tunapokea baraka nyingi kwa sababu tuna kweli hizi za injili.

Ni hazina za thamani jinsi gani! ■

MICHAEL NA BRYAN BEACH

## MAANDIKO NA WIMBO

- Mafundisho na Maagano 35:17
- "The Sacred Grove," *Kitabu cha Watoto cha Nyimbo*, 87 (au wimbo mwingine wa Urejesho wa injili)


## TUONGEE

Shiriki jinsi hazina za injili ya Yesu Kristo zinabariki familia yako.

## TENGEZA SADUKU LA HAZINA YA INJILI

Kata na ukunje sanduku hili la hazina kama ilivyo katika picha hapa chini.

Kata sarafu zinazoorodhesha baadhi ya hazina ambazo injili imekupa kisha ziweke ndani ya sanduku. Tazama hazina sandukini mara nyingi kujikumbusha mvényewe juu ya baraka za injili.



# Mahali ambapo Kanisa Lilianzishwa



Na Jan Pinborough

Majarida ya Kanisa

*Kuja pamoja nasi kugundua mahali pa umuhimu katika historia ya Kanisa!*

**K**ama Maggie na Lily E. wanataka kuona pale ambapo ambapo Kanisa lillianzishwa kwa mara ya kwanza, hawafai kuangalia mbali sana. Ni hapo tu mlangoni mwa kanisa katika Fayette, New York, ambapo wanaenda kanisani kila Jumapili!

Kanisa halikuanzishwa katika jengo la kanisa, lakini katika nyumba la mbao. Nabii Joseph Smith alikuwa amekuja kukaa hupo na familia ya Whitmer mnamo 1829. Nyumba ya asili haisimami tena, lakini chumba hiki cha mbao kipo mahali pale pale.


Jengo la kanisa ambapo Maggie na Lily huenda kanisani lina kituo cha wageni na maonyesho kuhusu nyumba ya Whitmer na mambo malum ambayo yalitendeka hapo. ■

*1. Joseph Smith alimaliza kutafsiri Kitabu cha Mormoni hapa.*





**2. Nje, si mbali na nyumba, wanaume watatu walimuona malaika Moroni na mabamba ya dhahabu. Wanaitwa Mashahidi Watatu kwa sababu walishuhudia, au kuona, mabamba. Unaweza kupata ushahidi wao mbele ya Kitabu cha Mormoni.**



**3. Mnamo Aprili 6, 1830, takriban watu 60 walikuja kwenye mkutano maalum. Joseph Smith alianzisha rasmi Kanisa, na sakramenti ilibarikiwa na kupitishwa. Huu ulikuwa ya mkutano wa kwanza wa sakramenti!**


## UBATIZO WAKATI ULE NA SASA

Maggie, 11, na Lily, 9, walibatizwa katika kidimbwi karibu na mahali ambapo washiriki wa kwanza wa Kanisa walibatizwa.

Wasichana wote walifurahia sana kubatizwa. Ilipofika zamu ya Lily kubatizwa, alikuwa na mahojiano na Askofu wake. "Aliniuliza kama nilikuwa na ushuhuda wa nabii na kama nilikuwa nikilipa sadaka," alisema Lily.

Wasichana wote wana kumbukumbu mzuri ya siku zao za ubatizo. "Nilipotoka nje ya maji, nihiisi kuwa ningeweza kufanya chochote," Maggie alisema.

Wasichana wote walipata shajara ili waweze kuandika hisia zao juu ya siku yao maalum.



**4. Mara tu baada ya mkutano, wazazi wa Joseph Smith na watu kadhaa wenye walibatizwa nje.**

# Max na Mia Waokoa Siku

Na Chris Deaver, Texas, USA



Max alijiandaa kucheza shujaa jasiri. Alivaa t-shati yake nyekundu Alivaa kofia yake ya shujaa jasiri. Kisha akaenda chumbani mwa dadake mdogo.

“Njo Mia,” alisema Max. “Twende tukaokoe siku!”



Max na Mia walienda  
sebuleni. Waliona ndoo imejaa  
nguo.

“Mtanisaidia?” aliuliza Mama.  
“SAWA,” Max akasema.  
“Kisha twende  
tukaokoe siku.”




Max na Mia walimsaidia  
Mama kukunja nguo zote  
na kuziweka kando.

Kisha Max akaona takataka  
kiasi kwenye sakafu.  
“Tuokote takataka zote,”  
alisema Max. “Kisha twende  
tukaokoe siku.”

Max na Mia wakashindana kote nyumbani. Wakatupa takataka zote walizoweza kupata.

Walimuona Mama akifagia sakafu ya jikoni “Tunaweza kukusaidia,” Max alisema.

Mia alishikilia kiokota taka Max akifagia sakafu.



“Sasa twende tukaokoe siku,” Max alisema.

Mama alitazama kote katika nyumba safi. Kisha akawakumbatia Max na Mia. “Nafikiri tayari mmeokoa siku!” ■



### YESU ANATEMBEA JUU YA MAJI

“Wanafunzi walipomwona akitembea juu ya bahari, wakafadhaika, wakisema, Ni kivuli; wakapiga yowe kwa hofu.

“Mara Yesu alinena, akawaambia, Jipeni moyo; ni mimi; msiogope”  
(Mathayo 14:26–27).

# HABARI ZA KANISA

Nenda kwa [news.lds.org](http://news.lds.org) kwa habari zaidi za Kanisa na matukio.

## Mafunzo ya Uongozi Duniani Kote—Mbinu Mpya



**Mzee L. Tom**

**Perry, Mzee**

**Donald L.**

**Hallstrom, na**

**Askofu Dean M.**

**Davies wana-  
ongoza jopo la  
mjadala juu ya  
umuhimu wa  
kutumia funguo  
za ukuhani.**

**K**atika miezi ijayo, washiriki wa Kanisa ulimwenguni watashiriki katika mfumo mpya wa maongozi ya Mafunzo ya Uongozi Duniani Kote.

Tofauti na mikutano ya awali ya mafunzo, Mafunzo ya Uongozi Duniani Kote ya mwaka huu hayatatangazwa kama tukio moja kwa ajili ya viongozi wa kata na vizingi. Badala yake, yatagawanywa katika vipingili tisa vifupi—katika DVD na kwenye LDS.org—ambayo inahimiza majadiliano na viongozi wote, washiriki, na familia mwaka ujao mzima na baadaye.

Lengo la mafunzo ni Kuimarisha Familia na Kanisa kuititia Ukuhani. Katika mafunzo, washiriki wa Urais wa Kwanza na Jamii ya Mitume Kumi na Wawili, pamoja na Viongozi wengine Wenye Mamlaka na maafisa wakuu, wanatoa maelekezo ya kuvutia juu ya:

- Jinsi familia zinaweza kupata nguvu na amani kuititia uwezo wa ukuhani.
- Jinsi ya kusaidia kila familia kuwa na uzoefu wa baraka za ukuhani.
- Jinsi wenye funguo za ukuhani wanaimarisha nyumba na familia.

- Jinsi ya kushiriki kwa njia za Kikristo
- Jinsi ya kuwalea watoto katika nuru na ukweli.

Vitengo vyote vya Kanisa vitapokea nakala za DVD, na mabaraza ya kata na vizingi yanaombwa yazitazame kikamilifu. Kisha wanapaswa kushauriana kuhusu jinsi ya kusaidia washiriki wa kata na kigingi kufaidika kutohana na mafundisho.

Katika mikutano na madarasa, washiriki wanaweza kutazama na kujadili vipingili vya DVD. Familia na watu binafsi wanaweza kutazama vipingili, pamoja na nyenzo za ziada ili kuboresha masomo yao, katika [wwlt.lds.org](http://wwlt.lds.org).

Katika kila mazingira, sehemu yenye umuhimu zaidi ya mafunzo itatokea baada ya kukamilika kwa kipingili na mjadala kuanza. Viongozi, washiriki, na familia wanapotafakari, kushiriki, na kushuhudia kuhusu walichokisikia na kuhisi, Roho Mtakatifu atawavutia na kuwfundisha jinsi ya kutumia mafundi-sho katika mazingira yao wenye. Kupitia uzoefu huu, Mafunzo ya Uongozi Duniani Kote haya yata-saidia kuimarisha familia na Kanisa duniani kote. ■

**Wakiwa wamesimama nje ya nyumba ya Mary Fielding Smith katika "This Is the Place Heritage Park", Mzee M. Russell Ballard, Linda K. Burton, Mzee Ronald A. Rasband, Elaine S. Dalton, Rosemary M. Wixom, na Askofu Gary E. Stevenson wanajadili baraka za kuwa na ukuhani katika kila nyumba.**



## KUITIKIA WITO KWA WAMISIONARI ZAIDI:

# Kukuza Mawazo ya Umisionari Nyumbani na katika Kanisa

Na Heather Whittle Wrigley

Habari za Kanisa na Matukio

**A**skofu Victor Nogales wa kata ya Parque Chacabuco, kigingi cha Buenos Aires Argentina Congreso ameketi mbele ya ubao ya matangazo akiwa amefunika na picha za wauvulana na wasichana 37 katika kata yake. Wakati mmoja wao anaondoka kuenda misheni, yeche huandika maneno kando ya picha.

Vijana wangu hufurahia wanapokuja ofisini mwangu na kuona picha na maneno, alisema. Inawatia moyo kujitayarisha kwa ajili ya misheni zao wenyewe.

Kata hii katika Buenos Aires ina-elekeza roho ya kazi ya umisionari. Katika miezi sita za kwanza ya 2012, vijana 19—14 wakiwa waongofu—waliwacha nyumba zao ili kuhudumu misheni ya muda katika mataifa nane. Zaidi ya asilimia 80 ya vijana wanaostahili wamejitelea kuhudumu misheni.

Katika miaka ya hivi majuzi viongozi wa Kanisa wametoa maombi kadhaa kwamba vijana wengi zaidi wahudumu misheni.

Wakati wa mkutano mkuu wa Aprili 2005, punde tu baada ya Kanisa kutoa *Hubiri Injili Yangu: Mwongozo wa Huduma ya Umisionari*, Mzee M. Russell Ballard wa Jamii ya Mitume Kumi na Wawili

alishauri familia na viongozi kukuza roho ya umisionari na kuandaa wavulana na wasichana zaidi kumtumikia kwa heshima kwa kuwasaidia kuelewa wao ni nani na kwa kuwafundisha mafundisho (ona “One More,” *Liahona*, Mai 2005, 69).

Tangazo la Rais Thomas S. Monson wakati wa mkutano mkuu wa Oktoba 2012 kwamba mipaka ya umri ya umisionari ingepunguzwa lilifanyanyika kama ukumbusho mwingine kuwa Bwana anaharakisha kazi Yake.

Leo familia nyingi na viongozi wenyeji wa Kanisa wanachukulia ujumbe huu moyoni na kuanzisha desturi nzuri ya huduma ya umisionari katika maeneo yao.

### Kuwasiadia Vijana Kuelewa Wao ni Kina Nani

Kwa kujibu swalii hili, Umewezaje kuwatayarisha vijana wengi kuwa tayari kuhudumu? Askofu Nogales alijibu, Nilipoitwa kama askofu, jambo la muhimu la kwanza lilikuwa vijana wa kata yangu, na niliifanya kuwa wazi kwa viongozi wengine wa kata kwamba tulihitajika kuwa sehemu ya maisha yao.

Kwa mfano, kila mmisionari wa Chacabuco alikuwa na wito katika kata kabla ya kuondoka

kwao. Mara nyingi waongofu wapya na washiriki wasioshiriki kikamilifu walialikwa kuhudumu kama walimu, jambo ambalo liliwasaidia kujitayarisha kufundisha injili.

Askofu Nogales pia alipangia vijana kuijandaa kiroho kwa ajili ya misheni kwa kufanya kazi pamoja na wamisionari wa muda wa kwao.

Viongozi wa Kanisa na washiriki wanavyojitelea wenyewe kwa ajili ya vijana wa kata, wamezawadiwa kwa kuona roho ya umisionari ikikua sana.

### Familia Yenye Wazo ya Umisionari

Garth na Eloise Andrus wa Draper, Utah, Marekani, wanajua inamaanisha nini kuwa na familia yenye wazo la umisionari. Wao wana wajukuu 17 ambaao wameshiriki misheni, na wameshiriki misheni sita wao wenyewe.

Kukuza roho ya huduma ya umisionari katika familia yako ni kitu ambacho huanza kutoka wakati watoto ni wadogo, Ndugu Andrus alisema.

Dada Andrus alikubali. Hauwachi kushiriki misheni kuwa matarajio ya kimya, lakini unawazungumzia watoto wako na wajukuu kuihusu ni kama vile swalii ni—*wakati* gani utaenda misheni yako, si *kama* alisema.

Kufundisha vijana wao ni kina nani kwa kuweka mfano wa huduma ya umisionari ni muhimu pia. Ndugu na Dada Andrus walipokea wito wao wa kwanza mnano 1980, punde tu mtoto wao mdogo alipokuwa akiondoka kuenda misheni yake.

Mjukuu moja aliwandikia baada ya kupokea zawadi waliomtumia



**Askofu Victor Nogales anasimama karibu na ubao wa matangazo ambao unaonyesha vijana wote wa kata yake, ikiwa ni pamoja na wale ambao kwa sasa wanahudumu misheni.**

kumsaidia kuijandaa kwa ajili ya misheni yake. “Alituomba [zawadi], lakinii akasema, ‘Ya muhimu zaidi ni kuwashukuru kwa mfano ambao mmeweka,’” Dada Andrus alisema.

### Kufundisha Mafundisho

“Vijana wetu wana haki ya kutarajia kwamba wazazi wao na viongozi wa Kanisa na walimu watahakikisha kwa mba wanajua na kuelewa injili ya Yesu Kristo,” Mzee Ballard alisema. “Roho Mtakatifu atathibitisha ukweli kwa miyo yao, na atawasha Nuru ya Kristo katika roho zao. Na kisha utakuwa na mmisionari *moja zaidi* ambaye atakuwa tayari kikamilifu” (M. Russell Ballard, “One More”, 71).

Maili 6000 (9600 km) kutoka

Buenos Aires, tawi la kijijini la Horseshoe Bend karibu na Boise, Idaho, Marekani, pia limeshuhudia ongezeko kubwa la huduma ya umisionari wakati familia na viongozi wakiweka mkazo juhudhi za kufundisha injili kwa vijana wao.

Kutoka tawi dogo la washiriki 75, vijana tisa wanahudumu misheni.

Mzee Russell M. Nelson wa Jamii ya Mitume Kumi na Wawili alisistiza sababu na faida ya kuhudumu. “Wamisionari wote hutumikia kwa matumaini ya pekee ya kufanya maisha yawe bora kwa watu wengine alisema. Uamuzi wa kuhudumu misheni utajenga hatima ya kiroho ya mmisionari, mume au mke wake na dhuria zao kwa vizazi vijavyo. Hamu

ya kuhudumu ni matokeo asili ya uongofu wa mtu, ustahili, na maandalizi” (“Ask the Missionaries! They Can Help You!” *Liahona*, Nov. 2012, 18).

Martin Walker, rais wa kigingi cha Emmett Idaho, alikubali. Kuhudumu katika misheni humweka kijana katika njia ambayo itaathiri vizazi, alisema. Kama kigingi, tunafanya kila kitu tunachoweza ili kuwatayarisha vijana kwa ajili ya huduma ya umisionari.

Sehemu ya maandalizi hayo inajumuisha kuwafunza vijana mafundisho. Vijana katika tawi la Horseshoe Bend wana darasa la kila wiki la maandalizi ya umisionari linalofundishwa na rais wa zamani wa misheni—mafunzo ambayo yanajaliza mafunzo yaliyotolewa na mkutano wa kigingi wa kila mwezi wa vijana wa maandalizi ya umisionari na Kambi yake ya kila mwaka ya Ukuhani ya Haruni.

LaRene Adam—mmoja wa watoto sita wa Ndugu na Dada Andrus—alihudumu pamoja na mmewe, Jim, katika Misheni ya Copenhagen Denmark kutoka 2007 hadi 2009. Yeye alishuhudia umuhimu wa kuwafundisha watoto injili nyumbani.

“Mojawapo wa mambo makuu unayoweza kufanya ili kuwasaidia watoto wako kujenga ushuhuda wa kazi ya umisionari ni kufanya mkutano wako wa jioni ya familia nyumbani na kujifundisha maandiko na familia,” alisema. “Ukiwapa msingi huo dhabitwa kujifundisha injili na ufahamu wa injili, wanakuwa tayari zaidi na wanajua mengi zaidi kuhusu Injili.” ■

# Vijana Wamisionari wa Huduma wa Kanisa Wapata Furaha katika Huduma

Na Carolyn Carter

Habari za Kanisa na Matukio

Mzee Ernesto Sarabia alivaa baji nyeusi ya umisionari kila siku ya misheni yake. Lakini misheni yake ilikuwa tofauti na ya watu wengine wengi—Mzee Sarabia alihudumu kama Vijana Wamisionari wa Huduma ya Kanisa (VMHK) katika ofisi ya Misheni ya Mexico Hermosillo.

Tunatambua kwamba huenda kuwa si busara kwa baadhi ya vijana wetu na wasichana kukabiliana na ugumu na changamoto za misheni ya muda, Mzee M. Russell Ballard wa Jamii ya

Mitume Kumi na Wawili amesema. Lakini hii, alisema, haimaanishi hawawezi ku-shiriki katika baraka za huduma za umisionari (“One More”, *Liahona*, Mei 2005, 69).

Mzee Russell M. Nelson wa Jamii ya Mitume Kumi na Wawili, alisema,

Kuhudumu misheni ni kitendo cha huduma ya kujitolea kwa Mungu na wanadamu (“Ask the Missionaries! They Can Help You!” *Liahona*, Nov. 2012, 18), na kuna njia nyingi za kutoa huduma hio.

Kwa wale ambao wamekubaliwa kwa heshima kutohudumu misheni ya kuhubiri ya muda, ama kwa wale ambao ni lazima warudi nyumbani mapema, mpango ya VMHK una-weza kutoa uzoefu wa maana wa misheni.

## Mahitaji ya Kuhudumu

Wa VMHK ni lazima wawe na uwezo wa kimwili, kiakili, kiroho, na kihisia ili kutekeleza kazi za wito wao, ambao wanalinganishwa kwa makini.

Kazi ya VMHK inakuwa kutoka miezi 6 hadi 24 na inaweza kuwa na anuwai kuanzia kuhudumu kwa siku kadhaa za wiki hadi kufanya kazi kwa muda mzima. Kuna nafasi za kuhudumu katika jamii na pia kutoka nyumbani. Uwezekano wa kazi za VMHK inajumuisha utafiti wa historia ya familia, teknologia ya habari, wasaidizi wa ofisi ya misheni, hifadhi za askofu, na zaidi.

## Uhimili wa Familia na Ukuhani

Wazazi, viongozi wa ukuhani, na washiriki wa Kanisa wanaweza

kusaidia wa VMHK kujiardaa kutumika misheni.

Familia changa ya Dada Eliza Joy Young imekuwa msaada wa nguvu kwake, kumwendesha kwa gari hadi na kutoka ofisi za Kanisa katika Sydney, Australia.

Mzee Michael Hillam, ambaye ana-fanya kazi katika Kituo cha Usambazaji cha Hong Kong, alisema, “Walimu wangu wa seminari ya asubuhi mapema na viongozi wa Wavulana hunisaidia kujiardaa.”


## Dhabihu Huleta Baraka

Dada Young alijitolea siku zake za mapumziko kutokana na ajira yake ili kuhudumu Misheni ya Huduma ya Kanisa. Alisema, “Najisikia karibu na Baba yangu wa Mbinguni nikija kwa-mba ninamsaidia.”

Kama ziada ya baraka za kiroho, kuhudumu misheni ya Huduma ya Kanisa huwapa wamisionari vijana fursa muhimu ya kijamii na kitaaluma. “Misheni yangu imenionyesha kwamba ninaweza kufanya kazi katika ajira ya huria,” Dada Young alisema. (Alikuwa awali amefanya kazi tu katika ajira ya kusaidiwa.)

Ingawa si vijana wote wazima ambao wangependa kuhudumu wanaweza, juhudhi kubwa zinafanywa kuweza ku-chukua kila kijana mzima mwenye kustahili. Wavulana na wasichana ambao wangependa kuhudumu katika njia hii wanaweza kuongea na askofu wao ama rais wa tawi, ambaye anaweza kupata fursa mwafaka kwa ajili yao.

Soma zaidi katika news.lds.org young church-service missionaries. ■



# Viongozi Wakuu wa Wasichana na Muungano wa Usaidizi wa Kina Mama Wanazuru Eneo la Asia

**Na Brenda Frandsen, mtaalamu wa vyombo vya habari Eneo la Asia**

Kwa michango kutoka kwa Daudi O. Heaps, Paul Stevens, na Linda Rae Pond Smith

**K**wa siku tisa Novemba 2012, Mary N. Cook, mshauri wa kwanza katika urais mkuu wa Wasichana, na Linda S. Reeves, mshauri wa pili katika urais mkuu wa Muungano wa Usaidizi wa Kina Mama, walifundisha na kuvutia akina dada vijana kwa wazee kote katika Eneo la Asia.

Safari ilienda sambamba na tangazo ya marekebisho ya mtaala wa vijana, *Njo, Mnifuateni*, ambayo Wavulana, Wasichana na Shule ya Jumapili ya vijana itaanza kutumia Januari 2013. Mtaala mpya imeundwa kusaidia walimu kufundisha zaidi kama Mwokozi alivyofundisha na kuendeleza uhusiano bora zaidi na washiriki wa darasa.

Kufuatia safari ya Dada Cook na Dada Reeves katika Eneo la Asia, vijana wengi wa Kiasia na wazazi wao walifakari kuwa walikuwa na motisha zaidi kutakasa na kuelekeza maisha yao na kuwa mifano kwa jamii zao.

Mjini Hong Kong, Dada Reeves aliahidi vijana, “Ukibaki kuwa msafi katika maisha yako, unaweza kusimama kwa kujiamini mbele ya mtu yejote!”

Akiwa amevutiwa na maneno yake, Tang Kak Kei wa umri ya miaka 12 alinena baada ya mktano, “Najua kwamba ninafaa kusoma Kitabu cha Mormoni kila siku. Kujifunza kutubu na kuishi kwa wema ndio kile *Kwa Nguvu ya Vijana* imenifunza kufanya ili Nuru ya Kristo na furaha ya kweli iweze kung’ara kupitia kwangu.”


Nchini India, Dada Cook alikutana na washiriki katika jumba jipya la mkutano katika Wilaya ya Chennai India na washiriki wa kigingi kipywa Hyderabad India na aliwashauri vijana kuijandaa kwa ajili ya siku zijazo. “Jiitimisheni wenyewe kielimu,” alitoa wito, “na ujuzi wa kukusaidia kujenga ufalme. Zingatia familia yako na kile unaweza kufanya ili kubariki wanafamilia wako, na kwa maandalizi yako ya kiroho ili uwe mstahiki wa ushawishi wa kiroho na ili ujue mahali pa kwenda na jambo la kufanya.”

Nchini Indonesia, Dada Reeves alishiriki katika mkutano wa kwanza wa kigingi wa Kigingi cha Surakarta Indonesia kipywa. “Tulihisi roho zao nye-nyekevu na zenye upendo. Washiriki waaminifu vipi!” alisema.

Dada Reeves kisha akatemebelea Malaysia, ambapo alijadili na kundi la akina dada wa Muungano wa Usaidizi wa Kina Mama, masuala makubwa zaidi ya Muungano wa Usaidizi wa Kina Kama kama shirika katika Malaysia na jinsi Kanisa linaweza kutoa mwongozo na msukumo.

Nchini Taiwan, Dada Reeves alinena kuhusu nguvu na kujitolea kwa washiriki huko. “Tunafurahia sana kujua kuhusu maisha yao ya uaminifu na uendaji kwao hekaluni kwa udhabiti. . . . Washiriki hao ni mfano wa kupendeza kwa marafiki zao na majirani,” alisema. ■





**Vijana duniani kote waonyesha jinsi wanavyosi-mama katika maeneo matakatifu.**

**Tangazo la Picha za Vijana**

Mada ya Mutual mwaka huu ni "Simameni katika mahali pa takatifu na wala msiondoshwe" (M&M 87:8). Wavulana na wasichana, *Liahona* inatafuta picha zenu mkiwa mmumesimama katika maeneo matakatifu. Picha zinaweza kuonyesha ukiwa na familia, ukihudumu, ukifanya kazi ya umisionari, ukitengeneza sanaa, kusoma Injili, kuchunguza mazingira, na zaidi! Hivi ndivyo unavyotuma picha yako:

- Acha mtu akupige picha ukiwa umesi-mama mahali pa takatifu.
- Tuma picha yako ya ubora wa juu kwa [liahona@ldschurch.org](mailto:liahona@ldschurch.org).
- Ongeza ujumbe kuhusu kwa nini mahali hapa ni pa takatifu kwako.
- Katika barua pepe yako, jumuisha jina lako kamili, siku ya kuzaliwa, jina la kata na kigingi (ama tavi na wilaya), na anwani ya barua pepe ya wazazi wako.

Picha za vijana kutoka duniani kote zitawekwa katika toleo lijalo.

**Mtume Anazuru Morocco**

Mnamo Desemba 2012, baada ya kuunda kigingi cha 3000 cha Kanisa kule Sierra Leone Afrika Magharibi, Mzee Jeffrey R.

Holland wa Jamii ya Mitume Kumi na Wawili alitembelea tawi dogo la Kanisa lililo mbali kule Rabat, Morocco.

Katika ibada maalum ya Jumapili jioni, Mzee Holland alishiriki upendo ambao viongozi wa Kanisa wanao kwa kila mshiriki wa Kanisa duniani kote, bila kujali jinsi walivyo wachache au umbali wa mahali walipo.

"Hamjasaulika, na ninyi ni sehemu ya kazi ya ajabu kama vile Bwana hubainisha na kuharakisha kukusanyika kwa Israeli katika kipindi hiki kikuu cha mwisho," alisema.

**Hekalu la Tegucigalpa Honduras Liwekwa Wakfu**

Jumapili wa Machi 17, 2013, kufuatia sherehe za kitamaduni na wiki tatu za kukaribisha wageni, Hekalu la Tegucigalpa Honduras liliwekwa wakfu katika vikao vitatu, ambavyo vilitangazwa kwa vitengo vyote vyta Kanisa katika Honduras na Nicaragua.

Washiriki wa Honduras, ambao kwa kawaida wamekuwa wakisafiri masaa mengi kwenda Guatemala kwa Hekalu la Guatemala Mjini, walifurahi kuona hekalu la kwanza nchini likiwekwa wakfu. Hekalu lilitangazwa kwa mara ya kwanza na Urais wa Kwanza katika barua ya Juni, 9, 2006, na ardhi ilichimbiliwa katika uwanja huo mnamo Septemba 12, 2009.

**Rais Monson Azuru Ujerumani**

Mwishoni mwa mwaka 2012 Rais Thomas S. Monson alisafiri kwenda Ujerumani kukutana na washiriki wa Kanisa Hamburg, Berlin, Munich, na Frankfurt, Ujerumani, na kuwashimiza wamfuate Yesu Kristo.

Alifunza msamaha kwa njia ya kusamehe, aliwaambia washiriki kule Frankfurt. Alifunza huruma kwa kuwa na huruma. Alifundisha ibada kwa kujitolea Mwenyewe.

**Roho Mtakatifu Hunifundisha Mimi**

Tangu familia yangu kujiunga na Kanisa, nimeona nguvu inayokuja kutokana na kusoma *Liahona*. Ni kuitia maneno haya ya kina ndio kwamba nilishawishika kuhudumu misheni. Mada nyingi hujadiliwa katika gazeti, lakini kinachojalisha kwangu ni yale ambayo Roho Mtakatifu hunifundisha kila wakati ninapokisoma. Hakika, tutakuwa huru—hata katika “eneo la adui” (ona Boyd K. Packer, “How to Survive in Enemy Territory,” *Liahona*, Oct. 2012, 24)—tunapojojfunza, tunaposoma, na kutumia kanuni zinazofundishwa. Mwokozi yu hai, ukuhani u duniani, na Mungu yu mbinguni.

**Newton T. Senyange, Uganda**

**Marekebisho**

Oktoba 2012 *Liahona* kimakosa ilihu-sisha picha katika hadithi “First Stake in India Organized” kwenye kurasa 76–77. Picha zilipigwa na Dada Gladys Wigg. Tunaomba radhi kwa makosa.

Katika *Liahona*, ya Desemba 2012 familia ya Vigil, ilojadiliwa katika mala “Sacred Transformations” katika ukurasa wa 36, ilibatizwa mnamo Julai 2010, si Juni 2011. Pia, Andrea Vigil alizaliwa mnamo Julai, si Agosti, 2012.

Katika *Teachings of Presidents of the Church: Lorenzo Snow*, picha katika ukurasa wa 2 imepatiwa jina lisilo sawa. Ni picha ya mwanawe Rais Snow, Oliver Goddard Snow. Pia, katika maelezo mapupi kwenye ukurasa wa 28 majina ya Brigham Young Jr. na Francis M. Lyman yanapaswa kubadilishwa.

# KUNYWA KUTOKA CHEMACHEMI

Na Aaron L. West

Mhariri, Huduma za Uenezi za Kanisa

Tunapozungumzia kuhusu uzuri wa hekalu, kwa kawaida sisi hutaja minara, madirisha, na picha. Sisi huzungumzia kwa heshima juu ya vidimbwi vya ubatizo, vyumba vya endaumenti, vyumba vya maunganisho, na vyumba vya selestia.

Lakini wakati nabii huweka wakfu hekalu kwa Bwana, ye ye huweka wakfu jumba lote, si tu sehemu nzuri ambazo kila mtu huona. Katika maombi ya kuweka wakfu Hekalu la Kansas City Missouri, Rais Thomas S. Monson alisema: “Tunaweka wakfu ardhi ambayo hekalu hili linasimama. Tunaweka wakfu kila sehemu ya muundo huu mzuri, kutoka kwa misingi usioonekana hadi kwa sanaa ya ajabu ya Moroni inayokaa kwenye kilele chake cha juu kabisa.”<sup>1</sup> Wakati Rais Joseph Fielding Smith alitamka sala ya kuweka wakfu juu ya Hekalu la Ogden Utah, aliweka wakfu “misingi, kuta, sakafu, paa, mnara, na maeneo yote ya jengo,” na aliomba kwa ajili ya ulinzi wa “sehemu zote za kimitambo, mfereji ya mataa na vifaa, shine ya hewa na lifti, na mambo yote yanayohusu jengo hili.”<sup>2</sup>

Ninashukuru kwamba Bwana huwashawishi manabii Wake kuweka wakfu kila sehemu ya hekalu. Ingawa bawaba la mlango au kiegezi mwanga kwa wazi kina lengo dogo kuliko



*Yesu Kristo ni chemchemi ya maji ya uzima.*

madhabahu katika chumba cha maunganisho, vile vipande vidogo vinachangia kusudi kuu la hekalu la kutukuza.

Mojawapo wa vipande hivi vidogo vimenisaidia kujifunza somo la kudumu. Nilikuwa katika Hekalu ya Salt Lake siku moja, nikijiandaa kutoka chumba cha kuvalia baada ya kushiriki katika agizo kwa niaba ya wafu. Kuona chemchemi ya maji ya kunya, nikatambua kuwa nilikuwa na kiu, kwa hivyo nikainama chini kwa ajili ya kunywa haraka. Ujumbe ukaja akilini mwangu:

*Wewe hunywa maji haya katika hekalu, lakini je, kweli wewe hunywa maji hai ambayo yanapatikana hapa?*


Haikuwa hukumu ya nguvu—wala tu uke-meo mpole na swali la kupena roho.

Jibu langu kwa swali hilo lilikuwa ni hapana. Sikuwa kabisa kimilifu nikinywa maji ya uhai ya hekalu. Ilinibidi nikubali kuwa akili yangu ilitanga dakika chache awali nilipo-kuwa nikipokea maagizo kwa niaba ya wafu. Ingawa nilikuwa nimefanya kazi nzuri kwa niaba ya watu waliohitaji msaada wangu, sikuwa nimejiruhusu kupokea msaada wote niliohitaji.

Sasa, kila wakati mimi huenda hekaluni, mimi hutafuta chemchemi ya maji ya kunywa na husimana kwa ajili ya kunywa. Mimi hujiuliza mwenyewe jinsi kwa undani mimi hunywa kutoka katika chemchemi ya maji hai. Jibu langu: Bado si kwa kina vya kutosha. Lakini kiu changu kinaongezeka. ■

## MUHTASARI


- Thomas S. Monson, katika “Kansas City Missouri Temple: ‘Beacon of Divine Light’—an Offering of Hands and Hearts,” *Church News*, Mei 12, 2012, ldschurchnews.com.
- Joseph Fielding Smith, katika “Ogden Temple Dedication Prayer,” *Ensign*, Mar. 1972, 12.



MCHORO NA ROBERT T. BARRETT

## **WILFORD WOODRUFF**

**Wilford Woodruff** alihudumu misheni kule Great Britain miaka ya 1840s. Kwa sababu ya utumishi wake, zaidi ya watu 1,000 walibatizwa Wilford Woodruff alihudumu baadaye kama rais wa **Hekalu la St. George Utah**. Kama Rais wa Kanisa, alitetea kwamba **Utah** ifanywe kuwa jumbo. Alipokea pia ufunuo na kutoa **Tamko Rasmi 1** likiwaelekeza Watakatifu kuacha kuwa na ndoa za mitala.



*W*aigizaji wanaonyesha ma-  
ndhari kutoka kwa maisha  
ya Yesu Kristo kwa video  
zinazodhibitiwa na kompyuta kuu  
katika biblevideos.lds.org; maonyesho  
kadha kutoka kwa wiki za mwisho za  
maisha ya Mwokozi yanaonyeshwa  
katika makala kwenye ukurasa wa 26.  
Katika "The Mission and Ministry of Jesus  
Christ" (ukurasa 18), Mzee Russell M.  
Nelson anafundisha maswala manne ya  
huduma ya Mwokozi ambayo tunaweza  
kuiga katika maisha yetu wenywewe.

KANISA LA  
**YESU KRISTO**  
LA WATAKATIFU  
WA SIKU ZA MWISHO